

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 26 Juni, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Tukae.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU WA MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (*The Finance Bill, 2019*).

MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:-

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (*The Finance Bill, 2019*).

MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:-

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (*The Finance Bill, 2019*).

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI:- KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, sasa aulize swali lake.

Na. 459

Mikataba ya Ajira kwa Madereva wa Malori na Mabasi

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasimamia na kuhakikisha Madereva wa Malori na Mabasi wanapata Mikataba ya Ajira ili kuboresha maslahi yao na kuongeza ufanisi katika Utumishi wao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia haki na maslahi ya Madereva nchini Tanzania, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto zinazowakabili madereva ambapo mnamo tarehe 2 Mei, 2015 Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliagiza iundwe Kamati ya Kudumu ya Kutatua Matatizo katika Sekta ya Usafirishaji chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Uchukuzi. Aidha, Kamati ndogo chini wa Uenyekiti wa iliyokuwa Wizara ya Kazi na Ajira iliundwa kwa ajili ya kushughulikia haki, maslahi na mkataba wa ajira wa Madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi Madereva na Viongozi wa Umoja wa Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji nchini waliufanyia marekebisho na kuuboresha Mkataba wa ajira wa Madereva uliokuwepo. Mkataba ulioboreshwa uliidhinishwa na wadau katika kikao kilichofanyika tarehe 23 Juni, 2015 na ilikubalika kwamba Mkataba huo uanze kutumika rasmi tarehe Mosi, Julai, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, masharti yamewekwa kwamba kila Mmiliki wa basi au lori anayeomba leseni ya usafirishaji toka *SUMATRA* ni lazima awasilishe mikataba ya ajira ya Madereva wake ambayo imehakikiwa na Maafisa wa Kazi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kusimamia majadiliano baina ya Vyama vya Wafanyakazi, Madereva na Umoja wa Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji ili kuwawezesha kufikia muafaka wa viwango vya posho za safari na kujikimu wakati Madereva wanaposafiri ndani na nje ya nchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, swali la nyongeza.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili

ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado kuna malalamiko makubwa sana kwa Madereva wa malori na mabasi na karibu asilimia 90 ya Madereva hao hawana mikataba ya kazi na kwa sababu Serikali inasema kwamba Mikataba yao ilitakiwa iboreshwe toka mwaka 2015 na mpaka sasa mikataba yao bado haijaboreshwa na bado hawajapewa mikataba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha jambo hili ili wafanyakazi hao waweze kufanya kazi yao vizuri kwa sababu wakiwa na mawazo sana wanaweza wakasababisha ajali na Watanzania wengi wapakoteza maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na tatizo kubwa sana kwa sisi ambao tunaishi mipakani na mmeona kuna migomo mingi sana inatokea pale Tunduma watu Madereva wanapaki malori kwa sababu tu ya migongano kati ya wamiliki wa mabasi na malori kwa ajili ya mikataba hiyo? Sasa Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba jambo hili linakwisha haraka kwa sababu ni muda mrefu sasa na Serikali ipo, inatoa majibu humu Bungeni lakini utekelezaji unakuwa hakuna? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yake nitayajibu yote kwa mkupuo. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na katika ahadi ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa akiwa Kahama mwaka 2015 juu ya Mikataba ya Wafanyakazi na hasa Madereva, Serikali inakuja na mpango mkakati ufuatao, hatua ya kwanza ilikuwa ni kuwataka Wamiliki wote wa Mabasi na Malori ambao watakwenda kuomba *SUMATRA* leseni ya usafirishaji wahakikishe kwamba

wanawasilisha na Mikataba ya Wafanyakazi kama eneo la kwanza la kuhakikisha kwamba Madereva hawa wanapata mikataba yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza hili, Serikali tumekuja na mkakati tofauti tumeona kwamba mkakati huu ulikuwa una mianya ya utekelezaji wake hivyo, siku mbili hizi zijazo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, watatoa tamko na maelekezo ya kuanzia tarehe moja mwezi Julai ni hatua gani zitachukuliwa. Kuanzia hapo nina hakika kwa mkakati huo ambao wameuweka ni kwamba kila Dereva wa nchi hii atakuwa na mkataba wake na tutahakikisha kwamba pia kila Mmiliki wa Chombo cha Usafiri anafuata masharti ya sheria kama Kifungu cha 14 cha Sheria za Ajira na Uhusiano Kazini kinavyosema. Kwa hiyo, nimwondoe tu hofu Mbunge kwamba si maneno tu lakini mkakati umeshawekwa vizuri kabisa na tumekaa na wenzetu wa Jeshi la Polisi muda siyo mrefu kuanzia tarehe Mosi, Julai mtaona cheche za Wizara.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge leo tuna maswali mengi sana, kwa hivyo tutaendelea na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

Na. 460

Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Simbo, Ziba, Choma cha Nkola na Igurubi kwa Ufadhili wa Benki ya Dunia

MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. SEIF K. GULAMALI) aliuliza:-

Wilaya ya Igunga ilipata ufadhili wa Benki ya Dunia wa ujenzi wa Vituo vya Afya vya Simbo, Ziba, Chomachankola na Igurubi ambapo Vituo vya Afya vya Ziba, Chomachankola na Igurubi vimekamilika na vifaa tayari vipo japo majengo na vifaa katika Kituo cha Afya cha Chomachankola na

Igurubi bado havijaanza kufanya kazi; Kituo cha Afya cha Simbo bado hakijakamilika na vifaa havipo na Wafadhii walishakabidhi Halmashauri bila kukamilisha ujenzi huo:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kujua nini kilicho jificha juu ya Mradi huo kukabidhiwa bila kukamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Wilaya ya Igunga ilipata ufadhili wa Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya Simbo, Ziba, Chomachankola na Igurubi. Sababu kuu ya kushindwa kukamilika kwa miradi hiyo kwa wakati ilitokana na makadirio ya chini ikilinganishwa na gharama halisi za kukamilisha ujenzi. Ili kukamilisha ujenzi wa Vituo hivyo kwa kuzingatia ramani mpya, Serikali ilitoa jumla ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya Simbo na Igurubi ambapo kila kituo kilipatiwa shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Simbo kimekamilisha ujenzi wa majengo ya upasuaji na nyumba ya mtumishi na sasa vifaa tiba vinaendelea kuletwa. Aidha, Kituo cha Afya Igurubi kinaendelea na ujenzi wa majengo manne ambayo ni Maabara, Jengo la Wazazi, Jengo la Kufulia na Jengo la Kuhifadhia maiti. Majengo yote haya yapo katika hatua za ukamilishaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mchemba, swali la nyongeza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami naomba niulize swali dogo la nyongeza, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo inafanya kukamilisha Vituo vya Afya ambavyo mimi mwenyewe kama Mjumbe wa Kamati hiyo nimejionea kwa macho yangu mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu sasa, kwa kuwa Kituo cha Afya Simbo kimekamilika na bado hakijaanza kazi, je, ni lini sasa hivyo vifaa tiba vitapelekwa haraka sana ili kuwapunguzia adha wagonjwa ambao wanakimbilia kwenda Hospitali ya *Private* ya Nkinga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchemba, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nipokee pongezi kwa niaba ya Wizara na yeye mwenyewe amekuwa shuhuda amejionea kwa macho yake, lakini katika swali lake anauliza lini Kituo cha Afya hicho ambacho kimeshakamilika kitaanza kutoa huduma kama ambavyo Serikali imekusudia. Naomba nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge tayari fedha tumeshalipa *MSD* na vifaa vinanunuliwa moja kwa moja kutoka mtengenezaji, kwa hiyo wakati wowote vifaa vikishakamilika, lakini pia kumekuwa na changamoto ya Wataalam wa kutoa tiba kwa ajili ya usingizi *anesthesia*, tayari wamepelekwa Bugando mmoja na mwingine amepolekwa Muhimbili ili vifaa vitakapofika na wataalam waweze kutoa huduma ili wananchi wasihangaikie kutembea umbali mrefu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 461

Upungufu wa Watumishi - Halmashauri ya Mji Kibaha

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Mji wa Kibaha unakua kwa kasi hivyo mahitaji ya Watumishi yameongezeka ikiwemo Watendaji wa Mitaa, Maofisa Mifugo, Walimu pamoja na Watumishi:-

Je, ni lini Serikali itatoa kibali cha ajira na kuajiri Watumishi pungufu ili kuleta ufanisi zaidi katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ikama ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 Halmashauri ya Mji wa Kibaha ilikuwa na uhitaji wa Watumishi 1,854 ambapo waliopo ni 1,713 na upungufu ni watumishi 140 sawa na asilimia 7.7. Hivyo, Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni miongoni mwa Halmashauri zenye tatizo dogo la upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri Watumishi wa Kada mbalimbali na kuwapanga kwenye halmashauri kwa kuzingatia mahitaji ya halmashauri kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, swali la nyongeza.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuipongeza Serikali yetu kwanza katika suala la afya ambapo tayari ilitupatia milioni 500 kwa upanuzi wa Kituo chetu cha Afya Mkoani na imetekelezwa, lakini vilevile bilioni moja na laki tano kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya mradi ambao unaendelea, sambamba na hilo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ikama ya Watumishi wa Afya ni 360 na tulio nao ni 255 tunao upungufu wa Watumishi 105 katika Idara yetu ya Afya jambo ambalo linasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wanapokwenda kupata huduma na tukizingatia kwamba sasa Hospitali ya Wilaya inakwenda kukamilika mapema; je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ajira kwa upungufu huu ili kusudio la kutoa huduma hii liweze kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa vilevile ikama ya Watendaji wa Mitaa ni 73 na tunao 50 na tuna upungufu wa Watendaji 23 na tunapata malalamiko sana hasa tunapofanya ziara katika mitaa yetu kwa wananchi wetu na ikizingatia kwamba tunakwenda sasa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; je, ni lini sasa Serikali itajazia upungufu wa watumishi hawa ili huduma hii iweze kuwafikia wananchi na tusiwe na malalamiko?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunamshukuru sana kwa pongezi zake kwa kazi nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano. Swali lake la kwanza ametaka kujua ni lini tutapata Watumishi kwenye Sekta ya Afya.

Tulizungumza mara kadhaa, turudie tu kwamba tumeshaangalia changamoto hii katika maeneo mbalimbali pamoja na Kibaha, lakini tumeshaomba Kibali Utumishi kupata Watumishi wa Sekta ya Afya 12,000. Kwa wakati huo tukipata kibali hiki na kuajiri tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba watumishi hawa watapelekwa katika eneo hilo wakatoe huduma kwa watu wetu ili waendeleo kufurahia maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anasema kuna upungufu katika Watendaji wa Mitaa na Vijiji na kwa sababu kuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo katika mitaa yetu na vijiji hatuna watendaji, lakini jambo hili la uchaguzi naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi na Watanzania wengine wote, hao hao wanaosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kupata Watendaji wa kila siku kutoa huduma kwa watu wetu, lakini wakati wa uchaguzi kama itatokea kuna kijiji au mtaa ambao hauna Mtendaji wa Kijiji, basi wale Watumishi wa Umma waliopo pale watafanya kazi hiyo kwa niaba ya Serikali na tunahakikisha kwamba jambo hilo litaenda vizuri bila tatizo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 462

Utekelezaji wa Mpango wa Matengenezo ya Barabara ya Mkanana hadi Chibwegele

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Serikali ilikuwa na Mpango wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya kutoka Mima kwenda Mkanana hadi Chibwegele, Mpango huo haujatekelezwa mpaka sasa.

Je, ni lini Serikali itatekeleza Mpango huo ili barabara hiyo iweze kupitika wakati wote bila matatizo kuliko ilivyo sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mima hadi Mkanana yenye urefu wa kilomita 23 inaunganisha Kijiji cha Mkanana kilichopo Uwanda wa Mlimani na barabara ya Wilaya itwayo Gulwe, Chitope inayoambaa uwanda wa chini wa safu za mlima. Barabara hii inahitaji matengenezo makubwa ya kuwekewa tabaka la zege katika sehemu yenye miamba na mlima kwa urefu wa kilomita tano, changarawe kwenye maeneo ya tambarare na ujenzi wa vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 99 kwa ajili ya kufanya matengenezo makubwa ya barabara ya Gulwe - Chitope yenye urefu wa kilomita 58.8 ambayo inaunganisha barabara ya Mima - Mkanana hadi Chibwegele, Makao Makuu ya Wilaya na Barabara kuu ya Iringa - Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa barabara ya Mima - Mkanana inafanyiwa matengenezo kwenye maeneo korofi kwa urefu wa kilomita tano kwa gharama ya shilingi milioni 42. *TARURA* imefanya tathmini ya kuikarabati barabara hiyo na kubaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 1.6 zinahitajika ili iweze kupitika katika nyakati zote. Hivyo, Serikali inaendelea kutafuta kiasi hicho cha fedha ili kuiwezesha *TARURA* kukamilisha kazi hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Malima Lubeleje, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, barabara hii ninayoizungumzia kutoka Mima – Nkanana – Chibwegele eneo korofi siyo kilomita 5 ni zaidi ya hapo. Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha kwa sababu shilingi milioni 42 hazitoshi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutambua kwamba barabara ya kutoka Gulwe – Berege - Mima - Chitope inahitaji shilingi bilioni 1.6 ili ipate matengenezo makubwa. Sasa ni lini fedha hizi zitatafutwa ili barabara hiyo iweze kufanyiwa ukarabati? Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameshapita barabara hiyo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze Naibu Mawaziri wawili kwa majibu mazuri kwa maswali ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lubeleje ambaye mimi namwita greda la zamani makali yaleyale siku zote ni Mbunge ambaye anafuatilia jimbo lake, ni kweli tulipokwenda ziarani jimboni kwake tumebaini changamoto kubwa, si barabara hiyo tu hata kwenda Nambi, Tubugwe na maeneo mbalimbali kuna changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu na Mheshimiwa Lubeleje anafahamu kwamba kwa kuwepo na kipaumbele kwanza,

sababu changamoto yake kubwa hata pale mjini tumeamua mwaka huu tutaenda kuwawekea barabara za lami lakini ile barabara ambayo ina changamoto kubwa, siku ile tulipita katika mazingira magumu sana, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba awe na amani kwamba tutafanya kila liwezekanalo barabara hii ambayo kwa kweli haipitiki na shilingi milioni 42 ili kuifanya marekebisho makubwa. Hata hivyo, nimhakikishie kwamba ni *commitment* ya Serikali na hasa katika Jimbo la Mpwapwa na Wilaya nzima ya Mpwapwa tutafanya kila liwezekanalo ili wananchi wa Mpwapwa wafaidi matunda mazuri ya Mbunge wao ambaye ni *senior MP* katika Bunge hili.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, sasa aulize swali lake.

Na. 463

Faida ya Miti ya Mikoko

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN aliuliza:-

Je, Serikali inafaidikaje na rasilimali ya miti ya mikoko iliyoanzia katika Ukanda wa Pwani ya Tanga mpaka Mtwara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa misitu ya mikoko ni pamoja na kuwa mazalia na makazi ya viumbe

wa baharini; nan i moja ya vivutio vya utalii nchini; na ni mfumo ikolojia unaosaidia kuondoa kiwango kikubwa cha hewa ukaa (*carbon sequestration*) ambayo ingeweza kuongeza kiwango cha joto la dunia na kusababisha mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, misitu hii huhifadhi fukwe na mazingira ya bahari kwa kuzuia uharibifu utokanao na mmomonyoko wa fukwe na kingo za bahari, hivyo kuokoa mali na maisha ya makazi ya wakazi wa Pwani kutokana na vimbunga, dhoruba na mawimbi ya bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile misitu hii husaidia kuchuja udongo, uchafu na sumu zinazoweza kutiririshwa na maji yanayoingia baharini ambayo huchangia kuharibu matumbawe ambapo ni makazi ya mazalia ya samaki wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, miti ya mikoko ina umuhimu kwa Taifa kama sehemu muhimu ya hifadhi ya ikolojia, huipatia jamii chakula na kipato kupitia shughuli za ujenzi, ufugaji nyuki na kuongeza pato la kaya pia ni chanzo cha mapato kwa Serikali kupitia vibali vya kuvuna miti ya mikoko na biashara ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa misitu ya mikoko nchini, misitu hii imekuwa ikihifadhiwa tangu kabla ya uhuru kwa kuchukua hatua ikiwemo kutunga sheria ijulikanayo kama *The Tanganyika Forest Laws and Rules Handbook* ya mwaka 1947. Baada ya uhuru Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha mikoko inalindwa. Mwaka 1987 Serikali ilipiga marufuku ukataji wa miti ya mikoko hadi mwaka 1991 ulipoandaliwa mpango wa usimamizi wa mikoko. Chini ya mpango huu, misitu ya mikoko imeendelea kuhifadhiwa na ukataji wake hufanyika kwa kibali maalum kutoka Wakala wa Misitu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhifadhi misitu hii, Tanzania inachangia katika malengo ya kidunia ya kupunguza hewa ukaa na kupunguza athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa kuzingatia umuhimu wa rasilimali hii, nawasihi wadau wote wakiwemo wananchi wa maeneo ya Pwani na Serikali zote za Mitaa kushirikiana katika kuitunza na kuihifadhi kwa manufaa ya Taifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya kitaalamu ambayo ameyatoa na mimi kwa uhaba wangu wa elimu naweza nikayagawanya au nikayafanyia *summary* majibu yake katika mambo matatu kwamba mikoko ina faida ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Ameshaeleza umuhimu wake, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, pamoja na hizo faida za kiuchumi na kijamii zilizopo, je, jamii inayozungukwa na miti hiyo inapewa elimu ya kutosha juu ya umuhimu, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ametaja faida za kimazingira kwamba kuhifadhi udongo, upepo, bionuai na kuhifadhi sumu. Je, ni kipi kipaumbele cha Serikali katika uhifadhi huo wa kimazingira ambacho wamekifanyia kazi hadi sasa? Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee shukrani zake lakini pia nimpongeze amekuwa mdau mzuri sana wa mazingira tangu tumeanza na tunashirikiana pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kuhusu kutoa elimu, ni kweli na sisi tunaendelea kutoa elimu na hili ni jukumu letu kama Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na ili tuweze kufanikiwa jambo lolote katika utekelezaji wake elimu tumeipa kipaumbele. Hata hivyo, kipaumbele kikubwa ni

mazingira na kwenye majibu yangu ya msingi nimeeleza namna ambavyo mikoko inavyotusaidia katika kuhifadhi kingo za maeneo ya Pwani hasa tunapokuwa na miradi ya mabadiliko ya tabia nchi katika kujenga zile kuta kwenye kingo tunatumia fursa hiyo hiyo katika mradi huo huo kuhakikisha tunapanda miti ya mikoko kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kutunza mazingira. Kwa hiyo, kipaumbele chetu ni kuhifadhi mazingira. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, sasa aulize swali lake.

Na. 464

Ujenzi wa Chuo cha VETA Kwimba

MHE. RICHARD M. NDASSA aliuliza:-

Wananchi wa Halmashauri ya Kwimba waliombwa kutafuta eneo la kujenga Chuo cha *VETA* ambapo eneo la ekari 60 lilishapatikana zaidi ya miaka 10 iliyopita na Serikali imekuwa ikiahidi kutenga fedha za ujenzi wa chuo hicho:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa chuo hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa nchi kuwekeza katika elimu ya ufundi na mafunzo ya

ufundi stadi, hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ipo katika jitihada za kuelekea uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi ikiwa na lengo la kutimiza azma ya kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi katika kila mkoa na wilaya. Ujenzi wa vyuo hivi unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kwimba ni moja ya Kata ya Wilaya zilizopo katika awamu ya pili inayotarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa sasa wananchi wa Kwimba wanashauriwa kutumia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya kilichopo Wilaya ya Kwimba na vingine vilivyo mkoa na wilaya za jirani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, swali la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kwanza niipongeze Serikali kwa kukubali na kupokea ombi la Wilaya ya Kwimba yenye majimbo mawili kwamba itaanza ujenzi huo kwenye mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa sababu Madiwani wa Wilaya ya Kwimba ambao sasa wamesharidhia kama walivyoombwa na *VETA* wenyewe kwamba ile hati ambayo ilikuwa imeandikwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ihame sasa iende *VETA* kazi ambayo imeshafanywa na tumeshapeleka hati hiyo kwenda kubadilishwa, nini hatua inayofuata sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, si vibaya kujua maoteo ya gharama ya ujenzi wa chuo hicho. Je, gharama hiyo ni shilingi ngapi hadi kikamilike?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunapokea pongezi zake lakini naomba nimhakikishie kwamba pindi wao watakapokuwa wamekamilisha taratibu za kupata ardhi na hati wawasilishe Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili mchakato wa ujenzi uweze kuanza mara moja. Nina hakika utaratibu ukikamilika mradi utasimamiwa vizuri kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amebahatika vilevile kuwa na DC mahiri na mzuri sana Mheshimiwa Senyi. Kwa hiyo, nategemea kwamba fedha zile zikipatikana mradi ule utaenda vizuri.

Kuhusu maoteo ya gharama za mradi ule kwa sasa Wizara imefikiria kwamba tutahitaji angalau shilingi bilioni 1.5 kama matumizi ya awali. Hata hivyo, Wizara iko tayari kuweka fedha kwenye mradi kadri mahitaji yatakavyotokea.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini.

Na. 465

Hitaji la Shule za Ufundi katika kila Halmashauri

MHE. EDWARD F. MWALONGO aliuliza:-

Elimu ya ufundi ni muhimu sana kwa vijana:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kubadili shule moja ya sekondari katika kila Halmashauri na kufanya kuwa shule ya ufundi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha kozi za ualimu wa ufundi iliyokuwa ikitolewa na *Dar es Saalam Institute of Technology*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule za ufundi, hususan wakati huu ambapo inatekeleza dhamira yake ya kujenga uchumi wa viwanda. Ili kufikia lengo hilo, Serikali tayari imekarabati shule za sekondari za ufundi kongwe saba (7) ambazo ni Musoma, Bwiru Wavulana, Ifunda, Tanga, Moshi, Iyunga na Mtwara. Hivyo, kwa sasa Serikali imejielekeza katika kuimarisha shule za ufundi zilizopo ili ziendelee kutoa elimu ya ufundi iliyo bora.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilikuwa ikitoa mafunzo ya walimu ufundi, kozi hiyo iliitwa *Diploma in Technical Education*. Baada ya Serikali kuanzisha Wizara mpya iliyokuwa inaitwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, *DIT* kikiwa chuo kimojapo cha teknolojia kiliamishiwa chini ya Wizara hiyo. Serikali ilifanya maamuzi kuwa kozi ya *DTE* iendelee kuwepo lakini iendeshwe katika mojawapo ya vyuo vilivyopo chini ya iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni na siyo *DIT*. Mwaka 1991 kozi ya *DTE* iliamishwa toka *DIT* kwenda Chuo cha Ualimu Kleruu kilichokuwa chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa masomo ya ufundi, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ina mpango wa kuanza tena mafunzo ya ualimu wa masomo ya ufundi. Vilevile Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kimeanza maandalizi ya utoaji wa mafunzo hayo ambapo kwa sasa mitaala ya masomo hayo inafanyiwa kazi na Tume ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kufanya maboresho makubwa katika Chuo cha Ualimu Kleruu pamoja na Chuo cha Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Morogoro (MVTCC) kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ikiwepo ujenzi wa mabweni ya wanafunzi kwa lengo la kuongeza nafasi za udahili kwa walimu wa masomo ya ufundi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD F. MWALONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote niipongeze sana Serikali kwa jitihada ambazo zinaendelea, niombe basi *speed* iongezeke kuwaandaa walimu, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ufundi ni ujuzi wa jambo lolote lile. Je, Serikali inaonaje sasa ikabadilisha mtizamo wa kuanza kujenga vyuo vya ufundi vikubwa na vyenye gharama kubwa badala yake iende kwenye fani ambazo zinahitaji fedha kidogo na kazi za mikono kwa vijana wa Tanzania kama vile kilimo na ufugaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Njombe tuliahidiwa kukarabatiwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Chuo kile ni kichakavu sana kinachukua wananfunzi wachache sana. Je, Serikali imefikia wapi katika ahadi yake ya kukarabati Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Njombe Mjini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kujielekeza zaidi kwenye vyuo vidogo badala ya vile ambavyo vina

gharama kubwa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendesha vyuo vya aina zote; vidogo, vya kati vilevile vikubwa. Yeye mwenyewe ni shahidi kwamba Serikali kwa sasa imeweka fedha nyingi katika kukarabati Vyuo vya Wananchi lengo lake ni ili wananchi waweze kupata kozi ambazo zinaendana na shughuli ambazo wanafanya. Kwa hiyo, kwenye maeneo ya kilimo kunakuwa na vyuo ambavyo viatoa elimu ya ufundi wa masuala ya kilimo au shughuli nyingine yoyote ambayo wananchi wanafanya. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba wazo lake hilo siyo baya na tayari Serikali inalifanyia kazi na ndiyo maana kuna vyuo vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la Chuo chake cha Wananchi kwamba ni lini kitaanza kukarabatiwa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa tumeanza na ukarabati wa vyuo 20 kati ya vile vyuo 55 na tunategemea vile vingine vilivyobaki ukarabati utaanza mwezi ujao. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba yeye na wananchi wake wawe tayari kwa sababu ukarabati unakwenda kuanza.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 466

Utekelezaji wa Miradi ya REA- Bagamoyo

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA aliuliza:-

Kasi ya utekelezaji wa miradi ya REA III Jimboni Bagamoro ni ndogo:-

Je, ni lini miradi hiyo itakamilishwa katika Jimbo la Bagamoyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea na utekelezaji wa usambazaji wa umeme katika Mkoa wa Pwani ambapo Bagamoyo ni miongoni mwa wilaya zinazonufaika na mradi unaoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya vijiji 10 vya Jimbo la Bagamoyo vimejumuishwa katika utekelezaji wa mradi wa *REA III*, mzunguko wa kwanza unaoendelea. Hadi kufikia tarehe 25 Juni, 2019, vijiji vyote 10 ambavyo ni Kongo, Kimarang'ombe, Kitopeni, Kiharaka (Kiembeni na Minazi Minane), Matimbwa (Ugongomoni na Kibahengwa), Udindivu KKKT, Fukayosi, Kimele A&B, Mto wa Nyanza na Migude vimepatiwa umeme na wateja wa awali 927 wameunganishiwa umeme. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kuunganisha wateja katika vijiji vyote vilivyotajwa kadri wanavyolipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo imejumuishwa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 9.84; njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 37.14; ufungaji wa transfoma 21 za KVA 50 na 100 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 1,154. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 2.05. Kazi ya kusambaza umeme katika mradi huu utakamilika ifikapo mwezi Juni 2020.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa. swali la nyongeza

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pia nichukue fursa hii kuwapa hongera sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi kubwa wanayoweka katika utekelezaji wa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Kijiji cha Kondo katika Kata ya Zinga ambacho kilikuwa kwenye mradi wa *REA II*, mpaka kufikia Juni 2016 kijiji hicho hakikutekelzewa mradi wake na Mheshimiwa Waziri akaahidi vijiji vyote ambavyo havikutekelzewa miradi yao katika *REA II* basi vitapewa kipaumbele katika *REA III*. Huu ni mwaka 2019 kijiji hicho ambacho kiko katika Kata ya Zinga na humo ndani kuna Shule ya Msingi ya Kondo na jirani kuna Shule ya Sekondari ya Zinga, sehemu zote hizo hazina umeme mpaka hivi sasa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana kauli gani kuhusu kukipatia umeme Kijiji hiki cha Kondo na miundombinu ya Shule ya Sekondari Zinga na Shule ya Msingi Kondo mapema iwezekanavyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kwenye swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Kawambwa kwa kazi nzuri anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijajibu swali, Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake vijiji vyote sasa vimeshapata umeme kwa sababu ya kazi anayofanya anavyofuatilia, kilichobaki ni vitongoji. Kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kati ya wilaya ambazo sasa hivi vijiji vyake ambavyo vimeshapata umeme ni pamoja na Jimbo la Bagamoyo, kwa hiyo Mheshimiwa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, alishughulika sana na Shule ya Sekondari ya Fukayosi mwaka jana, ilikuwa na changamoto ya umeme na imejengwa na Korea Kusini,

tunampongeza sana ina umeme sasa hivi na inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitongoji 169 katika Jimbo la Mheshimwa Mbunge; vitongoji 161, vitongoji 100 vyote vina umeme bado vitongoji 69 na Kati ya vitongoji 69 ambavyo havina umeme ni pamoja na Kitongoji cha Kondo. Kwenye Kijiji cha Kondo kuna vitongoji vitatu; vitongoji viwili tayari vina umeme isipokuwa Kondo Kati anayozungumza Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo nimpe tu imani Mheshimiwa Mbunge kwamba nimeshawaelekeza wakandarasi kwa kushirikiana na *TANESCO* wameshaanza kupeleka umeme kwenye Kitongoji cha Kondo na watakamilisha tarehe 12 mwezi ujao. Wanapeleka kwenye Kitongoji cha Kondo pamoja na Shule ya Msingi ya Kondo, lakini pamoja na Shule ya Sekondari ya Zinga. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wala asiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongeze kidogo kwa Jimbo la Bagamoyo na Chalinze, mkandarasi aliyeko kule anapeleka umeme kwenye vitongoji vyote na *Peri urban* inaanza tarehe Mosi mwezi ujao kujumuisha vitongoji vyote vya Bagamoyo pamoja na Chalinze. Chalinze kuna kijiji kirefu sana cha Msigi pamoja na Magurumatara cha kilomita 28 na chenyewe kinapelekewa umeme. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri ni kama yalitakiwa yawepo maswali mengi ya nishati leo ili kila Mbunge asikie kwenye Jimbo lake hiyo ratiba ilivyopendeza vizuri. Ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti sasa alulize swali lake.

Na. 467

Barabara inayounganisha Mkoa wa Arusha na Mara

MHE. MARWA R. CHACHA aliuliza:-

Barabara inayojengwa kuunganisha Mkoa wa Mara na Arusha inasuasua sana, kwani tangu ilipoanza kujengwa 2013 mpaka leo hata kilomita 50 zimeshindwa kukamilika.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani dhidi ya ukamilishaji wa barabara hii?

(b) Je, ni lini wananchi waliofanyiwa tathmini watalipwa fidia zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayounganisha Mikoa ya Mara na Arusha yenye urefu wa kilomita 452 kutoka Makutano Juu (Musoma) – Natta – Mugumu – Loliondo hadi Mto wa Mbu ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kukamilika mwaka 2013. Aidha, baada ya kukamilika kwa usanifu ujenzi wa barabara hiyo umeanza kwa awamu ambapo kilomita 50 kutoka Makutano Juu hadi Sanzate na kilomita 49 kutoka Wasso hadi Sale *Junction* unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mkandarasi amechelewa kukamilisha kazi kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia *TANROADS* imeshachukua

hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mkandarasi anamaliza kazi iliyobaki kwenye barabara ya Makutano – Sanzate inayotarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwaka huu. Sehemu ya pili ya Sanzete – Natta yenye urefu wa kilomita 40 ipo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi. Aidha, kwa upande wa Mkoa wa Arusha, kilomita 49 kutoka Wasso hadi Sale ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wote waliofanyiwa uthamini wanaendelea kulipwa fidia zao kabla ya kazi ya ujenzi kuanza. Aidha, mpaka sasa waathirika nane (8) wamefidiwa kiasi cha shilingi 12.871 kwa Mradi wa Wasso – Sale kilomita 49. Katika Mradi wa Makutano – Sanzate kilometa 50 wananchi waliolipwa fidia ni watu 433 kwa jumla ya shilingi milioni 2.608. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, swali la nyongeza.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kiukweli majibu haya hayaridhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulienda Serengeti na Naibu Waziri pamoja na Kamati ya Miundombinu, Naibu Waziri gari lake lilipata pancha mara nne, matairi manne. Tukampa *spare* zikaisha mpaka raia wananchi wakampa *spare*, hali ni mbaya kwa wananchi wa Serengeti. Ukiangalia barabara imeanza kujengwa tangu 2013, miaka sita (6) imepita kilomita 50 hazijakwisha; Je, itachukua miaka mingapi kumaliza kilomita 80 kutoka Sanzate mpaka Mugumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wananchi wa Mugumu kwenye hiyo kandokando ya barabara walishafanyiwa tathmini na kila mtu anajua analipwa shilingi ngapi, ni lini watalipwa fidia zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ryoba Chacha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pamoja na masikitiko yake lakini niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Ryoba kwa namna anavyofuatilia hasa miradi hii ya barabara. Ni kweli niseme tu kwamba barabara hii kwa historia ni barabara muhimu, hizi kilomita 452 mimi nimeipita hii barabara ina changamoto zake. Kwa historia Marehemu Baba wa Taifa alikuwa akipita barabara hii akitokea Arusha miaka ile, kwa hiyo ni muhimu na sisi kama Serikali tunaiangalia kwa macho mawili. Niseme tu pamoja na kuwa ujenzi huu umekwenda kwa hatua hiyo ya kusuasua lakini kama nilivyosema na kwa kweli kwa ushirikiano wa Wabunge wa Mkoa wa Mara nimejibu wiki juzi swali la Mheshimiwa Agness Marwa na wiki iliyopita nimejibu swali la Mheshimiwa Getere kuonesha umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Ryoba avute subira, lakini niseme tu kwamba kama *commitment* nilivyosema hapa na namna tunavyosimamia vizuri sasa pamoja na kuchelewa lakini barabara hii itakamilika na kama nilivyokuwa nikizungumza hapa, kwa hiyo tunaisimamia vizuri itakamilika vuta subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kilomita 452 tuko asilimia 41 ya *commitment* ya barabara, kwa Mradi huo wa Makutano Juu – Sanzate kilomita 50. Kama nilivyosema kutoka Sanzate – Natta kilomita 40 tuko hatua ya manunuzi, lakini pia kwenye bajeti Natta – Mugumu kilomita 45 tumeitengea bajeti na ujenzi wa eneo la Wasso – Sale kilomita 49. Utaona asilimia 41 tunaendelea kuisogelea kuweza kuikamilisha barabara hii, kwa hiyo avute tu subira Mheshimiwa Ryoba tutaisimamia vizuri barabara hii ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya swali lake kuhusu tathmini ya wale wananchi; kama nilivyosema, kiutaratibu tunatakiwa tulipe kabla ya ujenzi kuanza. Kwa hiyo

tutazingatia sheria, kanuni na taratibu zilizokuwepo, Sheria ya Ardhi, Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, wananchi watalipwa haki yao kulingana na sheria, kwa hiyo avute tu subira kabla ya kuanza ujenzi wananchi hao watalipwa mara moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niulize swali la nyongeza, naamini kwamba kwa watu wale ambao wanategemea usafiri wao wa maji kivuko ni barabara. Sasa kwa kuwa kivuko ni barabara nataka kuzungumzia kivuko cha Lindi ambacho kinatoka Msinjaili kuelekea Kitumbikwera. Kivuko hiki ni muhimu sana kwa usafiri wa watu wa eneo lile. Sasa kivuko kile kimeshawahi kuharibika na kikapotea kikaelekea maeneo ya mbali. Kutokana na kupotea huko tunamshukuru Mungu hakikuweza kusababisha ajali ya kuua watu. Kwa kuwa kivuko hiki kinaharibika mara kwa mara; Je, Serikali ina mpango gani wa kututengenezea kwa uhakika ili kivuko hiki kiendeleo kutumika katika eneo husika? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama yangu amekuwa akifuatilia sana mambo mbalimbali hasa kwenye Mkoa wa Lindi, kwa hiyo nitumie nafasi hii kumpongeze. Niseme tu kwa ufupi kabisa tunafahamu umuhimu wa kivuko hiki na tunafahamu namna kivuko hiki kinavyowahudumia wananchi wa Lindi. Tumefanya kwa kweli maboresho makubwa sana katika eneo hili, tumetengeza eneo la maegesho ya kivuko, tumetengeneza nyumba kwa ajili ya abiria wanaovuka kwenda ng'ambo kule. Niseme tu kwa tatizo la kivuko hiki kweli kimekuwa na matatizo kidogo na tumefanya ukarabati mkubwa lakini nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba

tumejipanga kwa sababu Bunge hili limetupitishia fedha za kutosha kwa ajili ya kuongeza vivuko katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapatazama pale, itakapokuwa imewezekana tutabadilisha injini ya kivuko hiki, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge avute subira, tumejipanga ili tuone kwamba changamoto ambazo zilikuwa zinajitokeza na zinaendelea kujitokeza tutaendelea kuzitatua na kuziondoa kabisa. Kwa hiyo wananchi wa Lindi wawe na subira lakini niwape *comfort* tu kwamba, tumejipanga vizuri tutafanya maboresho makubwa pamoja na ile barabara ya kule ng'ambo tutaifanyia matengenezo ili wananchi baada ya kuvuka waweze kwenda na shughuli zao bila kikwazo chochote. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi sasa, aulize swali lake.

Na. 468

Barabara ya Bunda Mpaka Musoma Vijijini

MHE. JOYCE B. SOKOMBI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara itokayo Bunda kwenda Musoma Vijijini ili kuwapunguzia wananchi wa Saragana, Bugoji, Mabui Merafuru, Melaturu, Kangetutya na Kanderema aidha ya kuzunguka kupitia Musoma Mjini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo; ingawaje marekebisho aliyoyafanya sikuyapata sawasawa kwa hiyo kama nitakosea haya majina magumu naomba aniwie radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara kuu kutoka Bunda hadi Manyamanyama chenye urefu wa kilomita 5.79 kinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mara. Aidha, ukarabati wa kipande hiki ulikamilika mwaka 2016 na kwa sasa kipo katika hali nzuri hivyo kupitika kwa urahisi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mkoa kutoka Manyamanya kupitia Vijiji vya Bugoji – Saragana hadi Nyambui kilomita 37.45 inahudumiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Mara na kwa sasa barabara hii inapitika vizuri. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 351.976 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 130.855 kwa ajili ya kuendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili ipitike majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayoanzia Saragana hadi Kanderema kupitia Vijiji vya Mabui Merafuru na Kangetutya ni barabara ya wilaya ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA). Hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na TAMISEMI kuhusu mipango waliyonayo kwa sehemu hiyo ya barabara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, swali la nyongeza.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, majibu hayajaniridhisha kwa sababu mimi mwenyewe natokea hukohuko Musoma Vijijini. Barabara hii ni kiunganishi kikubwa sana kwa wakazi wa maeneo hayo na barabara hii haipitiki kama anavyoelezea. Watambue kwamba kuna wakulima na wafanyakazi na wafanyabiashara pamoja na wafugaji. Barabara hii ni mateso sana kwa wakulima kutoa mazao yao kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Serikali haioni sasa ni wakati wa kuijenga barabara hii ili kuinua uchumi wa maeneo hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana ya Serikali, naomba *commitment* ya Serikali; Je, ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza, kwani wananchi wa maeneo hayo wanateseka sana? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kutekelezwa na barabara hii imeendelea kujengwa kulingana na upatikanaji wa fedha na ni ahadi kwamba hawa wananchi tutahakikisha kwamba wanapita katika hiyo barabara. Barabara hiyo kwa sababu imegawanyika; upande wanasimamia *TANROADS*, upande wanasimamia *TARURA* na ndiyo maana sasa hivi iko Kamati Maalum ambayo inapitia barabara zote ili kuweza pia kuweka mgawanyo mzuri wa Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, akawaambie hao wananchi kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi itatekelezwa, hiyo barabara itatengenezwa na wasiwe na wasiwasi wowote kwa sababu tunaendelea kufanya hivyo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.

Na. 469

Umuhimu wa Kufanya Utafiti Ziwa Rukwa

MHE. VICTOR K. MWAMBALASA aliuliza:-

Miaka ya karibuni samaki aina ya Ngege (Pelege) katika Ziwa Rukwa wamepungua na kudumaa na hii ni

kutokana na uchimbaji wa dhahabu Wilayani Chunya na Songwe ambao mara nyingi ulihusisha zebaki.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti katika Ziwa hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma samaki aina ya ngege katika Ziwa Rukwa walikuwa wanakuwa wakubwa kutokana na kuwa walikuwa hawakabiliwi na changamoto zinazowakabili sasa.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFIRI*) katika mwaka huu wa 2019 kwenye Ziwa Rukwa, ilibainika kuwa kuna udumavu na upungufu wa samaki katika ziwa hilo na hasa kwa samaki wa jamii ya ngege. ngege aina ya *Oreochromis rukwaensis* ambaye ni wa asili katika ziwa hilo wamepungua zaidi kulinganisha na ngege aina ya *Oreochromis esculentus* ambao wamepandikizwa. Udumavu na upungufu wa samaki katika ziwa hilo unasababishwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, uchafuzi wa mazingira utokanao na kuongezeka kwa shughuli za binadamu kama vile:-

(i) Kuongezeka kwa idadi ya mifugo inayotegemea ziwa kupata maji ya kunywa na pia malisho ya mifugo hiyo pembezoni mwa ziwa;

(ii) Kilimo kisichofuata taratibu karibu ama pembezoni mwa ziwa;

(iii) Uchimbaji wa madini ya dhahabu ambapo zebaki, (*mercury*) hutumika kuchakata dhahabu hizo; na

(iv) Ongezeko la matumizi ya *petrol* katika machimbo ya dhahabu ambapo *petrol* hiyo yaweza kusababisha madini ya risasi (*lead*) kuingia ziwani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi haramu ambao wavuvi hutumia makokoro na nyavu zisizoruhusiwa; Uvuvi haramu usiozingatia taratibu za kulinda rasimali za za uvuvi na mazingira unaendelea kushamiri katika eneo hilo. Uvuvi huo unahusisha makokoro na nyavu zisizoruhusiwa kama vile matumizi ya vyandarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sampuli za minofu zimechukuliwa katika Ziwa Rukwa zinaendea kuchakatwa ili kujua kiwango cha zebaki na risasi katika minofu ya samaki na pia kuangalia kiasi hicho kama kipo ndani ya viwango vinavyokubalika na Shirika la Afya Duniani (*WHO*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Niseme kwa kweli kabisa kutoka katika upachupachu wa moyo kwamba mimi na mdogo wangu Mheshimiwa Mulugo hapa mbele yangu tumefurahishwa sana na majibu ya Serikali. Serikali imefanya utafiti, utafiti wa kisayansi na utafiti wa mwaka huu, Mheshimiwa Waziri hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa utafiti uliofanywa na Serikali unaonesha kwamba sababu zilizofanya samaki hawa wadumae ziko ndani ya uwezo wa Serikali, kwa mfano, uharibifu wa mazingira na uvuvi haramu, zote ziko ndani ya uwezo wa Serikali. Je, Serikali inafanya nini

kuzuia huu uharibifu wa mazingira ili samaki warudi kama walivyokuwa zamani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kijana mchapakazi sana na anatembea sana hapa Tanzania hajafika tu Chunya na Songwe, je, yuko tayari kufanya ziara Songwe ili mimi na Mheshimiwa Mulugo tuambatane naye kwenda kurekebisha kasoro hizi kwenye Ziwa Rukwa? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya *Senator*, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uniruhusu kupokea shukrani kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge Mulugo na Mwambalaswa kwa Serikali baada ya kutimiza ahadi ambayo imekuwa ikiombwa kila Bunge, kila msimu na Mheshimiwa Mulugo ya kwamba ni lini Serikali itafanya utafiti katika Ziwa Rukwa kujua sababu za udumavu na sasa Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imetekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza anauliza nini sisi Serikali tutafanya ili kuzuia uharibifu huu wa mazingira. Jambo hili ni mtambuka. Kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba sababu zinazosababisha kuharibika kwa mazingira zipo ambazo zinatokana na wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu wanaozunguka eneo lile ambao hawa kimsingi wanatumia teknolojia ya zamani ya kuchakata dhahabu kwa kutumia madini ya *mercury* kwa maana ya zebaki ambapo inatiririka na kuingia katika maji ya ziwa lakini vilevile nimezungumzia idadi ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pamoja sisi katika Serikali, Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Madini na

hata Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), tunao utangamano wa pamoja wa kuhakikisha kwamba hawa wachakataji wadogo wadogo wanaelimishwa na kuelekezwa namna iliyobora ya kuboresha uchimbaji na uchakataji wao. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mwambalasa na jirani yake Mheshimiwa Mulugo kwamba hili tutalifanya kwa pamoja ikiwa ni pamoja na kutengeneza zile tunaita *holding tanks* kwa ajili ya maji yanayotoka katika uchakataji yaweze kuingia kwenye mifumo ile ya kudhibiti maji yale yasiende moja kwa moja katika maziwa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la kama niko tayari kufanya ziara. Nataka nimhakikishie kuwa tukimaliza hili Bunge niko tayari kabisa kwa ajili ya kwenda kufanya ziara kwenye eneo hili na kujionea mimi mwenyewe uharibifu wa mazingira na kuhamasisha Watanzania wanaofanya shughuli zile wafuate sheria na taratibu zetu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, katika huo utangamano mliano ni vizuri Wizara ya Afya iingie kwa sababu madhara kwa samaki kudumaa ni moja, lakini madhara kwa binadamu anayekula samaki wa ziwa hilo ni makubwa zaidi. Kwa hiyo, naamini wakati mkifanya hizo juhudi mtaihusisha Wizara ya Afya kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Phillip Mulugo.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na mimi niipongeze Serikali, miaka yangu tisa ya kukaa hapa Bungeni nimekuwa nikiuliza swali la kufanya utafiti angalau Serikali sasa imeridhia na imefanya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu moja la nyongeza, kwa kuwa Serikali imefanya utafiti na imeona kabisa kwamba kweli samaki wanadumaa kutokana na sababu walizozieleza lakini upo upande mwingine wa kuweza

kupandikiza samaki wa aina nyingine katika Ziwa Rukwa kama ambayo mwaka 1978, Serikali ilichukua samaki kutoka Singida wakatuletea kule Ziwa Rukwa na tulikuwa tunawaita samaki aina ya Singida ambao ndiyo wameisha.

Je, Serikali iko tayari sasa kuangalia samaki wengine upande wa Ziwa Tanganyika, Nyasa au bwawa la Mtera hapa wakachukua wale samaki wakaja kuwapandikiza kwenye Ziwa Rukwa ili kuongeza idadi ya samaki katika ziwa hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Phillipo Mulugo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa rai yako juu ya uwepo wa madini yale na umeelekeza Wizara ya Afya itakapokuja itaendelea kujibu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie watafiti wetu wanatazama maana viko viwango ambavyo vimekuwa *recommended* na *WHO* ikiwa kama vitaonekana vimefikia au vimezidi basi zipo hatua ambazo sisi pamoja na Wizara ya Afya tutazichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jambo la Mheshimiwa Mulugo la namna ya kupandikiza samaki wengine kutoka maeneo mengine, naomba nichukue ushauri huu na tutakwenda kuufanyia kazi, ukionekana ni ushauri wenye kufaa basi tutautekeleza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 470

Hitaji la Nyumba za Madaktari Bingwa Hospitali ya Mkoa wa Iringa

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Iringa inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa nyumba kwa ajili ya madaktari bingwa na hivyo kusababisha madaktari hao kuishi mbali na hospitali:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kutatua changamoto hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa ina madaktari 26 kati ya hao, madaktari wanne ni madaktari bingwa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, hospitali ilitenga kiasi cha Sh.40,000,000 kwa ajili ya kuwapa motisha madaktari wa kulipia gharama za nyumba kila mwezi kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani na fedha kutoka Serikali Kuu kwa maana ya OC. Hadi kufikia mwezi Mei, 2019 kiasi cha Sh.25,500,000 kimekipwa kwa ajili ya malipo ya kodi ya nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya motisha ya watumishi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake lakini pia niendeleo kumshukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Iringa, Dkt. Mwakalebela kwa kazi nzuri sana ambayo amekuwa akiifanya katika hospitali yetu kutokana na changamoto nyingi zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mkoa wetu wa Iringa unakabiliwa na ajali nyingi sana lakini kipindi kirefu hatuna daktari bingwa wa mifupa pia hatujawahi kupatiwa daktari bingwa wa watoto toka hospitali ile imeanzishwa. Tuna wodi kubwa sana katika hospitali yetu ya Mkoa kuliko hospitali zote za Nyanda za Juu Kusini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri sasa anatupa ahadi gani wananchi wa Mkoa wa Iringa kutokana na changamoto hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba niipongeze Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano kwa ujenzi wa Hospitali za Wilaya katika nchi yetu. Mkoa wetu una upungufu mkubwa sana wa watumishi takriban asilimia 70 inawafanya wauguzi na madaktari kufanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Je, nini mpango wa Serikali katika kukabiliana na changamoto hiyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Ritta Kabati amekuwa anafanya kazi nzuri sana ya kufuatilia masuala mbalimbali ya afya katika Mkoa wa Iringa. Kwa kweli amekuwa anafuatilia sana sisi ndani ya Wizara na tunashukuru kuona kwamba ni mdau mkubwa sana katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza linahusiana na kwamba kuna upungufu wa madaktari wa upasuaji wa mifupa pamoja na madaktari wa watoto. Hilo kama Serikali nakiri lakini sasa hivi Serikali inafanya mkakati wa kufanya mafunzo ya madaktari bingwa takribani 100 mwaka jana tumesomesha, mwaka huu tunasomesha madaktari wengine zaidi ya 100. Wwale watakaomaliza mafunzo na tumeweka utaratibu kwamba madaktari bingwa ambao wanasomesha kwa fedha za Serikali baada ya kuhitimu masomo yao, sisi Serikali tutawapangia wapi wanatakiwa kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi madaktari hawa watakapomaliza masomo yao basi Mkoa wa Iringa utakuwa ni moja ya mikoa ambayo tutawapa kipaumbele. Hawa madaktari ambao amewaongelea ni madaktari wa kipaumbele ambao na sisi tumeweka msisitizo kuhakikisha kwamba tunawapa mafunzo na hospitali zote za Rufaa za Mikoa zinakuwa na madaktari bingwa hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameuliza ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaongeza rasilimali watu. Ni kweli hili jambo tunalo na katika mwaka huu ambao unaisha sasa, Serikali imeajiri watumishi zaidi ya 11,000 kuziba mapengo mbalimbali ambayo yamekuwepo na ajira mpya. Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) pamoja na Ofisi ya Rais (Utumishi), tunaendelea kufuatilia vibali kuhakikisha kwamba tunapata wataalam wa afya kwa ajili ya maboresho makubwa ambayo tumeyafanya kwenye vituo vya afya na ujenzi wa hospitali za Wilaya ambazo tunaendelea kujijenga kwa sasa kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hii ya watumishi, kwa kweli watumishi wetu wa afya wanafanya kazi kubwa sana na nzuri katika kuwahudumia Watanzania. Rai yangu katika mikoa yote ikiwa ni pamoja na Mkoa huu wa Iringa ni kuhakikisha kwamba viongozi wa Serikali na viongozi wa vyama wanatengeneza mazingira wezeshi kuhakikisha kwamba watumishi ambao tunawapeleka kule basi wanatengenezewa mazingira wezeshi ya kuweza kufanya kazi zao vizuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 471

Elimu Dhidi ya Athari za Ndoa za Utotoni

MHE. FATMA H. TOUFIQ aliuliza:-

Ndoa za utotoni ni tatizo kubwa katika jamii zetu hususan katika jamii zenye umaskini:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa umma hasa katika maeneo ya vijijini ili wananchi wafahamu athari za kuoza watoto katika umri mdogo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa elimu kwa umma katika kupambana na ndoa za utotoni ambazo zina madhara makubwa kwa watoto wa kike

ambapo kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo TV, redio, magazeti na jarida imekuwa ikitoa elimu kwa umma kwa kuandaa ujumbe kuhusu madhara ya mimba za utotoni sambamba na kusisitiza wazazi na walezi na jamii kwa ujumla kutoozesha watoto mapema. Aidha, mwaka 2017, Tarime Mkoani Mara, Serikali ilizindua kampeni ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni ijulikanayo kama "Mimi Msichana Najitambua: Elimu Ndiyo Mpango Mzima".

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hiyo lilenga kutoa elimu kwa watoto kuhusiana na mimba za utotoni na umuhimu wa kuelekeza muda wao mwingi katika elimu, kujitambua na kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki zao. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2018, jumla ya wananchi 13,234 walifikwa na kampeni. Kati ya hao, wanafunzi 8,546, walimu 476, viongozi wa dini 110, wazee wa mila na wazee mashuhuri 90, ngariba 38, waendesha bodaboda 261, wazazi/walezi 3,600 na watendaji wa kijiji 113. Kampeni hii imefanyika katika Mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Lindi, Dodoma, Tanga, Dar es Salaam na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto. Sambamba na mpango huo, mwaka 2018, uliandaliwa Mdahalo wa Kitaifa ambao ulikuwa na lengo la kujadili vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwemo ndoa za utotoni. Mikoa yenye kiwango kikubwa cha ukatili dhidi ya watoto ilijumuishwa katika utaratibu wa kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa kampeni ambayo umeainisha jumbe za kipaumbele zitakazotumika na mikoa katika kuelimisha jamii katika mikoa husika kwa kuzingatia mazingira yao. Mikoa sita ilijumuishwa ikiwa ni pamoja na Shinyanga, Dodoma, Tabora, Mara, Katavi na Singida.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya

nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali yangu ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, idadi ya wananchi 13,234 waliofikiwa pamoja na wadau wengine ni ndogo sana kulingana na idadi ya watu tuliopo katika nchi hii. Nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuwafikia wananchi ili kampeni hii iweze kufika katika eneo kubwa zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, naipongeza sana Serikali kwa kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili pamoja na ndoa za utotoni. Hata hivyo, Mpango Kazi huu haufahamiki katika maeneo mengi na pia hata baadhi ya Wabunge hawafahamu. Je, Serikali haioni umefikia wakati sasa kuishirikisha jamii katika kampeni hii ili kuwanusu watoto wetu wa kike? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze amekuwa ni mdau mkubwa sana ambaye amekuwa anafuatilia haki mbalimbali na ustawi wa watoto wa kike pamoja na wanawake katika Mkoa wa Dodoma na Tanzania kwa ujumla. Nikupongeze sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maswali yake mawili, la kwanza ni kuhusu idadi ndogo ambayo tumeweza kuifikia. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tulianza katika mikoa sita na tulijaribu kulenga maeneo ambayo tumekuwa na changamoto kubwa sana ya mimba za utotoni. Takwimu zetu za Kitaifa zinaonesha kwamba asilimia 27 ya mabinti kati ya miaka 15-19 aidha wana ujauzito

au wameshazaa na Mkoa wa Katavi ndiyo unaongoza kwa takriban asilimia kama 49 na mikoa mingine ambayo tumekwenda kule katika kampeni yetu inaonesha kwamba ni ile mikoa ambayo kwa kweli ina mzigu mkubwa sana katika tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaribu sana kushirikisha makundi mbalimbali katika hili zoezi, siyo tu kwenda kuongea na jamii lakini tumejaribu kuangalia makundi gani ambayo yanaweza yakatusaidia kuweza kufikisha ujumbe. Tumeongea na viongozi wa kimila, kidini, Serikali, watu wa bodaboda, walimu na jamii kwa ujumla, lengo ni kuhakikisha kwamba ujumbe huu unafika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumekuwa tunatumia vyombo vya habari kwa kutumia televisheni, magazeti na majarida. Pia sasa hivi jambo lingine ambalo tumeanza kufanya ni matumizi ya sanaa katika kuhakikisha kwamba tunafikisha ujumbe. Tumeanza kufanya maongezi na wasanii mbalimbali ili na wao watusaidie kufikisha sauti zao kwa njia zao kwa makundi ambayo nao wanaongea nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili ambalo ameliulizia ni huu Mpango Kazi wa Serikali wa Kutokomezwa Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto na mimba za utotoni. Sisi kama Serikali tumeshaanza mkakati wa kuhakikisha kwamba hizi Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya vijiji zinatengenezwa na zinafanya kazi. Mpaka sasa hivi tuna Kamati takriban 10,000, tunaendelea kuziimarisha na kuzijengea uwezo ili nazo ziweze kwenda kusimamia majukumu haya ya kuhakikisha kwamba ukatili wa kijinsia ikiwa ni pamoja na mimba za utotoni unaondoka katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, tafiti zinaonesha kadri tunavyoendelea kuboresha elimu ndiyo hivyo hivyo mabinti wanachelewa kupata ujauzito. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais

(TAMISEMI) tutaendelea kuboresha mkakati wa kuonesha kwamba wasichana wote wanaendelea kukua shuleni ili kuanza kupunguza hili suala la ndoa na mimba za utotoni.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia swali letu la mwisho la Wizara ya Madini, Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu sasa aulize swali lake.

Na. 472

Ushauri kwa Vijana Wanaochimba Madini

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA aliuliza:-

Kumekuwa na dalili za upatikanaji wa madini ya dhahabu katika Vijiji vya Kabingo, Ruhuru, Nyakayenzi, Nyamwilonge na Muhange Wilayani Kakonko na katika baadhi ya vijiji uchimbaji umeanza:-

Je, Serikali inatoa ushauri gani kwa vijana ambao wapo tayari kujishughulisha na uchimbaji wa madini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Madini, majibu.

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na dalili za upatikanaji wa madini ya dhahabu katika Vijiji vya Kabingo, Ruhuru, Nyakayenzi, Nyamwilonge na Muhange, Wilayani Kakonko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa katika Kijiji cha Nyamwilonge uchimbaji unaendelea na Serikali imekwishakutoa leseni saba kupitia Tume ya Madini, leseni

za uchimbaji mdogo (*primary mining licence*) kwa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Mei, 2017, Wizara ya Madini kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*) ilifanya utafiti wa awali ambao uliombwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kubaini maeneo yenye madini ya dhahabu. Katika ripoti yake ilibainika uwepo wa dhahabu katika Vijiji vya Nyakayenzi, Nyakahura na Nyamwilongo. Pia ripoti hiyo ilishauri utafiti wa kina ufanyike ili kujua kiwango cha wingi na upatikanaji wa dhahabu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini inashauri vijana wote wanaotaka kujishughulisha na shughuli za uchimbaji madini kwenye maeneo hayo, wafike kwenye Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Kigoma ili waweze kupewa ushauri wa kitaalam pamoja na kuelimishwa kuhusu utaratibu wa kufuatwa kupata leseni ya uchimbaji madini ili waweze kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christopher Chiza, swali la nyongeza!

MHE. ENG. CHRISTPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amefika Kakonko na kuzungumza na wadau ambao wanataka kuchimba madini hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, Naibu Waziri alipokuja wadau walimwonesha nia ya kuchimba madini haya pamoja na madini ya chokaa, yanayopatikana kwa wingi katika Wilaya ya Kakonko na katika Mkoa wa Kigoma ambayo yanatumika sana kwa shughuli za ujenzi, shughuli za kulainisha ngozi na kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwa kuwa sisi tumejiandaa katika Wilaya ya Kakonko, kujenga kiwanda cha kuchakata chokaa kuwasaidia vijana. Katika majibu ya

Mheshimiwa Waziri, sehemu ya tatu, Mheshimiwa Waziri ameshauri vijana wote wanaotaka kushughulika na uchimbaji wafike kwenye Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Kigoma. Kutoka Nyamwilonge mpaka Kigoma ni kilomita zaidi ya 300. Swali la kwanza, je, haoni kwamba ingekuwa busara sasa, badala ya vijana wote hawa kwenda Kigoma kilomita 300, amwagize Afisa Mkazi huyu wa Madini yeye ndiye awatembelee kuwapa ushauri kule waliko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa madini ya chokaa yanapatikana kwa wingi katika Wilaya ya Kakono na katika Mkoa wa Kigoma, lakini katika Wilaya ya Kakonko, madini yote haya yapo katika Pori la Akiba la Moyowosi, ambalo Serikali inawazuia kuchimba au kufanya shughuli za uchimbaji katika pori la akiba. Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari sasa kukaa na Wizara ya Maliasili ili kuangalia uwezekano wa Wizara hizi mbili kutoa kibali kwa wachimbaji hawa kufanya uchimbaji salama ili waweze kuchimba chokaa hii? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Madini, majibu!

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nianze tu kumpongeza sana Mheshimiwa Chiza kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele sana kushughulika na suala la madini kwenye Wilaya ya Kakonko na kama utakumbuka tarehe 5 mwezi wa Aprili, aliuliza swali hapa hapa kwa ajili ya madini ya chokaa na leo ameuliza kwa ajili ya madini ya dhahabu, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze tu kwamba ni kweli, tumeweka Ofisi za Madini kila Mkoa ambazo kazi yake ni kutoa huduma kwa watu wanaotaka kujishughulisha na uchimbaji wa madini na sasa kutoka Kakonko kwenda Kigoma pana umbali mrefu sana. Nakubaliana naye, kwamba, Afisa Madini awatembelee aweze kutoa elimuj

hiyo. Pia nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge, yeye pamoja na wale vijana wapange tarehe, tarehe fulani watakuwa tayari, Afisa Madini atakuja pale kuwapa elimu juu ya utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa madini haya yako kwenye hifadhi na kwamba wanataka wachimbe ndani ya hifadhi ya Kigosi. Naomba tu nimjulisha kwamba Mheshimiwa Mbunge, utaratibu uliopo ni kwamba, Wizara ya Madini wajibu wake ni kutoa leseni ya Madini (*Mineral Right*) na mwenye wajibu wa kutoa kibali kwa ajili ya mtu kupata *access* ya kuingia kwenye mapori hayo ni yule mwenye *surface right* ambaye kwa mujibu wa sheria ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, yeye pamoja na wenzetu Wizara ya Maliasili na Utalii, wazungumze kuona namna gani bora wanaweza kupata kibali cha kuwea kufanya kazi kwenye maeneo hayo kama Sheria ya Maliasili itaruhusu. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali, nilete kwenu matangazo tuliyonayo siku ya leo.

Tangazo la kwanza linahusu wageni walioko hapa Bungeni na kundi la kwanza ni wageni waliopo jukwaa ya Mheshimiwa Spika, na kwanza kabisa ni wageni 63 wa Naibu Spika ambao ni Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, kutoka Jijini Mbeya, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Vijana Jijini Mbeya. Ndugu Zaituni Rajab Hamis. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni mwingine ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Mkoa wa Mbeya. Ndg. Oliva Asukenye Kibona. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni 74 wa Mheshimiwa Suleiman Jafo, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na hawa ni viongozi katika Wilaya Kisarawe na Wajumbe wa Kamati mbalimbali kutoka Halmashauri ya wilaya hiyo, wakiongozwa na

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kisarawe, Ndugu Halfani Siki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na huyu ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa na pia ni Diwani wa Kata ya Mwanga Kusini, Manispaa ya Kigoma Ujiji, Mkoa wa Kigoma, huyu ni Mheshimiwa Mussa Maulid. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Mwita Waitara, ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ni wawakilishi wa Walimu na Wanafunzi wa Sekondari, Mkoa wa Ruvuma ambao wameshinda mashindano ya UMISETA ya mwaka 2019. Wawakilishi kutoka, karibuni sana. Hawa ni wawakilishi wa Mkoa wa Ruvuma kwa upande wa shule na wanafunzi wa Mkoa wa Ruvuma, walikuwa washindi wa UMISETA Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Pia, katika hawa yuko mwanafunzi ambaye ndiye alikuwa goal keeper bora kabisa, Nice Julius Kahemele. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri yeye anataka kutoa unabii kwamba Nice anaweza goal keeper wa Timu ya Taifa itakapokwenda *AFCOM* mwaka 2023, atakuwa kakamilisha masomo yake. Karibu sana Nice na hongera sana kwa kuwa *goalkeeper* bora wa michezo ya UMISETA, 2019. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Josephat Kandege ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu wa Shule Binafsi Tanzania (*TPTU*), Ndugu Cornel Burpolloh na Ndg. Julius Mabula. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, ambaye ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu wenye Ulemavu) na huyu ni Ndugu Mwita Marwa, mkazi wa Dodoma

ambaye anafanya shughuli za kutengeneza viti mwendo (*wheelchairs*) kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Karibu sana Ndg. Mwita Marwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo yetu tunafahamu wako watu mbalimbali wenye ulemavu ambao huwa wanahitaji hivi viti mwendo, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuwatengeneza viti hivyo wale watu wenye ulemavu kwenye maeneo yao ambao wanahitaji vit mwendo, basi wanaweza kumuona Ndugu Mwita Marwa, yeye anatengeneza mwenyewe hivyo viti na kwa hivyo, mnaweza pia kumsaidia katika uwekezaji wake na yeye akawa ni mtu ambaye anaweza kutengeneza kiwanda kabisa cha kutengeneza hivi viti mwendo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wanaotokea *Foundation for Women Developments Quest* wakiongozwa na Ndugu Flora Festo Mvungi. Karibuni sana na nimefurahi kuwaona kuna akinababa hapo ambao inaonekana wanaunga mkono juhudi za maendeleo ya mwanamke. (*Makofi*)

Pia tuna wageni 40 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, ambao ni viongozi wa wasanii wa bendi zote za muziki wa *dance* kutoka Jijini Dodoma. (*Makofi*)

Karibuni sana, Waheshimiwa Wabunge inavyoonekana, Dodoma, Jiji la Dodoma wamejipanga vizuri. Kama kikosi kazi hicho chote ni cha viongozi tu wa muziki na *dances* masihara. Wako tayari kuwapokea wahamiaji wote Dodoma. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na hawa ni Viongozi wa Baraza la Wazee Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani na hawa ni Ndugu Abdul Lugome, Ndugu Abdallah

Legele na Ndugu Said Majiwa. Karibuni sana viongozi wetu.
(*Makofi*)

Tunao pia wageni 60 wa Mheshimiwa Mendrad Kigla ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mufindi, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ndugu Zuhura Mbuma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 30 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni Wachungaji kutoka Kanisa la KKKT Mbulu Vijijini, Mkoa wa Manyara, wakiongozwa na Mchungaji Marcel Daniel. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 18 wa Mheshimiwa Dkt. Suleiman Yussuf, ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ali Bakar. Karibuni sana, hawakusema hapa lakini bila shaka wanatokea Zanzibar hawa. Bila shaka na wengine naambiwa wanatoka Mbeya, kwenye kundi hilo. Haya, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambao ni Walimu wa Shule ya Msingi Vikawe kutoa Wilaya ya Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Mkuu, Ndg. Franco Vigao. Sijui wamekaa upande gani, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Maida Abdallah ambao ni wadau wa Elimu wakiongozwa na Mkuu wa Shule ya Sekondari *Fountain Gate* ya Jijini Dodoma, naye ni Ndg. Dennis Joel. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambao ni ndugu zake kutoka Muheza Mkoa wa Tanga wakiongozwa na kaka yake Ndugu Godfrey Komba. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambao ni Viongozi wa Baraza la Vijana, CHADEMA kutoka Karatu, Mkoa wa Arusha, nao ni Katibu Mwenezi

Ndugu John Akonaay na Mwenyekiti wa Vijana, Kata ya Karatu Ndugu Merus Ammi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, nao ni wageni 90 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Martin Luther ya Dodoma Mjini wakiongozwa na Mwalimu Gilbert Nuguti. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tullionao Bungeni siku ya leo na kwa upande wa wageni mnakaribishwa sana Bungeni na kwa wale waliotoka mbali, mnakaribishwa sana Dodoma.

Tangazo la pili linatoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Mo Bunge, Mheshimiwa Shally Raymond, anawatangazia Wakristo wote Wakatoliki, kwamba leo baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, saa saba mchana, katika Ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili kutakuwa na Ibada. Waheshimiwa Wabunge wote, Wakristo wote na wageni wote wanaoweza kushiriki ibada hiyo wanakaribishwa.

Baada ya matangazo hayo, Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamida!

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kueleza hoja yangu. Natumia Kanuni ya 68(7). Kwa kuwa swali namba 460 lililoulizwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, limeeleza mafanikio makubwa ya Serikali yaliyotekelezwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja za upotoshaji zinazoendelea katika maeneo yetu hasa Mkoani kwetu Lindi. Wapo wanasiasa ambao wanataka, wanaoendelea

kupotosha wananchi katika kujiimarisha kisiasa wakitumia hoja za ununuzi wa korosho, hoja za vitambulisho vya wajasimali, ambavyo Mheshimiwa Rais alivitoa, lakini pia hoja ya kupinga mafanikio makubwa yanayofanywa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba sasa Serikali itoe tamko la hoja hizi zikiendelea katika Mkoa wetu wa Lindi zinaweza zikasababisha uvunjifu mkubwa wa amani katika Mkoa wetu wa Lindi na hoja hizi zinaendelea hivi sasa ninavyozungumza katika eneo letu la Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, ningependa kujua sasa, Serikali inasema nini juu ya hoja hizi ambazo zinaweza zikaleta athari kubwa mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hakuna mtu mwingine alikuwa amesimama wakati Mwongozo ukiombwa, kwa hiyo ni huyo mmoja tu atajibiwa.

MBUNGE FULANI: Mwongozo, nilikuwa nimesimama! Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Hamida Abdallah akieleza mambo yanayotokea Lindi na ameyahusianisha na swali namba 460 la Mheshimiwa Gulamali ambalo lilikuwa likieleza kuhusu mafanikio mbalimbali ya miradi ya Serikali kwenye eneo lake na yeye anaeleza kwamba Mkoani Lindi kuna upotoshaji unaoendelea huko wa mambo mbalimbali kama ambavyo ameyataja.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo kwa Kanuni ya 68(7), inataka jambo linaloombewa mwongozo liwe limetokea hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, uhalisia, uthibitisho, ama ukweli wa hayo mambo yanayotokea Lindi, hapa ndani

hayajajadiliwa kwa hivyo, mimi siwezi kuyatolea mwongozo wowote, lakini Serikali kama inaona kuna jambo lolote la kufuatilia katika hayo inaweza ikachukua hatua.

Katibu!

NDG. MOSSY V. LUKUVI - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
Na. 4 wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous
Amendments) No. 4 Bill 2019*)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
Na. 5 wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous
Amendments) No. 5 Bill 2019*)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa
Mwaka 2019 (*The e-Government Bill, 2019*)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, imesomwa Miswada mitatu hapa kwa mara ya kwanza na kwa mujibu wa taratibu zetu, Miswada hii itapelekwa kwenye Kamati zinazohusika ili iifanyie kazi. Waheshimiwa Wabunge itakapofika huko kwenye Kamati basi muitendee haki maana

Bunge zima linategemea mawazo yenu mtakayoyaleta hapa. Pia kwa sababu Miswada hii imeshasomwa kwa mara ya kwanza, wale ambao wanaona kuna Muswada ambao wangependa kushiriki basi wanaweza kwenda kushirikiana na hizo Kamati zitakazopelekewa Miswada hii kwa utaratibu wetu wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019
(The Finance Bill 2019)

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nieleze kidogo kabla sijamuita Mheshimiwa Naibu Waziri, mtakumbuka jana wakati tukihitimisha hoja ya Bajeti ya Serikali, Mheshimiwa Waziri hakuwa katika hali nzuri sana kwa sababu hiyo *care taker* wa Wizara hiyo kwa sasa na kwa muktadha wa jambo hili lililo mbele yetu ni Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, karibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 *(The Finance Act 2019)* pamoja na marekebisho yake sasa Usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, wakati tulipowasilisha Muswada huu mbele ya Kamati kwa ajili ya

kupata maoni na ushauri. Aidha, katika kipindi chote cha majadiliano, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu vyanzo mbalimbali vya mapato pamoja na namna bora ya kukusanya kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu kwa kiwango kikubwa umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati. Serikali itaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine ya Kamati ambayo hayakuingizwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia katika hotuba ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni tarehe 25 Juni, 2019. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam wake wa Uandishi wa Sheria kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake, wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kwa kiwango kikubwa umezingatia ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa viwanda, wafanyabiashara, taasisi mbalimbali binafsi na taasisi za Serikali. Serikali ilishirikisha wadau hawa katika uchambuzi wa hatua za kodi ambazo zimebainishwa kwenye Muswada huu katika ngazi mbili. Kwanza, kupitia kwenye Kikosi Kazi cha Maboresho ya Mfumo wa Kodi (*Task Force on Tax Reforms*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mapendekezo kutoka kwenye Kikosi Kazi yalijadiliwa kwenye Kamati ya Ushauri kwa Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu hatua za mapato (*Advisory Committee on Revenue Measures*).

Vilevile, baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa kwenye mkutano baina ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wafanyabiashara mbalimbali uliofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 7 Juni, 2019 yamezingatiwa ndani ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho sheria tisa (9) zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali ili kuweka mfumo wa kodi ambao ni tulivu na unaotabirika, kuboresha taratibu za ulipaji na ukusanyaji kodi na kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kwenye sekta za kilimo na viwanda na hatimaye kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali. Sheria zinazofanyiwa marekebisho au kufutwa ni zifuatazo:-

- (i) Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura 365;
- (ii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
- (iii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
- (iv) Sheria ya Tozo ya Huduma za Bandari, Sura 264;
- (v) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168;
- (vi) Sheria ya Viwango, Sura 130;
- (vii) Sheria ya Chakula, Madawa na Vipodozi, Sura 219;
- (viii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; na
- (ix) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu 10 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza yenye Ibara ya 1 na 2 inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2019 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 cha Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura 365 ili kuweka sharti kwa mawakala wa ukusanyaji wa tozo ya huduma ya viwanja vya ndege kuwasilisha *return* ya kila mwezi kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Lengo la hatua hii ni kurahisisha ukaguzi wa hesabu pamoja na kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa bidhaa, Sura 147, kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe Ushuru wa Bidhaa kwenye vilainishi vya ndege (*lubricants*) vinavyoingizwa nchini au kununuliwa ndani ya nchi na Mashirika ya ndege ya ndani yaani *local operators* au mashirika ya ndege yanayotambulika katika mikataba ya Kimataifa ya huduma za anga (*Bilateral Air Services Agreements*).

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuimarisha sekta ya usafiri wa anga na kuiwezesha nchi yetu kusaini mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo.

(ii) Kurekebisha Jedwali la Nne ili:-

(a) Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 10 kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa ndani ya nchi na asilimia 25 kwenye nywele bandia zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambuliwa kwa *HS Code 67.03, 67.04 na 05.01*. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

(b) Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa asilimia 10 kwenye bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake

vinavyotumika kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji kwa kuwa hivi sasa kuna viwanda vingi vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hizo na kutosheleza mahitaji hapa nchini. Hatua hii inahusisha bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake vinavyoingizwa nchini pekee na vinavyotambuliwa katika *HS Code 39.17*. Lengo la kutoza Ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa hizo ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza fursa za kazi, ajira na mapato ya Serikali.

(c) Kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda kama ndizi, mabibo, rozela/choya, nyanya na kadhalika yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka Sh.200 kwa lita hadi Sh.61 kwa lita ikiwa ni punguzo la Sh.139 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vidogo vidogo vya aina hii, kuongeza thamani na hivyo kuhamasisha kilimo cha mazao hayo. Aidha, bei ya kinywaji hicho kwa sasa ni sawa na bei ya vinywaji baridi.

(d) Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa Sh.8,000 kwa kilo kwenye bidhaa za tumbaku ya kusokota (*cut rag* au *filler*) zinazozalishwa hapa nchini kwa kutumia tumbaku ya ndani kwa kiwango cha zaidi ya asilimia 75. Hapo awali bidhaa hizo zilikuwa zinatozwa Sh.28,232.40 kwa kilo kwa bidhaa za ndani na zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuhamasisha kilimo cha tumbaku hapa nchini na kulinda afya za walaji ambao walikuwa wanatumia tumbaku ya kienyeji yenye madhara makubwa kiafya na vilevile hatua hii itaongeza fursa za ajira na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kama ifuatavyo:-

(i) Katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii kwa:-

(a) Kurekebisha aya ya 2(2) ili kuondoa wajibu wa kutengeneza hesabu zinazotakiwa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya ukokotoaji wa Kodi ya Mapato kwa walipa kodi binafsi yaani *presumptive taxpayers* wenye mauzo ghafi ya shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 100 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa mlipa kodi binafsi ya kutafuta mtaalam (*Certified Public Accountant*) kwa ajili ya kutengeneza hesabu. Aidha, hatua hii inalenga pia kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza mapato ya Serikali.

(b) Kufuta Jedwali dogo lililopo chini ya aya ya 2(3) ili kupunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka Sh.150,000 hadi Sh.100,000 kwa mwaka kwa wafanyabiashara wenye mauzo yanayozidi Sh.4,000,000. Lengo la hatua hii ni kupunguza mzigo wa kodi kwa walipa kodi wadogo pamoja na kuoanisha viwango vya kodi na kiwango cha chini kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kutumia mashine ya kodi ya kielektroniki ambacho kwa sasa ni Sh.14,000,000. Aidha, hatua hii inalenga pia katika kusisitiza matumizi ya mashine za kielektroniki ili kuwezesha ukokotoaji wa kodi ulio sahihi na kuongeza ulipaji kodi wa hiari.

(c) Kurekebisha aya ya 3(2) kwa kuongeza aya ndogo ya (d) ili kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni yaani *Corporate Income Tax* kutoka asilimia 30

hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe 1 Julai, 2019 hadi tarehe 30 Juni, 2021 kwa wazalishaji waliopo na wazalishaji wapya watakaowekeza kwenye viwanda vya kuzalisha taulo za kike. Aidha, wazalishaji hao watalazimika kuingia mkataba wa utekelezaji na Serikali yaani *Performance Agreement* unaoainisha wajibu wa kila upande.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu na hivyo kupungua kwa bei yake, kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Vilevile hatua hii itahamasisha uzalishaji wa bidhaa hii ndani ya nchi na hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaona kutakuwepo na mgongano wa maslahi kwa TRA kwani itatakiwa kukusanya mapato na kuondosha mizigo. Kamati inaishauri Serikali kuwa Mamlaka ya Mapato ibaki na jukumu lake msingi la kukusanya kodi na suala la kuondosha mizigo bandarini liachwe kwa mawakala na taasisi nyingine za Serikali ambazo zinatekeleza jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukwamua miradi ya wafadhili na wahisani wa maendeleo iliyokwama kutokana na msamaha wa kodi uliotolewa kutohusisha miradi iliyoanzishwa kabla ya mabadiliko ya sheria. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Bunge lilifanya mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, kifungu cha 6, ili kutoa msamaha kwa miradi ya wafadhili pamoja na ile ambayo Serikali imeingia mikataba na wahisani wa maendeleo. Lengo la mabadiliko haya lilikuwa ni kukwamua changamoto katika utekelezaji wa miradi iliyokuwepo kabla ya mabadiliko ya sheria. Hata hivyo, utekelezaji wa mabadiliko hayo haukuweza kutatua changamoto hiyo kutokana na ukweli kwamba sheria iliyotungwa hairudi nyuma (*retrospective*). Aidha, Serikali imeahidi kuwa itaandaa mwongozo wa kutatua changamoto hiyo ili kuruhusu miradi iliyoanzishwa kipindi cha nyuma kunufaika na msamaha huo. Ni maoni ya Kamati kuwa suala hili litafanyiwa kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 (*The Local Government Finance Act*). Kifungu cha 16(6) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kinaweka masharti ya kutotoza ushuru wa mazao kwa wanunuzi wa mazao yanayouzwa nje au kuyaongeza thamani mazao ya kilimo, hivyo wanawajibika kulipa ushuru wa huduma (*service levy*) tu. Kifungu hiki kimesababisha baadhi ya Halmashauri kushindwa kukusanya ushuru wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani Halmashauri za Mkoa wa Tanga zinashindwa kukusanya ushuru wa mazao kwa zao la mkonge kwa kuwa zao hilo kwa kiasi kikubwa linanunuliwa na kuuzwa nje ya nchi. Hivi sasa kwa Mkoa wa Tanga peke yake mapato yanayotokana na *service levy* asilimia 0.03 kwa zao la mkonge ni Sh.932,051,137.79, kiasi kilichotakiwa kulipwa kutokana na msamaha wa ushuru wa mazao wa asilimia 3 ni shilingi Sh.9,320,000,000. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko ya kifungu hiki cha sheria ili kuruhusu ukusanyaji wa ushuru wa mazao kwenye zao la mkonge maana Serikali inapoteza mapato mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa na maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2019/2020 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Ndugu Dotto James, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu wawili. Niwashukuru pia Prof. Florence Luoga, Gavana wa Benki Kuu; Ndugu Athumani Mbutuka, Msajili wa Hazina; Dkt. Edwin Mhede, Kamishna mpya wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Prof. Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa masuala kodi waliofika mbele yake na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuiwezesha Kamati kuweza kutoa maamuzi sahihi. Aidha, pia niwashukuru Wabunge wengi walioweza kufika ambao siyo Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, lakini walikuja kwenye Kamati ya Bajeti kwa nia ya kutusaidia kwa mujibu wa Kanuni inayoruhusu Wabunge wengine kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Kwa sababu ya muda sitawataja Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa namna ya pekee, naomba kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe,

Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti; Ndg. Mathew Kileo, Mkurugenzi Msaidizi na Makatibu wa Kamati; Ndg. Godfrey Godwin; Ndg. Emmanuel Rhobi; Ndg. Lilian Masabala na Ndg. Maombi Kakozi pamoja na Wanasheria wa Ofisi ya Bunge akiwemo Ndg. Prudence Rweyongeza na Ndg. Seraphine Tamba kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2019 (*THE FINANCE BILL, 2019*) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (*The Finance Bill, 2019*).

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Juni, 2019, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/20, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi na kiutawala zitakazochukuliwa na Serikali zenye lengo la kuongeza mapato, kuimarisha usimamizi wa kodi pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Baada ya wasilisho hilo Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipewa jukumu la kuuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 pamoja na kushauriana na Serikali kisha kutoa maoni na mapendekezo kuhusu muswada huo.

1.1. Madhumuni ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 una lengo la kufanya marekebisho kwenye Sheria mbalimbali kwa kubadili mfumo wa kodi, ushuru na tozo

mbalimbali. Marekebisho hayo yamejikita katika kurekebisha viwango, kupunguza, kufuta baadhi ya kodi, ushuru na tozo mbalimbali. Kimsingi, Muswada huu umelenga kufanya marekebisho ya sheria zipatazo kumi (10).

1.2. Uchambuzi wa Muswada

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti, kwa nyakati tofauti ilifanya vikao na wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na masuala mengine ya kikodi na kiutawala ili kupata maoni yao. Kati ya Tarehe 20 na 21 Juni, 2019 Kamati ilikutana na Wadau wafuatao: - Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation-TPSF*), Wamiliki wa Viwanda Tanzania (*Confederation of Tanzania Industries -CTI*), Baraza la Kilimo (Agriculture Council of Tanzania), Wadau wa Michezo ya Kubahatisha, Kiwanda cha Sigara (TCC), Wazalishaji wa mafuta ya Alizeti nchini, Umoja wa Mawakala wa Forodha (TASAA), Umoja wa Mabenki Nchini (TBA), Jumuiya ya Wazalishaji wa Vyuma (SMA), Wadau wa Usafirishaji wa Ndege, Baraza la Makandarasi (CCA), Wadau wa sekta ya Bima, Wadau wa Sekta ya Usafirishaji, Baraza la Wanawake Wajasiliamali (TWCC) pamoja na Asasi za kiraia kama Vile Sikika na *Policy Forum*.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho pale inapobidi. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wa Wizara yake kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Kumi (10) zilizopo kwenye Muswada huu.

2.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2019

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu Kumi kama ifuatavyo:- Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi, Sehemu ya pili inapendekeza kufanya mabadiliko katika Sheria ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura 365, Sehemu ya tatu inafanya mabadiliko katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147, Sehemu ya Nne inahusu mabadiliko katika Sheria ya Mapato Sura 332, Sehemu ya

tano inafanya mabadiliko katika Sheria ya Huduma za Bandari Sura ya 264, Sehemu ya sita inafanya mabadiliko katika Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168, Sehemu ya Saba inafanya mabadiliko katika sheria ya Viwango Sura 130, Sehemu ya nane inafanya mabadiliko katika Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219, Sehemu ya Tisa inafanya mabadiliko katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 na Sehemu ya Mwisho inapendekeza kufanya mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148.

2.1. Sheria ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura ya 365 (*The Airport Service Charge Act*) na Sheria ya Huduma za Bandari Sura ya 264 (*The Port Service Charge Act*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili na ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisha katika Sheria za Huduma za Viwanja vya Ndege Sura 365 na Sheria ya Huduma za Bandari Sura ya 264 kwa kuongeza vifungu viwili vipya vya (3) na (4) katika Kifungu cha 7 cha sheria hizo. Maudhui ya marekebisho katika sheria hizi yana lengo sanjali la kuweka utaratibu, muda na namna ya kukusanya na kufanya marejesho (*returns*) ya tozo hiyo kwa Kamishina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Utaratibu unaopendekezwa haukuwepo kwenye sheria hizo awali hivyo ilisababisha kutokuwa na takwimu sahihi na taarifa muhimu kwa ajili ya ukusanyaji wa tozo hiyo toka kwa mawakala wa ndege ambao wanakusanya kwa niaba ya Mamlaka.

2.2. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147 (*The Excise (Management and Tariff) Act*).

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Kifungu cha 124(2) kinampa mamlaka Waziri kufanya mabadiliko ya viwango kwa bidhaa zisizo za petroli kwa kiwango cha mfumuko wa bei, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutofanya mabadiliko hayo kwa mwaka huu wa fedha na badala yake imekuja na vyanzo vipya vya mapato pamoja na kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya ushuru wa bidhaa kwa kuingiza

kifungu kipya cha **135A** mara baada ya Kifungu cha 135. Kifungu hiki kinatoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa vilainishi vya ndege (*Lubricants*) ambavyo vinaingizwa na Mashirika ya Ndege yanayotambulika katika mikataba na makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mataifa mengine. Baada ya majadiliano Serikali ilikubali kuongeza maneno "*Local operator of air Transportation*" ili kuondoa mkanganyiko ambao ungeweza kujitokeza kwa kuwa na maneno "*local operator*" tu. Aidha, Serikali ilihakikishia kamati kwamba kwa sasa hatuna wazalishaji wa ndani wa vilainishi hivyo na hatua hii haitakuwa na athari hasi kwa viwanda vya ndani kwa sababu hivi sasa havipo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kufanya marekebisho katika Jedwali la Nne kwa kuingiza HS code mpya baada ya HS code 2009.11.00 zenye lengo la kutoza Ushuru wa Bidhaa wa **asilimia 10** kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa nchini na **asilimia 25** kwenye nywele za bandia zinazotoka nje ya nchi zinazotambuliwa kwa HS Code 67.0367.04 na 05.01. Kamati inakubaliana na pendekezo hili kwa sababu kuu tatu kwanza; sababu za kimazingira ambapo baadhi ya nywele hizo zina athari sawa na ile ya mifuko ya *plastic* na pili; bidhaa hizo sio za lazima ni bidhaa za anasa (*luxury goods*) na *mwisho ni* kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na Serikali kukubali kufanya marekebisho ya kiuandishi katika HS code 39.17 ili maudhui yake yalenge bidhaa kutoka nje na si bidhaa zote kama ilivyokuwa inasomeka awali kwenye muswada. Hivyo Kamati inakubaliana na Serikali kutoza Ushuru wa Bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake vinavyotoka nje kwa **asilimia 10** ambazo zinafahamika kwa **HS Code 39.17** Lengo ni kulinda Viwanda vya ndani kwa kuwa vipo na vina uwezo wa kuzalisha bidhaa hiyo. Marekebisho hayo yamezingatiwa katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo

uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda kama ndizi, mabibo, rozela/choya na nyanya yanayozalishwa hapa nchini. Lengo ni kuhamasisha kilimo, uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo na kuongeza thamani ya mazao. Aidha, hatua hii inatokana na ukweli kwamba bei na gharama za uzalishaji wa bidhaa hizo zilikuwa chini kuliko kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kilichokuwa kinatozwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuanzisha HS Code mpya kwa ajili ya *cut fillers* zinazozalishwa ndani kwa ajili ya kutengenezea bidhaa ijulikanayo kama goso (*Making Roll on your own – RYO*). Hivi sasa mali ghafi ya kutengenezea bidhaa hizo hutupwa. Aidha, Hs Code hiyo itofautishwe na *cut fillers* inayotoka nje ambayo inatozwa kwa **shilingi 28,232**. Hatua hii itaongeza mapato ya Serikali kwa takribani **Shilingi bilioni 2** na itapunguza matumizi ya goso isiyo na ubora kwa wananchi ambayo kimsingi inakuwa sio safi na salama kwa sababu husokotwa kwa karatasi na tumbaku ambazo hazina utaratibu rasmi wa utunzaji. Hivyo baada ya ushauri huo Serikali ilikubali kuongeeza katika HS code 2403.19.00 kama inavyoonekana kwenye mabadiliko na kutoza jumla ya shilingi **8,000 sio 2,000** kama ilivyopendekezwa kama inavyoonekana katika hizo kupitia Jedwali la marekebisho. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi bilioni 8**.

2.3. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mabadiliko yanayopendekezwa kwenye Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki na imekubaliana nayo hasa kwa kuzingatia kwamba yana lengo la kulinda viwanda vya ndani ya jumuiya na kuchochea uzalishaji viwandani. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupeleka mapendekezo ya kuongeza ushuru wa bidhaa za nondo na vyuma vyenye **HS code 7214.20.00** ambazo nondo zitozwe ushuru wa **asilimia 35** au **Dola za Marekani 350** kwa tani au kiwango ambacho ni kikubwa (*Which ever is higher*). Lengo ni kulinda viwanda vya ndani ambavyo vina

uwezo wa kuzalisha na kutosheleza mahitaji ya bidhaa hizo nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa niaba ya Bunge inaleta rasmi pendekezo lake la kuangalia uwezekano wa kufanya mabadiliko kwenye sheria ya Bajeti kifungu cha 9(10) kwa kuongeza kipengele kipya cha (k) ambacho kitasomeka hivi *“ To review, analyse consider and approve on behalf of the Parliament all measures related to amendment of the East African Customs Management Act 2004 before they are tabled to the East Africa Council of Ministers Responsible for Finance, Trade and Investment”* Pendekezo hili lina lengo la kutoa fursa ya kisheria kwa Bunge ili kuiwezesha Kamati ya Bunge ya Bajeti kupitia mapendekezo yanayopelekwa katika Bunge la Afrika Mashariki, kwa ajili ya kupata maoni na mapendekezo ya Bunge. Hali ilivyo hivi sasa endapo Bunge linakataa mapendekezo haya utaratibu wa kuyarejesha katika Jumuiya ni mgumu na unachukua muda mrefu.

2.4. Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 (*The Income Tax Act,*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho yanayofanywa na Serikali Katika jedwali la kwanza kwa kuongeza kiwango cha juu cha walipa kodi ambao hawatunzi vitabu vya mahesabu (*presumptive tax*) kutoka **shilingi milioni 20,000,000** hadi kufikia kiwango cha **shilingi milioni 100,000,000**. Lengo ni kupanua wigo wa ukusanyaji kodi kwa walipa kodi walio chini ya utaratibu huo wa wasiotunza vitabu. Marekebisho hayo yameenda sambamba na kurekebisha jedwali la pili (2) aya ya tatu (3) ili liendane na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kufanya mabadiliko katika aya 3(2) kwa kuongeza aya (d) ambayo inaweka masharti kwa wawekezaji wapya na viwanda vilivyopo (*Existing Industries*) vya kutengeneza taulo za kike (*sanitary pads*) kupunguziwa kodi ya a mapato ya Kampuni kwa **asilimia 5** kutoka **asilimia 30** ya kisheria hadi **asilimia 25** kwa miaka miwili mfululizo kuanzia tarehe 1 Julai, 2019 hadi

30 Juni, 2021. Aidha, punguzo hilo litazingatia mikataba ya ufanisi kati ya Serikali na Makampuni husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kufanya marekebisho katika Jedwali la Pili kwa kuingiza maneno "*fees*" na "*charges*" kati ya maneno "*interest*" na "*paid*" yanayoonekana katika aya 1(v). Hata hivyo, kamati imeishauri Serikali kutumia maneno "*or other financial charges*" badala ya neno "*charges*" maboresho hayo yatawapa Serikali uwanja mpana zaidi wa tozo na gharama nyingine zitakazokuwa zikiambatana na mikopo hiyo zaidi ya zilizotajwa. Aidha, Kamati ilitahadharisha Serikali kwamba kama pendekezo hili limeletwa kwa ajili ya kukwamua mikataba iliyokwisha sainiwa, ni vema uandishi wake ukazingatia hilo kwani Sheria hairudi nyuma. Mapendekezo haya ya kamati yamezingatiwa na Serikali katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa Bungeni.

2.5. Sheria ya Usalama wa Barabarani Sura ya 148 (The Road Traffic Act)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kufanya marekebisho katika Kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Usalama barabarani kwa kuongeza muda wa kutumika kwa leseni kutoka miaka mitatu hadi miaka mitano. Hatua hii imeenda sambamba na kupandisha ada ya leseni hiyo kutoka **shilingi 40,000** ya sasa hadi **shilingi 70,000**. Vilevile, kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kupandisha ada za usajili wa magari kutoka **shilingi 10,000** ya sasa hadi **shilingi 50,000**, pikipiki za matairi matatu kutoka **shilingi 10,000** ya sasa hadi **shilingi 30,000** na pikipiki za matairi mawili kutoka **shilingi 10,000** ya sasa hadi **shilingi 20,000**. Lengo la hatua hizo ni kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kupunguza gharama za uchapishaji wa leseni na kuondoa usumbufu.

2.6. Sheria ya Viwango Sura 130 (The Standards Act)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo yote ya Serikali ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Viwango. Marekebisho hayo yameongeza Tafsiri za maneno

pamoja na kuongeza vifungu vipya kuanzia kifungu cha 21A hadi 21Y baada ya kifungu cha 21 cha Sheria hiyo. Vifungu vingine vilivyofanyiwa marekebisho vina lengo la kuiwezesha Sheria kubeba maudhui ya vifungu vilivyohamishiwa kutoka Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura ya 219. Kimsingi Tafsiri hizo za maneno na vifungu hivyo vimetolewa katika sheria ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Mazingira ya Biashara "*Blue Print*". Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kama ifuatavyo:-

i. Tunapokuwa tunatekeleza *blue print* kwa kufanya marekebisho mbalimbali inapaswa kuzingatia matakwa ya kimataifa (*international standards*) kuhusu masuala ya chakula na dawa;

ii. Kuhamisha majukumu ya TFDA kwenda TBS kuwe ni ahueni kwa wafanyabishara na wawekezaji na utekelezaji wake usiwe na mapungufu yaliyokuwepo TFDA. Endapo changamoto zilizokuwepo TFDA zitahamia TBS hatua hii itakuwa ni kuhamisha changamoto kutoka eneo moja kwenda lingine;

iii. Kwa kuwa, TFDA ilikuwa imejenga uwezo mkubwa katika masuala ya ukaguzi wa Chakula na Dawa ni vyema wataalamu pamoja na vifaa vilivyokuwa vinatumika kwa majukumu yaliyohamishwa navyo kuhamia TBS.

2.7. Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219 (*Tanzania Food, Drugs, and cosmetics act*)

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano Kamati imekubaliana na Serikali kufanya mabadiliko kwenye jina refu (*Long title*) katika Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219 na sasa sheria hiyo itaitwa "***Tanzania Medicines and Medical Devices Act***". Hatua hii ina lengo la kutambua mabadiliko yaliyofanyika ya kuhamishwa kwa baadhi ya majukumu yaliyokuwa kwenye Sheria hiyo kwenda katika Sheria ya Viwango. Vilevile, mabadiliko mengine yaliyofanyika ni kufuta masharti yote yanayohusu viwango vya usalama na ubora wa chakula na vipodozi yaliyokuwa yanafanywa chini ya Sheria hiyo.

2.8. Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 238 (*Tax Administration Act*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwanza; kukubali kutoa wigo wa miezi sita kutolipa kodi kwa biashara mpya baada ya kupata nambari ya Usajili ya Mlipa Kodi (*Tax Identification Number - TIN*). Aidha, Kamati baada ya mashauriano na Serikali ilionekana kwamba kifungu cha **22** kinachofanyiwa marekebisho kikiachwa kama kilivyo kingeweza kutumika vibaya. Hivyo utaratibu uliobainishwa katika jedwali la marekebisho ni wa kuahirisha kulipa kodi yaani "*deferment*" kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo ili kodi isilipwe kutokana na mtaji na badala yake kodi ilipwe kwa mikupuo mitatu (*Three installmentment*) mara baada ya kipindi cha miezi sita kuisha. Aidha, endapo itaonekana ni vigumu kufanya malipo hayo katika muda uliotajwa Sheria ya Usimamizi wa Kodi chini ya Kifungu cha 55 inampa mamlaka Kamishna Mkuu wa TRA kuangalia namna bora ya kulipa malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine kwenye Sheria hii yanalenga kutoa tafsiri ya maneno "*Fiscal device*" na "*Fiscal receipt*" ambayo hayakuwepo kwenye sheria hapo awali pamoja na kufanya marekebisho yenye nia ya kuleta maudhui sawa na mabadiliko yaliyofanywa katika Sheria za Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura ya 365 na Sheria ya Tozo ya Huduma za Bandari Sura 264.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha waheshimiwa Wabunge kwamba vitambulisho vya wajasiliamali vinakosa msingi wa kisheria na mwongozo wa namna ya utoaji wa vitambulisho vya wajasiliamali na hivyo kusababisha kero na mkanganyiko katika utekelezaji wake. Baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, imekubalika kufanya mabadiliko katika kifungu cha **22A** cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 238 ambayo inatoa fursa kwa Waziri kutunga kanuni (*Regulation*) kuhusu muda wa vitambulisho, ada ya vitambulisho, utolewaji wake pamoja na walengwa wa vitambulisho hivyo. Mabadiliko hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/20 imekusudia kuanzisha kitengo cha kupokea malalamiko ya Kodi. Kitengo hiki kinatarajiwa kufanya upembuzi na kuondoa changamoto zilizopo katika masuala yafuatayo; kwanza, ni kupokea na kuchambua malalamiko ya walipa kodi kuhusu utaratibu na usimamizi wa kodi na pili, ni changamoto zinazojitokeza wakati wa usimamizi wa kodi. Pendekezo hili halikuwa na msingi wa kisheria ili kuwezesha uanzishwaji wa Ofisi hiyo ya " *Tax Ombudsman*".

Mheshimiwa Spika, Baada ya majadiliano ya kina Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuongeza vifungu vipya vya **28A, 28B na 28C** kwa lengo la kuweka msingi wa kisheria wa kuanzisha ofisi hiyo na kubainisha majukumu yake pamoja na kuweka utaratibu wa kumteuwa kiongozi wa Ofisi hiyo. Pamoja na mapungufu machache katika mabadiliko hayo ambayo Serikali imekwisha yafanyia kazi kupitia jedwali lake la mabadiliko Kamati inaitaka Serikali kuanzisha mara moja ofisi hiyo ili kuondoa kadhia ya usimamizi wa kodi na ukwepaji wa kodi nchini. Hofu kubwa ya Wadau ni kwamba Kitengo hicho kisiwe chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango ili kiweze kuwa na uhuru wa kushughulikia masuala hayo. Endapo kitawekwa chini ya Wizara ya fedha au Mamlaka ya Mapato ni wazi kwamba kutakuwa na mgongano wa maslahi.

2.9. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 (Value Added Tax)

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inapendekeza kutoa msamaha kwa kodi kwenye vifaa vya kukaushia nafaka kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa (*post harvest loss*) nia ni kuchochea ukuaji wa kilimo cha mazao ya nafaka nchini. Vilevile, Serikali imekusudia kufanya marekebisho katika Sehemu ya kwanza ya jedwali la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye ndege, injini za ndege, vilainishi vya ndege pamoja na vipuri vya ndege kwa lengo la kuchochea ukuaji wa sekta ya usafiri na usafirishaji wa anga nchini. Hata hivyo, Kamati bado inaendelea kuitaka Serikali kuhakikisha kwamba msamaha

uliotolewa katika “*refrigerated containers*” ujumuishe wazalishaji na wasambazaji wa nyama, maziwa na samaki kwa sababu majokofu hayo pia yanatumika katika kusafirisha na kuhifadhi mazao hayo jinsi ilivyoandikwa hivi sasa inagusa mazao ya mboga mboga tu (horticulture).

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri wazi kwamba suala la kuondoa msamaha wa kodi ya ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike lilileta mjadala mkubwa sana katika kamati, katika suala hili kamati ilifanya majadiliano kwa muda mrefu na masuala yafuatayo yalibainishwa:-

i. Msamaha huo ulinufaisha viwanda vya nje kuliko viwanda vya ndani kwa sababu viwanda vya ndani havikuweza kudai kodi ya ongezeko la thamani waliyolipia kwenye malighafi na gharama nyingine za kuzalisha bidhaa hiyo;

ii. Kulikuwa na ongezeko kubwa la uingizaji wa taulo za kike kutoka nje kuliko kasi ya kushuka bei iliyokuwa ikitarajiwa;

iii. Viwanda vya ndani havikuweza kuwa na bei shindani katika soko na hivyo kuwa hatarini kusimamisha uzalishaji wa bidhaa hizo; na

iv. Msamaha huu haukuwanufaisha walengwa ambao ni wanafunzi wa kike na wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina na Serikali na kusikiliza mipango ya Serikali kuhusu hatua inazochukua kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Bariadi – Simiyu na Kiwanda cha MSD - Kibaha na kuzingatia hatua mbalimbali zilizokwisha kuchukuliwa katika Jumuiya ya Afrika mashariki kwa kutoa msamaha wa ushuru wa Forodha kwa watu maalumu (*Duty remission*) kwenye malighafi za utengenezaji wa taulo za kike tangu mwaka 2009. Pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kama zilivyoainishwa hapo juu, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali iendelee na jitihada hizo ili hakikisha taulo hizo zinapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu kwa wanafunzi wa kike na wanawake wenye kipato cha chini.

3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kupitisha muswada wa Sheria ya fedha:-

3.1. Sekta ya Ngozi nchini

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya ngozi kuna changamoto kuu mbili, moja ni **export levy** ya **asilimia 10** kwenye ngozi iliyosindikwa hadi kufikia kiwango cha *wet blue* na pili ni **asilimia 80** ya **export levy** kwenye ngozi ghafi. Kulingana na taarifa za wadau imeonekana kwamba kuna idadi kubwa cha ngozi kilichopo mikononi mwa wafanyabiashara hao ambacho kimekosa soko kutokana na tozo hizo. Kamati inaishauri Serikali kuangalia changamoto hizi kwa undani na kutoa suluhisho kwani wadau wa Sekta hiyo wanalalamikia tozo hizo na Taarifa zao zinaonesha kuwa baadhi yao wameanza kujihusisha na biashara ya magendo ili kukwepa tozo hizo. Hivyo, Serikali kupitia vyombo vyake ifanye utafiti wa kina ili kubaini kiasi cha ngozi kilichopo nchini, changamoto za soko la ngozi pamoja na uwezo wa viwanda vya ndani kutumia ngozi inayozalishwa nchini ili kuhakikisha ngozi zinazosemekana zipo mikononi mwa wafanyabishara wa ngozi zinapata soko.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali kuongeza kiwango cha *export levy* ya ngozi ya punda kutoka **sh. 5000** hadi **sh. 20,000** ili kuongeza mapato ya Serikali na pia kulinda punda waliopo nchini. Kimsingi, Punda anatumia muda wa miezi 11 hadi 14 kutoka kuchukua mimba hadi kuzaa. Hivyo, punda mmoja anazaa punda mmoja kwa mwaka. Kwa mantiki hii kuongezwa kwa kiwango hiki kitasaidia kupunguza biashara ya ngozi ya Punda na mazao yake nje ya nchi na hivyo kunusuru wanyama hawa kupungua.

3.2. Sekta ya Uvuvi Nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Sekta ya uvuvi imeathiriwa na hatua mbili kuu za kikodi kwanza; ni *export levy* ya dagaa wa Kigoma inayotozwa kwa **dola** za Kimarekani **1.5 kwa kilo** na kiwango cha mrabaha (royalty) cha dola za **kimarekani 0.4 kwa kilo**. Baada ya mashauriano, Serikali ilikubali kushusha kiwango cha *export levy*

kinachotozwa kwenye dagaa wa kigoma kutoka **dola ya marekani 1.5** kwa kilo hadi **dola 1** kwa kilo. Vile vile Serikali ilikubali kushusha *export levy* kutoka **dola za marekani 0.5** kwa kilo hadi **dola 0.3** kwa dagaa wa baharini na ziwa nyasa. Kwa upande wa mrahaba Serikali iliomba kupewa muda ili kulishughulikia jambo hili. Aidha, Kamati inashauri Serikali kufanyia kazi suala hili kwa haraka kwa sababu kwa kiasi kikubwa linaathiri shughuli za uvuvi katika bahari kuu na pia limesababisha Meli nyingi za uvuvi kutoka nje na ndani kushindwa kuvua kwenye bahari kuu hivyo kuikoshesha Serikali mapato.

3.3. Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mitambo ya kuchimbua visima pamoja na pampu za maji zinazotumia nguvu ya jua

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya majadiliano ya kina na Serikali na kuishauri kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani katika mitambo ya uchimbaji visima vya maji pamoja na kuondoa suala la uchimbaji wa maji kama huduma ya kibiashara. Kamati inaamini kwamba hatua hii itasababisha uingizwaji wa mitambo ya kuchimba maji kwa wingi na kushusha gharama za uchimbaji maji kwa Wananchi na Serikali yenyewe.

3.4. Msamaha wa Ushuru kwa Vifungashio vya Mvinyo

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kunusuru zao pekee la biashara la zabibu la Mkoa wa Dodoma. Hata hivyo, biashara hiyo bado inakabiliwa na kodi mbalimbali kama vile VAT pamoja na ushuru wa forodha kwa malighafi za vifungashio vya mvinyo ambavyo kimsingi havizalishwi nchini. Kamati inaishauri Serikali kufanyia kazi suala hili na kuhakikisha kwamba katika mwaka ujao wa fedha inatoa suluhisho la kudumu.

3.5. Uondoshwaji wa Mizigo Bandarini bila kutumia mawakala wa forodha.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 81, aya ya 51 ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali inapendekeza kuwekwa utaratibu utakaoruhusu wananchi wa kawaida kuondoa mizigo yao

bandarini bila kutumia mawakala. Kamati ilipata fursa ya kuongea na wadau wa forodha na Serikali na kubaini kwamba, Serikali inachokusudia ni kuanzisha dawati chini ya Mamlaka ya mapato ambalo litafanya kazi hizo. Hivyo, Mamlaka ya Mapato ndiyo itakuwa Wakala wa Wananchi wa Kawaida wakati wa kuondosha mizigo yao Bandarini. Aidha, kamati inaona kutakuwepo na mgongano wa maslahi kwa TRA kwani itatakiwa kukusanya mapato na kuondosha mizigo. Kamati inaishauri Serikali kuwa, Mamlaka ya Mapato ibaki na jukumu lake la msingi la kukusanya kodi na suala la kuondosha mizigo bandarini iliachwe kwa mawakala na Taasisi nyingine za Serikali ambazo zinafanya jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unazingatia ukweli kwamba utaratibu huu una changamoto za kisheria na pia unaweza kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa kawaida ambao hawana elimu ya uondoshaji wa mizigo bandarini, mipakani na kwenye viwanja vya ndege.

3.6. Kukwamua Miradi ya wafadhili na wahisani wa maendeleo iliyokwama kutokana na Msamaha wa kodi uliotolewa kutohusisha miradi iliyoanzishwa kabla ya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19 Bunge lilifanya mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya ongezeko la Thamani Sura 148 kifungu cha 6 ili kutoa msamaha kwa miradi ya wafadhili pamoja na ile ambayo Serikali imeingia mikataba na Wahisani wa maendeleo. Lengo la mabadiliko hayo ilikuwa ni kukwamua changamoto katika utekelezaji wa miradi iliyokuwepo kabla ya mabadiliko ya sheria. Hata hivyo, utekelezaji wa mabadiliko hayo hayakuweza kutatua changamoto hiyo kutokana na ukweli kwamba Sheria inapotungwa hairudi nyuma (*Retrospective*). Aidha, Serikali imeahidi kuwa itaandaa mwongozo wa kutatua changamoto hiyo ili kuruhusu miradi iliyoanzishwa nyuma kunufaika na msamaha huo. Ni maoni ya Kamati kuwa suala hili litafanyiwa kazi haraka.

3.7. Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 (*The Local Government Finance Act*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16(6) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kinaweka masharti ya kutotoza ushuru wa mazao kwa wanunuzi wa mazao wanaouza nje au kuyaongeza thamani mazao ya kilimo, hivyo wanawajibika kulipa ushuru wa huduma (*Service levy*) tu. Kifungu hiki kimesababisha baadhi ya Halmashauri kushindwa kukusanya ushuru wa mazao. Mathalani, Halmashauri za Mkoa wa Tanga zinashindwa kukusanya ushuru wa mazao kwa zao la mkonge kwa kuwa zao hilo kwa kiasi kikubwa linanunuliwa na kuuzwa nje ya nchi. Hivi sasa kwa Mkoa wa Tanga peke yake mapato yanayotokana na *Service levy* (**asilimia 0.03**) kwa zao la mkonge ni **shilingi 932,051,137.79** na kiasi kilichotakiwa kulipwa kutokana na msamaha wa ushuru wa mazao (**asilimia 3**) ni kiasi cha shilingi **shilingi 9,320,511,377.90**. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika kifungu hiki cha sheria ili kuruhusu ukusanyaji wa ushuru wa mazao kwenye zao la Mkonge.

4.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2019/20 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nimshukuru Mhe Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha napenda nimshukuru Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Ndg. Doto James Katibu Mkuu pamoja na Kamishna Mpya wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Dkt Edwin P. Mhede na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa masuala ya kodi waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki Mbunge wa Maswa Magharibi pamoja na Wajumbe wote wa Kamati Bajeti kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo.

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
3. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb
5. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
6. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
7. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
8. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
9. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
10. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
13. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
14. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
19. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
20. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
21. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
22. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
23. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb
24. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
25. Mhe. Jumanne Kishimba Mb
26. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb
27. Mhe. Joseph George Kakunda Mb

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti

ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndg. Mathew Kileo, Mkurugenzi Msaidizi na Makatibu wa Kamati Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Maombi Kakozi pamoja na wanasheria wa Ofisi ya Bunge akiwemo Ndg. Prudence Rweyongeza na Ndg. Seraphine Tamba kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

George Boniface Simbachawene (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
26 Juni, 2019

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Nimuite sasa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini kabla hajaja kuna tangazo moja hapa.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba leo Saa 7.00 Mchana baada ya kusitisha Shughuli za Bunge kutakuwa na uzinduzi wa kitabu katika Ukumbi wa Msekwa. Kitabu hicho kinaitwa “ *Viwanda Moving Tanzania Forward*”. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Spika. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki zoezi hili la uzinduzi wa hiki kitabu muhimu sana katika awamu hii ambayo ni ya viwanda.

Mheshimiwa Silinde, karibu.

MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara nyingine tena ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa kutunga Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 (*The Bill to enact the Finance Act, 2019*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni haya, naomba kwanza kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kuendelea kutupatia uhai, busara na maarifa ya kuendelea kuishauri Serikali hata kama haiko tayari kupokea ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba Muswada huu ambao kimsingi unakusudia kutekeleza malengo ya Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2019/2020 ni Muswada ambao kiuhalisia hautaweza kusaidia kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika sekta ya viwanda ambayo ndiyo inabeba kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda. Ni Muswada ambao unalenga kutekeleza Bajeti ambayo si rafiki kwa sekta ya kilimo ambayo inajiri takribani asilimia 75 ya Watanzania wote na ukiachilia mbali mazingira yasiyo rafiki kwa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha na kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara kunahitaji jitihada za makusudi zinazochochewa na sera madhubuti, rafiki na shirikishi kwa wadau wote wa kujenga uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla hatua ya kupitishwa kwa Muswada huu, ambao kwa kiwango kikubwa na kwa kadri ya maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni Muswada ambao kwa kiwango kikubwa na kama ilivyo kwa miaka yote na Serikali zote ambazo zimetangulia umeshindwa kuainisha vyanzo vipya vya mapato nje ya utaratibu wa kawaida wa kurekebisha viwango vya kodi, tozo na ada mbalimbali, ni Muswada ambao unaainisha vyanzo vya mapato vya Serikali kwa taifa ambalo limepata uhuru kwa zaidi ya miaka hamsini kuwa ni pamoja na nywele bandia na taulo za kike, hii ni aibu kwa taifa kama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali hii ya CCM ikatambua na kukubaliana na sera za CHADEMA kuhusu uchumi zinazofuata uchumi wa soko la jamii, sera za kuanzisha mamlaka imara za kusimamia na kuratibu sekta binafsi, ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye uchumi na kujenga

mustakabali wa mwelekeo wa uchumi. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani yamejikita kwenye imani ya uchumi wa soko jamii ambao ni mfumo wa uchumi unaozingatia maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga uchumi imara utakaowezesha Taifa kupata kodi zenye uhakika, CHADEMA na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tutajikita katika misingi mikuu ya uchumi wa soko huria iliyojikita katika ushirikishwaji na mshikamano, ambapo jamii ya Watanzania itasimama pamoja kwa wakati wote kushiriki katika masuala ya maendeleo kuanzia ngazi za chini mpaka Taifa. Aidha, msingi mwingine katika mfumo huu wa uchumi, ni kujenga na kuruhusu ushindani katika soko huria, kuruhusu watu na sekta binafsi kumiliki mali, mifuko ya hifadhi za jamii pamoja na kutoa huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyoko madarakani, Kambi Rasmi ya Upinzani itaweka mfumo wa kodi ambao utasaidia utajiri na keki ya Taifa kutumika kwa manufaa ya watu wote nchini, Kambi Rasmi tutahitaji ukuaji wa uchumi ambao unazingatia utunzaji endelevu wa mazingira. Pamoja na hayo CHADEMA na Kambi itashirikisha angalau 60% ya uchumi unaomilikiwa na Watanzania wenyewe. Ili kufikia lengo hilo la Serikali ya Upinzani ikiongozwa na CHADEMA itahakikisha kwamba kunakuwepo uwazi na uwajibikaji katika miradi mikubwa ya uchumi na uwazi katika mikataba na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kipato na mapato ya Serikali, tutahakikisha tunashirikisha sekta binafsi inayokua katika uchumi kwa kuanzisha mamlaka imara za kusimamia na kuratibu sekta binafsi. Kwa kufanya hivyo, tutachochea sekta za uzalishaji kwa kuanzisha bodi mbalimbali za biashara ambazo zitafanya kazi kwa ukaribu na mamlaka za Serikali za Mitaa katika majadiliano kuhusu masuala ya miongozo mbalimbali ya kibiashara kwa ajili ya ukuaji wa uchumi. Pamoja na hayo, tutaimarisha sekta ya fedha kwa ajili ya uwekezaji kwa sababu biashara zinachukua muda mrefu kufikia hatua ya kupata faida. Kutokana na hilo,

CHADEMA itaweka mipango ya kifedha kwa ajili ya miradi ya muda mfupi na wa kati na muda mrefu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi. Pia, tutahakikisha kwamba biashara mpya zinazoanzishwa zinapata muda maalumu na unafuu wa kodi kabla ya kuanza kupata faida pamoja na kuwa na mkakati wa kuwaendeleza wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huo, Watanzania watanufaika kwa kuona Serikali yao ikishirikiana na sekta binafsi, kukua kwa uwekezaji kutokana na ushirikishwaji katika maamuzi na kupungua kwa migogoro katika sehemu za kazi, kuongezeka kwa ufanisi na ushindani katika sehemu za kazi na kuwafanya wafanyakazi kuridhika na mazingira ya kufanyia kazi, kukua kwa uchumi kutakakochangiwa na ubia kati ya Serikali na sekta binafsi, kuwa na taasisi huru zinazosimamia utaratibu wa sheria kwa ajili ya kukua na kunawiri kwa sekta binafsi, kuwepo kwa mfumo wa ushirikishwaji wa nguvu kazi pamoja katika kukuza uchumi na kuwa na njia za kukuza biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa tungekuwa na Serikali, Serikali hiyo ingetarajiwa kupata mapato ya kikodi kwa kuwa na mikakati jumuiishi ya uchumi wa Taifa. Katika mkakati huu jumuiifu tunalenga kuimarisha uchumi kukabiliana na changamoto za ajira na bei ya bidhaa, kuwa na mfumo wa Kodi unaotabirika kuliko utaratibu uliopo sasa, kuhakikisha kwamba kuna uwiano kati ya mauzo ya nje ya nchi na kuagiza bidhaa nje ya nchi pamoja na kusimamia Deni la Taifa. Msimamo wetu ni kuwa na mfumo wa kodi ulio wazi utakaozingatia uwezo wa mlipa kodi au taasisi inayolipa kodi kama njia bora kwa nchi na utajumuisha kodi nyingine kama Kodi ya Ongezeko ya Thamani na Kodi ya Ardhi. Kwa kufanya hivyo, kodi zote zitalipwa kwa wakati unaofahamika na kwa misingi na kanuni zinazokubalika. Kodi hizo zitakusanywa kwa gharama nafuu na kwa mfumo uliogatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna yoyote ile hatuwezi kupata mapato ya kuendesha nchi bila kuwa na uchumi wa viwanda vyenye tija. Ili kufikia hapo tunapaswa kutekeleza mkakati wa mabadiliko makubwa katika sekta

ya viwanda, kufungamanisha uchumi wa ndani na viwanda, kuwa na viwanda vinavyotumia teknolojia rafiki kwa mazingira na kuwekeza kwenye uchumi unaotegemea ubora, ufanisi na urahisi wa kupata taarifa. Aidha, kwenye sekta ya fedha na mabenzi tutafanya mabadiliko katika soko la mitaji, kuwa na sera za fedha rafiki na sekta binafsi pamoja na kuanzisha maeneo maalumu yasiyokuwa na kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kutoa utangulizi huo ili kuonesha ni kwa namna gani sera na sheria mbalimbali vinapaswa kujikita kupanua wigo wa kulipa kodi. Tuko hapa tulipo kwa sababu ya sera na wigo uliopo wa kukusanya mapato. Aidha, nimeweka utangulizi huo kwa kifupi ili kuonesha namna ambavyo sera mbadala zitalipelekea Taifa hili kupata mapato mengi na njia ya kufikia hapo ni kufanya mabadiliko makubwa na kupanua vyanzo vya mapato kuliko kuwa na bajeti inayotegemea vyanzo vya sasa ambavyo haviaminiki na kutabirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya vifungu mbalimbali Katika Muswada ulio mbele yetu, marekebisho ya Sheria ya Viwango, Sura ya 130. Sehemu ya Saba ya Muswada inafanyia marekebisho Sheria ya Viwango, Sura ya 130, kwa lengo la kuainisha masharti yanayohusu ukaguzi, usajili wa vyakula na majengo yanayohusika na vipodozi, majengo ya kuchinjia wanyama na uuzaji wa nyama, usajili, usalama wa chakula, zuio la uzalishaji na uzalishaji wa bidhaa ya vipodozi na adhabu dhidi ya uzalishaji, uagizaji kutoka nje, uuzaji au usambazaji wa vipodozi kinyume na masharti ya sheria kwa lengo la kudhibiti usalama na ubora wa vyakula na vipodozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli marekebisho yanayofanyika yanatasaidia wafanyabiashara kupunguza mlolongo wa uombaji wa leseni kutoka katika mamlaka mbili tofauti kwani kulikuwa na muingiliano mkubwa wa kimajukumu lakini bado kuna bidhaa kama vipodozi ambavyo vimeidhinishwa kuwa chini ya usimamizi wa *TBS* badala ya kubakia kuwa chini ya *TFDA*. Kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Muswada kinachofanyia marekebisho

kifungu cha 2 cha sheria mama kwenye tafsiri ya maneno, kimetoa tafsiri ya neno “*cosmetic*” kwamba ni, “*any article intended to be used by means of rubbing, pouring, steaming, sprinkling, spraying on or otherwise applied to the human body or any part there of for cleansing, beautifying, promoting attractiveness or altering the appearance and includes any article intended for use as a component of a cosmetic, but excludes articles intended for use in the diagnosis, treatment or prevention of disease and those intended to affect the structure or any function of the body*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyakula vyote vimehamishwa kutoka *TBS* kwenda *TFDA* lakini kwa tafsiri ya hapo juu *cosmetics* ni dawa, hivyo haipaswi kuwa chini ya Sheria ya Viwango na badala yake ilipaswa kuwa chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Kifungu cha 6 cha Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019, kinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, kwa kuingiza kifungu kipya cha 135A baada ya kifungu cha 135. Kifungu hiki kipya kinatoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa vilainishi vya ndege ambavyo vimetengenezwa mahsusi kutumika katika ndege vinavyoingizwa na mashirika ya ndege yanayotambulika katika mikataba ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali za nje.

Kwa mujibu wa Serikali, hatua hiyo inadaiwa kwamba itaiwezesha Tanzania kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo na hivyo kuimarisha usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7 cha Muswada huo kinapendekeza kufanya marekebisho katika Jedwali la Nne kwa kuingiza *HS Code* mpya baada ya *HS Code* 2009.11.00 kwa kutoza ushuru wa bidhaa za nywele za bandia zinazotengenezwa nchini na 25% kwa nywele bandia zinazotoka nje ya nchi kwa lengo la kukuza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la ajabu kwamba Bajeti ya Serikali sasa inategemea nywele bandia, kwa mantiki ya kawaida ikitokea wanawake wote wakaamua kunyoa nywele zao na wasivae tena nywele bandia mapato haya hayapatikana. Hata hivyo, kwa upande mwingine Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaliona jambo hili kama siyo sawa kwa sababu ni mapato yanayotarajiwa kupatikana kutoka kwa mama zetu kwa sababu tu wao ni wanawake na watumiaji wakubwa wa nywele bandia. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kwamba kifungu hiki kifutwe na Serikali itafute vyanzo vingine vya mapato vinavyotokana na rasilimali za Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 7 cha Muswada kinachopendekeza kufanyia marekebisho katika Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kinapendekeza marekebisho ya jedwali kwa kutoza ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake vinavyotoka nje ya nchi kwa 10% zinazofahamika kwa *HS Code* 39.17 eti kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubaliani na kifungu hiki kwa sababu kubwa tatu; sababu ya kwanza kifungu kinachopendekezwa kufanyiwa mabadiliko katika muswada hakisemi kama mapendekezo ya kutoza ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa ni kwa mabomba yanayotoka nje ya nchi au kama ni pamoja na mabomba yanayozalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa ufafanuzi huo, tafsiri yake ni kwamba ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake utatozwa kwa mabomba yanayozalishwa hapa nchini na mabomba yanayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa kuwa mabomba yote yanatambulika kwa *HS Code* 39.17.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya kifungu hicho yatakuwa ni kufanya mabomba yanayozalishwa hapa nchini kuwa ya gharama kubwa na hivyo kushindwa kuleta ushindani katika soko, lakini pia ushuru huu utapunguza

uzalishwaji wa mabomba ya ndani ya nchi na hivyo kupelekea upungufu wa ajira kwenye viwanda vinavyozalisha mabomba ya plastiki ndani ya nchi na pia hivyo Serikali itakosa mapato kutokana na uzalishaji kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili, ni kwamba hakuna mkakati wowote utakaowawezesha wananchi wa kawaida kutambua utofauti kati ya mabomba yanayozalishwa nchini na yale yanayozalishwa nje ya nchi, matokeo yake wananchi watauziwa kwa bei ile ile. Sababu kama hii imetolewa na Serikali hii kupitia kwa Waziri wa Fedha na Mipango wakati akitoa sababu za kufutwa kwa msamaha wa kodi kwenye taulo za kike, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa kwa nini sasa Serikali inakuja na jambo lile lile ambalo limewashinda kutekelezeka kwenye taulo za kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya tatu ni kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua matatizo ya Watanzania wanayopata ya ukosefu wa maji, kuwaongezea kodi kwenye mabomba ambayo yangewasaidia kupata maji safi na salama ni sawa na tishio dhidi ya uhai wao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hatuungi mkono kodi zinazotowza kwenye vifaa vya ujenzi ili kuwawezesha Watanzania kumudu gharama za vifaa hivyo na kuwapunguzia magonjwa ya mlipuko inayotokana na ukosefu wa maji safi na salama kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Serikali inapendekeza pia katika jedwali hili kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo, hali kadhalika Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake, usitowze kodi. Endapo Serikali haitataka kuondoa ushuru huo kwenye mabomba ya plastiki, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Serikali itoze kiwango cha VAT kwa 0% kwa mabomba yanayozalishwa ndani ya nchi ambayo yanajulikana kwa HS Code 39.17 kwa lengo lile lile la kulinda viwanda vya ndani, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali. Pia Serikali iweke utaratibu wa namna ya kudhibiti mabomba yanayozalishwa

ndani kutouzwa kwa bei kubwa sawa na mabomba yanayoingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; Kifungu cha 9 cha Muswada wa Sheria ya Fedha ya 2019, kilikusudia kufanya marekebisho kwenye jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato kwa kuingiza kipengele kipya baada ya kipengele cha (c) cha aya ya 3(2) cha (d) ambacho kimeweka masharti ya mwekezaji wa taulo za kike na kuwa na mkataba wa makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapunguziwa kodi ya kampuni (*corporate tax*) kwa kiwango cha 25% kwa miaka miwili mfululizo kuanzia tarehe 1 Julai, 2019 hadi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubaliani na kitendo cha Serikali kufuta msamaha wa kodi kwenye taulo za kike. Dhamira ya Serikali kufuta kodi kwenye taulo za kike iliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Waziri wa Fedha na Mipango katika hotuba yake pale aliposema “Serikali inapendekeza Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike (*HS Code 9619.00.10*) kwa kuwa haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara. Aidha, wakati Serikali ilipoweka msamaha huu ilitarajia kwamba wazalishaji wa taulo za kike wataziua kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ukiangalia Muswada kwa umakini katika mapendekezo yanayohusu Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 hakuna sehemu inayosema na au kutekeleza takwa hilo la kisheria. Matokeo yake sasa Serikali imepitia katika Sheria ya Mapato kwa kuongeza kodi kwa wawekezaji wanaotengeneza taulo za kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele hicho kipya cha (c) na (d) cha aya ya 3(2) kupitia kifungu cha 9 cha Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019, kimetokana na kile

ambacho Serikali imekisema aya ya 40(viii) ya hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kwamba wakati Serikali ilipoweka msamaha huu ilitarajia kwamba wazalishaji wa taulo za kike wataziuza kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi na kwamba msamaha wa kodi uliwanufaisha wafanyabiashara badala ya watumiaji wa taulo za kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wa taulo za kike ni mama zetu, wake zetu, dada zetu, watoto wetu ambao wanatumia taulo hizi kwa ajili ya kujihifadhi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiungi mkono kutumia hedhi kama chanzo cha mapato ya Serikali. Kifungu hiki kinapendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba kifutwe na Serikali itimize wajibu wake wa kuhakikisha wanufaika wa taulo za kike wananufaika wenyewe badala ya wafanyabiashara. Wajibu huo ni wajibu wa Serikali na kamwe haiwezekani kushindwa kutekelezwa kwa wajibu wa Serikali ikiwa ni kwa gharama za hedhi ya wanawake wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438; Sehemu ya Tisa ya Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 unahusu vifungu vya 38, 39 na 40. Kifungu cha 38 cha Muswada wa Fedha kinarekebisha kifungu cha 3(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 kwa kuingiza tafsiri ya maneno *fiscal device* na *fiscal receipts* katika sheria ili yatambuliwe, wakati kifungu cha 39 cha Muswada kinafanya mabadiliko ya kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) na (6). Kifungu cha 40 kinafanya marekebisho sehemu ya kwanza ya jedwali la kwanza la Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya vifungu hivyo ni kumwondolea mfanyabiashara anayeanza kufanya biashara masharti ya kuwasilisha taarifa ya makadirio ya kodi na kulipa kodi kwa awamu kulingana na kodi ya mapato kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo. Pamoja na mapendekezo haya, lakini Sheria ya Usimamizi wa Fedha pamoja na Muswada huu wa Fedha havijaainisha nini kitakachotokea endapo mfanyabiashara

atahindwa kuwasilisha taarifa ya makadirio ya kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuweka kifungu kinachofafanua hatua zitakazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; Kifungu cha 45 cha Muswada kinafanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kwa kufanya marekebisho ya sehemu ya pili ya jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, kipengele 40(vi) Serikali inasema na nanukuu:

“Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, karatasi zenye nembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya shirika husika la ndege, kwa kufanya marekebisho ya sehemu ya pili katika Jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuongeza kipengele kipyua kinachotoa msamaha pale vinapoingizwa nchini na mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inadhani Serikali inapaswa kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye tiketi za ndani za ndege ili kupunguza gharama ya tiketi za ndege kwa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha Watanzania kupanda ndege ambazo zimenunuliwa kwa kodi zao. Bila hivyo jitihada za Serikali za kununua ndege hazitakuwa na maana yoyote endapo Watanzania walio wengi hawamudu kupanda ndege kutokana na gharama kubwa. VAT kwenye tiketi za ndege zinapaswa kulenga kupunguza gharama ya kununua tiketi kwa safari za ndani ya nchi, kuliko mapendekezo ya sasa ya kuondoa kodi kwenye tiketi za ndege zinazoingizwa nchini yanayolenga kusaini tu misamaha ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; Muswada huu wa Sheria kwa kiasi kikubwa hauna jambo geni sana kutokana

na Serikali kushindwa kutambua vyanzo vipya vya mapato, badala yake Serikali kama ambavyo imekuwa ikifanya kwa miaka yote inapendekeza kufanya mabadiliko katika sheria mbalimbali kwa lengo la kuongeza mapato katika vyanzo visivyoaminika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaamini na inashauri Serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vya ujenzi, kuondoa kodi kwenye taulo za kike, kuondoa kodi kwenye nywele bandia pamoja na kuondoa kodi kwenye tiketi za ndege kwa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha Watanzania kupanda ndege zilizonunuliwa kwa kodi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaendelea kuishauri Serikali kuwekeza katika kujenga mazingira rafiki kwa wafanyabiashara nchini, kujenga mazingira rafiki kwa sekta binafsi na kutengeneza mazingira ambayo yatawawezesha wadau wa kodi kulipa kodi kwa mujibu wa sheria. Hatuwezi kutarajia maziwa mengi kwa ng'ombe usiyemlisha majani ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO, KUHUSU
MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2019 (THE
FINANCE ACT, 2019) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge-
Toleo la Januari 2016*

1. UTANGULIZI:

1. Mheshimiwa Spika, Nasimama mbele ya Bunge lako tukufu kwa mara nyingine tena ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa kutunga Sheria ya Fedha ya 2019 yaani **“the Bill to enact the Finance Act, 2019”** na kabla ya kutoa maoni haya, naomba kwanza kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kuendelea kutupatia uhai, busara na maarifa ya kuendelea kuishauri Serikali hata kama haiko tayari kupokea ushauri huo.

2. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba Muswada huu ambao kimsingi unakusudia kutekeleza malengo ya Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2019/2020 ni muswada ambao kiuhalisia hautaweza kusaidia kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika sekta ya viwanda ambayo inabeba kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda, ni muswada ambao unalenga kutekeleza Bajeti ambayo si rafiki kwa Sekta ya Kilimo ambayo inaajiri takribani asilimia 75 ya watazania wote na ukiachilia mbali mazingira yasiyo rafiki kwa biashara.

3. Mheshimiwa Spika, Kuboresha na kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara kunahitaji jitihada za makusudi zinazochochewa na sera madhubuti, rafiki na shirikishi kwa wadau wote wa kujenga uchumi wa Taifa.

4. Mheshimiwa Spika, Kabla hata ya kupitishwa kwa muswada huu, ambao kwa kiwango kikubwa na kwa kadri ya maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni muswada ambao kwa kiwango kikubwa na kama ilivyo kwa miaka yote na Serikali zote ambazo zimetangulia ni muswada ambao umeshindwa kuainisha vyanzo vipya vya mapato nje ya utaratibu wa kawaida wa kurekebisha viwango vya kodi, tozo na ada mbalimbali, ni muswada ambao unaainisha vyanzo vya mapato vya Serikali, kwa taifa ambalo limepata uhuru kwa miaka zaidi ya hamsini kuwa ni pamoja na nywele za Bandia pamoja na taulo za kike, hii ni aibu kwa taifa kama Tanzania.

5. Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali hii ya CCM ikatambua na kukubaliana na sera za CHADEMA kuhusu uchumi zinazofuata mfumo wa uchumi wa soko jamii, sera za kuanzisha mamlaka imara za kusimamia na kutaribu sekta binafsi, ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye uchumi, kujenga mustakabali wa mwelekeo wa uchumi. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani yamejikita kwenye imani ya uchumi wa soko jamii ambao ni mfumo wa uchumi unaozingatia maendeleo na ustawi wa jamii.

6. Mheshimiwa Spika, ili kujenga uchumi imara utakaowezesha taifa kupata kodi zenye uhakika, CHADEMA tutajikita katika misingi mikuu ya uchumi wa soko huria iliyojikita katika ushirikishwaji na mshikamano, ambapo jamii ya watanzania itasimama pamoja wakati wote kushiriki katika masuala ya maendeleo kuanzia ngazi za chini mpaka Taifa. Aidha msingi mwingine katika mfumo huu wa uchumi, ni kujenga na kuruhusu ushindani, soko huria, kuruhusu watu na sekta binafsi kumiliki mali, mifuko ya hifadhi za jamii pamoja na kutoa huduma za jamii.

7. Mheshimiwa Spika, Tofauti na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi iliyoko madarakani, CHADEMA itaweka mfumo wa kodi ambao utasaidia utajiri na keki ya Taifa kutumika kwa manufaa ya watu wote nchini, CHADEMA tutahitaji ukuaji wa uchumi ambao unazingatia utunzaji endelevu wa mazingira. Pamoja na hayo CHADEMA itahakikisha kwamba angalau 60% ya uchumi inamilikiwa na watanzania wenyewe na ili kufikia lengo hilo Serikali ya CHADEMA itahakikisha kwamba kunakuwepo uwazi na uwajibikaji katika miradi mikubwa ya uchumi na uwazi katika mikataba na uwekezaji.

8. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mapato ya Serikali, CHADEMA tutahakikisha tunashirikisha sekta binafsi inayokua katika uchumi kwa kuanzisha mamlaka imara za kusimamia na kuratibu sekta binafsi, kwa kufanya hivyo tutachochea sekta za uzalishaji kwa kuanzisha bodi mbalimbali za biashara ambazo zitafanya kazi kwa karibu na mamlaka za Serikali katika majadiliano kuhusu masuala ya miongozo mbalimblai ya kibiashara kwa ajili ya ukuaji wa uchumi.

Pamoja na hayo tutaimarisha sekta ya fedha kwa ajili ya uwekezaji kwa sababu biashara zinachukua muda mrefu kufikia hatua ya kupata faida. Kutokana na hilo, CHADEMA itaweka mipango ya kifedha kwa ajili ya miradi ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi pia tutahakikisha kwamba biashara mpya zinazoanzishwa zinapata muda maalumu wa unafuu wa kodi kabla ya kuanza kupata faida pamoja na kuwa na mkakati wa kuwaendeleza wajasiriamali.

9. Mheshimiwa Spika, kwa utaraibu huo watanzania watanufaika kwa kuona Serikali yao ikishirikiana na sekta binafsi, kukua kwa uwekezaji kutokana na ushirikishwaji katika maamuzi na kupungua kwa migogoro katika sehemu za kazi, kuongezeka kwa ufanisi na ushindani katika sehemu za kazi na kuwafanya wafanyakazi kuridhika na mazingira ya kufanyia kazi, kukua kwa uchumi kutakakochangiwa na ubia kati ya Serikali na sekta binafsi, kuwa na taasisi huru zinazosimamia utaratibu wa sheria kwa ajili ya kukua na kunawiri kwa sekta binafsi, kuwepo kwa mfumo wa ushirikishwaji wa nguvu kazi ya pamoja katika kukuza uchumi na kuwa na njia za kukuza biashara.

10. Mheshimiwa Spika, ikiwa CHADEMA tungekuwa na Serikali, Serikali hiyo ingetarajiwa kupata mapato ya kikodi kwa kuwa na mkakati jumuiishi wa uchumi wa Taifa, katika mkakati huu jumuiishi, CHADEMA tunalenga kuimarisha uchumi kukabiliana na changamoto za ajira na bei ya bidhaa, kuwa na mfumo wa Kodi unaotabirika kuliko utaratibu uliopo sasa, kuhakikisha kwamba kuna uwiano kati ya mauzo ya nje ya nchi na kuagiza bidhaa nje ya nchi pamoja na kusimamia Deni la Taifa. Msimamo wetu ni kuwa na mfumo wa kodi uliowazi utakaozingatia uwezo wa mlipa kodi au taasisi inayolipa kodi kama njia bora kwa nchi na utajumuisha kodi nyingine kama Kodi ya Ongezeko ya Thamani na Kodi ya Ardhi. Kwa kufanya hivyo kodi zote zitalipwa kwa wakati unaofahamika na kwa misingi na kanuni zinazokubalika. Kodi hizo zitakusanywa kwa gharama nafuu na kwa mfumo uliogatuliwa.

11. Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote ile hatutaweza kupata mapato ya kuendesha nchi bila kuwa na uchumi wa viwanda wenye tija, na ili kufikia hapo tutapaswa kutekeleza mkakati wa mabadiliko makubwa katika sekta ya viwanda, kufungamanisha uchumi wa ndani na viwanda, kuwa na viwanda vinavyotumia teknolojia rafiki kwa mazingira na kuwekeza kwenye uchumi unaotegemea ubora, ufanisi na urahisi wa kupata taarifa. Aidha kwenye sekta ya fedha na mabenki tutafanya mabadiliko katika soko la mitaji, kuwa na sera za kifedha rafiki kwa sekta binafsi pamoja na kuanzisha maeneo maalumu yasiyokuwa na kodi.

12. Mheshimiwa Spika, nimejaribu kutoa utangulizi huo ili kuonesha ni kwa namna gani sera na sheria mbalimbali vinapaswa kujikita kupanua wigo wa kulipa kodi. Tuko hapa tulipo kwa sababu ya sera na wigo uliopo wa kukusanya mapato. Aidha nimeweka utangulizi huo kwa kifupi ili kuonesha namna ambavyo sera mbadala zitalipelekea Taifa hili kupata mapato mengi, na njia ya kufikia hapo ni kufanya mabadiliko makubwa na kupanua vyanzo vya mapato kuliko kuwa na bajeti inayotegemea vyanzo vya sasa ambavyo haviaminiki na kutabirika.

2. MAPITIO YA VIFUNGU MBALIMBALI KATIKA MUSWADA ULIO MBELE YETU

A. MAREKEBISHO YA SHERIA YA VIWANGO SURA YA 130

13. Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya muswada inafanyia marekebisho Sheria ya Viwango, Sura ya 130, kwa lengo la kuainisha masharti yanayohusu ukaguzi, usajili wa vyakula na majengo yanayohusika na vipodozi, majengo ya kuchinjia wanyama na uuzaji wa nyama, usajili, usalama wa chakula, zuiu la uzalishaji na uuzaji wa bidhaa ya vipodozi na adhabu dhidi ya uzalishaji, uagizaji kutoka nje, uuzaji au usambazaji wa vipodozi kinyume na masharti ya sheria kwa lengo la kudhibiti usalama na ubora wa vyakula na vipodozi.

14. Mheshimiwa Spika, ni kweli marekebisho yanayofanyika yanatasaidia wafanyabiashara kupunguza mlolongo wa uombaji wa leseni kutoka katika mamlaka mbili tofauti kwani kulikuwa na muingiliano mkubwa wa kimajukumu, lakini bado kuna bidhaa kama vipodozi ambavyo vimeidhinishwa kuwa chini ya usimamizi wa TBS badala ya kubakia kuwa chini ya TFDA.

15. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 2 cha sheria mama kwenye tafsiri ya maneno, kimetoa tafsiri ya neno "cosmetic" kwamba; "any article intended to be used by means of rubbing, pouring, steaming, sprinkling, spraying on or otherwise applied to the human body or any part there

of for cleansing, beautifying, promoting attractiveness or altering the appearance and includes any article intended for use as a component of a cosmetic, but excludes articles intended for use in the diagnosis, treatment or prevention of diseases and those intended to affect the structure or any function of the body”

16. Mheshimiwa Spika, Kwa tasfiri hiyo hapo juu, vyakula vyote vimehamishwa kutoka TBS kwenda TFDA lakini kwa tafsiri ya hapo juu cosmetics ni dawa, hivyo haipaswi kuwa chini ya Sheria ya Viwango na badala yake ilipaswa kuwa chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

B. SHERIA YA USHURU WA BIDHAA (SURA YA 147)
(The Excise Management and Tariff Act, (CAP 147)

17. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 cha Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019, kinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147, kwa kuingiza kifungu kipya cha 135 A baada ya kifungu cha 135. Kifungu hiki kipya kinatoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa vilainishi vya ndege ambavyo vimetengenezwa mahsusi kutumika katika ndege vinavyoingizwa na Mashirika ya Ndege yanayotambulika katika mikataba ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali za nje. Kwa mujibu wa Serikali hatua hiyo inadaiwa kwamba itaiwezesha Tanzania kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo na hivyo kuimarisha usafiri wa anga nchini.

18. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Jedwali la Nne kwa kuingiza HS Code mpya baada ya HS Code 2009.11.00 kwa kutoza ushuru wa bidhaa za nywele za bandia zinazotengenezwa nchini na 25% kwa nywele bandia zinazotoka nje ya nchi kwa lengo la kukuza mapato ya Serikali.

19. Mheshimiwa Spika, Ni jambo la ajabu kwamba Bajeti ya Serikali sasa inategemea nywele bandia, kwa mantiki ya kawaida ikitokea wanawake wote wakaamua kunyoa nywele zao na wasivae tena nywele bandia mapato haya

hayapatikana. Lakini kwa upande mwingine Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunalionga jambo hili kama siyo sawa kwa sababu ni mapato yanayotarajiwa kupatikana kutoka kwa mama zetu kwa sababu tu wao ni wanawake na watumiaji wakubwa wa nywele bandia, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kwamba kifungu hiki kifutwe na Serikali itafute vyanzo vingine vya mapato vinavyotokana na rasilimali za Taifa hili.

20. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 cha muswada kinachopendekeza kufanyika marekebisho katika Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kinapendekeza marekebisho ya jedwali kwa kutoza ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake zinazotoka nje ya nchi kwa 10% zinazofahamika kwa HS Code 39.17 eti kwa lengo la kulinda viwanda.

21. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubalini na kifungu hiki kwa sababu kubwa tatu, Mosi kifungu kinachopendekezwa kufanyiwa mabadiliko katika muswada hakisemi kama mapendekezo ya kutoza ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa ni kwa mabomba yanayotoka nje ya nchi au kama ni pamoja na mabomba yanayozalishwa ndani ya nchi.

22. Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa ufafanuzi huo, tafsiri yake ni kwamba ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake utatozwa kwa mabomba yanayozalishwa hapa nchini na mabomba yanayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa kuwa mabomba yote yanatambulika kwa HS Code 39.17

23. Mheshimiwa Spika, madhara ya kifungu hicho yatakuwa ni kufanya mabomba yanayozalishwa hapa nchini kuwa ya gharama kubwa na hivyo kushindwa kuleta ushindani katika soko, lakini pia ushuru huu utapunguza uzalishwaji wa mabomba ya ndani ya nchi, na hivyo kupelekea upungufu wa ajira kwenye viwanda vinavyozalisha mabomba ya plastiki ndani ya nchi na pia hivyo Serikali itakosa mapato kutokana na uzalishaji kidogo.

24. Mheshimiwa Spika, sababu ya Pili, ni kwamba hakuna mkakati wowote utakaowawezesha wananchi wa kawaida kutambua utofauti kati ya mabomba yanayozalishwa nchini na yale yanayozalishwa nje, matokeo yake wananchi watauziwa kwa bei ile ile. Sababu kama hii imetolewa na Serikali hii kupitia kwa Waziri wa Fedha na Mipango wakati akitoa sababu za kufutwa kwa msamaha wa kodi kwenye taulo za kike, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa kwa nini sasa Serikali inakuja na jambo lile lile ambalo limewashinda kutekelezeka kwenye taulo za kike.

25. Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu ni kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua matatizo ya watanzania wanayopata ya ukosefu wa maji, kuwaongezea kodi kwenye mabomba ambayo yangewasaidia kupata maji safi na salama ni sawa na tishio dhidi ya uhai wao, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hatuungi mkono kodi zinazotowa kwenye vifaa vya ujenzi ili kuwawezesha watanzania kumudu gharama za vifaa hivyo na kuwapunguzia magonjwa ya mlipuko inayotokana na ukosefu wa maji safi na salama kwenye maeneo yao.

26. Mheshimiwa Spika, Kama ambavyo Serikali inapendekeza pia katika jedwali hili kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo, hali kadhalika Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba ushuru wa bidhaa za mabomba ya plastiki na vifaa vyake, usitowe kodi. Na endapo Serikali haitataka kuondoa ushuru huo kwenye mabomba ya plastiki, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Serikali itoze kiwango cha VAT kwa 0% kwa mabomba yanayozalishwa ndani ya nchi ambayo yanajulikana kwa HS Code 39.17 kwa lengo lile lile la kulinda viwanda vya ndani, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali, lakini pia Serikali ikiweka utaratibu wa namna ya kudhibiti mabomba yanayozalishwa ndani kutouzwa kwa bei kubwa sawa na mabomba yanayoingizwa kutoka nje ya nchi.

C. SHERIA YA KODI YA MAPATO (SURA YA 332)

27. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 cha Muswada wa Sheria ya Fedha ya 2019, kilikusunafanya marekebisho kwenye

jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato kwa kuingiza kipengele kipya baada ya kipengele cha (c) cha aya ya 3(2) cha (d) ambacho kimeweka masharti ya mwekezaji wa **taulo za kike** na kuwa na mkataba wa makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapunguziwa kodi ya kampuni (corporate tax) kwa kiwango cha 25% kwa miaka miwili mfululizo kuanzia tarehe 1 Julai, 2019 hadi Juni, 2021.

28. Mheshimiwa Spika, kwanza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubaliani na kitendio cha Serikali kufuta msamaha wa kodi kwenye taulo za kike. Dhamira ya Serikali kufuta kodi kwenye taulo za kike iliwasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu na Waziri wa Fedha na Mipango katika hotuba yake pale aliposema “Serikali inapendekeza Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike (HS Code 9619.00.10) kwa kuwa haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara. Aidha, wakati Serikali ilipoweka msamaha huu ilitarajia kwamba wazalishaji wa taulo za kike wataziua kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi”

29. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukiangalia muswada kwa umakini katika mapendekezo yanayohusu Sheria ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 hakuna sehemu inayosema na au kutekeleza takwa hilo la Serikali. Matokeo yake sasa Serikali imepitia katika Sheria ya Mapato kwa kuongeza kodi kwa wawekezaji wanaotengeneza taulo za kike.

30. Mheshimiwa Spika, kipengele hicho kipya cha (c) na (d) cha aya ya 3(2) kupitia kifungu cha 9 cha muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019, kimetokana na kile ambacho Serikali imekisema aya ya 40(viii) ya hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kwamba **“wakati Serikali ilipoweka msamaha huu ilitarajia kwamba wazalishaji wa taulo za kike wataziua kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi”** na kwamba msamaha wa kodi uliwanufaisha wafanya biashara badala ya watumiaji wa taulo za kike.

31. Mheshimiwa Spika, watumiaji wa taulo za kike ni mama zetu, wake zetu, dada zetu, watoto wetu ambao wanatumia taulo hizi kwa ajili ya kujihifadhi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiungi mkono kutumia hedhi kama chanzo cha Mapato ya Serikali, kifungu hiki kinapendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba kifutwe na Serikali itimize wajibu wake wa kuhakikisha wanufaika wa taulo za kike wananufaika wenyewe badala ya wafanyabiashara, wajibu huo ni wajibu wa Serikali na kamwe haiwezekani kushindwa kutekelezwa kwa wajibu wa Serikali ikiwa ni kwa gharama za hedhi ya wanawake wa Tanzania.

D. SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI (SURA YA 438)

32. Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa ya muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 unahusu vifungu vya 38, 39 na 40. Kifungu cha 38 cha Muswada wa Fedha kinarekebisha kifungu cha 3(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Sura ya 438) kwa kuingiza tafsiri ya maneno fiscal device na fiscal receipt katika sheria ili yatambuliwe, wakati kifungu cha 39 cha muswada kinafanya mabadiliko ya kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) na (6). Kifungu cha 40 kinafanya marekebisho sehemu ya kwanza ya jedwali la kwanza la Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

33. Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya vifungu hivyo ni kumuondolea mfanyabiashara anayeanza kufanya biashara masharti ya kuwasilisha taarifa ya makadirio ya kodi na kulipa kodi kwa awamu kulingana na kodi ya mapato kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo, pamoja na mapendekezo haya, lakini Sheria ya Usimamizi wa Fedha pamoja na muswada huu wa fedha havijaaainisha nini kitakachotokea endapo mfanyabiashara atashindwa kuwasilisha taarifa ya makadirio ya kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuweka kifungu kinachofafanua hatua zitakazochukuliwa.

**E. SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI
(SURA YA 148)**

34. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 45 cha muswada kinafanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kwa kufanya marekebisho ya sehemu ya pili ya jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kipengele 40(vi) Serikali inasema na ninanukuu; ***"kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, Karatasi zenye nembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya shirika husika la ndege, kwa kufanya marekebisho ya sehemu ya pili katika Jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuongeza kipengele kipya kinachotoa msamaha pale vinapoingizwa nchini na mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo"***;

35. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inadhani Serikali inapaswa kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa tiketi za ndani ili **kupunguza gharama ya tiketi za ndege kwa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha watazania kupanda ndege ambazo zimenunuliwa kwa kodi zao**. Bila hivyo jitihada za Serikali za kununua ndege hazitakuwa na maana yoyote endapo watazania walio wengi hawamudu kupanda ndege kutokana na gharama kubwa. VAT kwenye tiketi za ndege zinapaswa kulenga kupunguza gharama ya kununua tiketi kwa safari za ndani ya nchi, kuliko mapendekezo ya sasa ya kuondoa kodi kwenye tiketi za ndege zinazolingizwa nchini yanayolenga kusaini tu misamaha ya kimataifa.

3. HITIMISHO

36. Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa sheria kwa kiasi kikubwa hauna jambo geni sana kutokana na Serikali

kushindwa kutambua vyanzo vipya vya mapato, badala yake Serikali kama ambavyo imekuwa ikifanya kwa miaka yote inapendekeza kufanya mabadiliko katika sheria mbalimbali kwa lengo la kuongeza mapato katika vyanzo visivyoaminika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaamini na inashauri Serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vya ujenzi, kuondoa kodi kwenye taulo za kike, kuondoa kodi kweye nywele bandia pamoja na kuondoa kodi kwenye tiketi za ndege kwa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha watazania kupanda ndege zilizounuliwa kwa kodi zao.

37. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaendelea kuishauri Serikali kuwekeza katika kujenga mazingira rafiki kwa wafanyabiashara nchini, kujenga mazingira rafiki kwa sekta binafsi na kutengeneza mazingira ambayo yatawawezesha wadau wa kodi kulipa kodi kwa mujibu wa sheria. Hatuwezi kutarajia maziwa mengi kwa ng'ombe usiyemlisha majani ya kutosha.

38. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

David Ernest Silinde (Mb)

**Kny: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

26 Juni, 2019

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumeshamsikia Waziri wa Fedha na Mipango, lakini pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na pia upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani na kwa utaratibu wetu tutaanza uchangiaji. Ninayo majina hapa ya kutoka vyama vyote vyenye uwakilishi hapa Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Mbene na Mheshimiwa Jaffary Michael ajiandae.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru sana Waziri kwa uwasilishaji wa hii Sheria ya Fedha, lakini pia niunge mkono mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na ushauri au maombi hasa kwenye hii taarifa ya Waziri wa Fedha, pale kwenye ukurasa wa (v) inayosema kwamba kuandaa kanuni za kuwawezesha, kuwatambua na kuwatoza ada ya mwaka ya vitambulisho wafanyabiashara hawa wadogowadogo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, suala hili limekuwa kidogo na matatizo mengi huko vijijini na hata mijini kwa sababu sasa umepewa meno ya kwenda kuandaa kanuni basi iwapendeze kanuni hizo ziandaliwe mapema ili iweze kujulikana kwamba nani hasa muhusika na vitambulisho hivi au nani anastahili kupata vitambulisho hivyo.

La pili, nitaomba tu Mheshimiwa Waziri anisaidie pale ukurasa wa 7(iii) inayozungumzia pesa za miradi ambapo wamempa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuongeza muda wa matumizi ya fedha ya mwaka wa fedha hususan upande wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo ambalo huwa linatukumba mara kwa mara hasa mwaka wa fedha unapokaribia kwisha. Mfano, mwezi huu ni Juni, lakini pesa zinaweza zikatumba leo, ikafika Agosti. Sasa tungependa kujua huo muda ambao huyu Mlipaji Mkuu wanasema anapewa muda, muda gani? Wanaweza wakasema ni muda gani ambao anatakiwa apewe, hii angalau itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu ushauri, tumepitisha bajeti yetu jana ya trilioni 33. Nawasihi sana wenzangu sina tatizo kwanza na Sheria ya Fedha sababu imeandaliwa vizuri na wataalam. Niombe kwao, *TRA* ni kama moyo wa binadamu, moyo wa binadamu usipofanya kazi vizuri, baadhi ya eneo au mwili mzima unaweza uka-*paralyze*, tunawategemea sana, lakini *BOT* tunawategemea sana, hatuwezi kupata hizi trilioni 33 endapo wafanyakazi wa *TRA* siyo wazalendo na siyo waaminifu. Ili tufikie huko kwenye trilioni 33 lazima mioyo yenu iwe ya uzalendo hasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa naona wafanyakazi wa *BOT* wao wanavaa mashati meupe, shati jeupe likiwa na

doa hutalivaa tena kwa sababu limeshachafuka. Niwaombe wafanyakazi wa *TRA* na *BOTH* hasa *TRA* vaeni mashati meupe wawe wasafi na usafi huo uonekane ndani ya mioyo yao, siyo juu juu tu, usafi uonekane ndani ya mioyo yao. Wanayo dhamana kubwa ndiyo maana nimesema *TRA* ni kama moyo kwa mwili wa binadamu, damu isiposambaa vizuri, wasipokusanya vizuri pesa, ina maana nchi yetu haya yote tulyopitisha itakuwa ni kazi bure, nawaomba sana *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe *TRA*, Mheshimiwa Waziri, pesa nyingi/makusanyo mengi iwe ni wilayani na mikoani pesa nyingi zinapotea kwa sababu ya baadhi ya wafanyakazi wetu wa *TRA*, siyo wote. Hata kwenye kikao cha wafanyabiashara na Mheshimiwa Rais sote tulisikia na tuliona malalamiko mengi yalikuwa ni *TRA*. Sasa tukijiuliza kwa nini tunashindwa kufikia malengo, lakini tukijiuliza kwa nini eneo lingine linavuka malengo, lazima tujjulize, lakini inawezekana tatizo ni wafanyakazi wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nasisitiza, bila *TRA* kusimamia vizuri makusanyo na mapato ya Serikali, hizi shilingi trilioni 33 ambazo tutazifanyia kazi kwenye shughuli za maendeleo, *recurrent* na *OC*, bila kuzisimamia vizuri tusishangae tutakapokuja mwakani tukiulizana makusanyo yamefikia asilimia ngapi; 45%, 60%, 70%, lakini nafikiri tunao uwezo, *TRA* wakiamua vizuri tunaweza tukakusanya zaidi. Kwa hiyo, niwaombe sana watu wa *TRA*, kuweni wazalendo ili pesa hizi shilingi trilioni 33 zipatikane na nchi yetu iweze kuneemeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia 100. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Mbene, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael na Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja hii lakini nina mambo machache ambayo napenda kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napongeza sana hatua zote muhimu zilizochukuliwa za kupunguza tozo au kuongeza ushuru sehemu zile ambazo zinalenga kulinda viwanda vyetu vya ndani. Napenda tu kutoa angalizo katika suala zima la kulinda viwanda vya ndani; bado kuna vikwazo ambavyo inabidi navyo viondolewe katika viwanda hivi vya ndani ili kuhakikisha kuwa tozo ile iliyoongezwa kwenye bidhaa zinazoagizwa kutoka nje inatimiza lengo lake maana siyo *automatic* kuwa kwa sababu umepunguza tozo au umeongeza tozo ya bidhaa inayoagizwa basi kiwanda cha ndani kitakua. La hasha kinatakiwa kifanyiwe kazi na kama tunavyojua kuwa suala la kodi ni sehemu ndogo tu ya uwezeshwaji unaotegemewa kwenye viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali imeonesha wazi imeshaanza kuifanyia kazi *blueprint* lakini hii sehemu ambayo tunaiona sasa hivi ni ndogo sana ya *blueprint* nzima ambayo imechapishwa au imetengenezwa. Tunategemea kwa haraka sana *blueprint* yote itaanza kutekelezwa na Serikali. Hii ndiyo njia peke yake itakayoweza sasa uchumi huu kuchangamka na kukua kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi bado roho yangu iko sana kwenye kilimo na naamini katika kilimo kwa kuwa Tanzania tuna ardhi nzuri sana inayofaa kwa kilimo lakini haitumiki vizuri. Najua sababu kubwa ni utaratibu mzima uliowekwa wa jinsi ya kuitumia hiyo ardhi kwa wawekezaji wanaohitaji kuwekeza kilimo cha kibiashara, kilimo kikubwa na cha kati. Siyo lazima nizungumzie watu wa nje tu, hata Watanzania walioko ndani bado kuwekeza katika kilimo inawashinda kutokana na vikwazo mbalimbali. Napenda sana navyo ningeviona katika Muswada huu ili tuone jinsi gani ambavyo kilimo kinaenda sasa kukuzwa kama vile ambavyo ndiyo lengo kubwa la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kinaajiri watu wengi sana na kinachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye mfumuko wa bei mdogo. Kilimo siyo sekta ambayo unaweza ukaipuuzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali sana kwa kuondoa *import duty* kwenye vifungashio vya mbegu lakini *VAT* bado haijaondolewa. Kwa hiyo, bado tunarudi palepale katika kuifanya mbegu ya Tanzania kuwa ghali kuliko mbegu inayotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuko nyuma sana katika masuala ya biashara na hii inatokana na urasimu na mtazamo ulioko Serikalini, hasa kwa watendaji wetu au tuseme *bureaucrats*. Wengi wa watendaji wetu hawa hawajui biashara, hawajawahi kufanya biashara na hawana biashara na kwa hali hiyo wao mtazamo wao kwa *private sector* ni hasi. Napenda sana nione sasa hivi tunapata watendaji Serikalini ambao wametoka kwenye *private sector* au kwenye sekta binafsi, naamini watabadilisha ule mtazamo mzima wa jinsi gani biashara ifanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu, tulipompata Mtendaji Mkuu wa *National Housing*, hata yule aliyekuwa *TIC*, walibadilisha kwa kiasi kikubwa sana jinsi ambavyo zile taasisi zao zimefanya kazi. Kwa hali hiyohiyo, ukimleta mtu ambaye ana uzoefu wa kufanya biashara atabadilisha kabisa jinsi ambavyo biashara zinafanyika. Kwa hiyo, tusione vibaya kuajiri Serikalini watu ambao wametoka kwenye sekta binafsi au kuweka kwenye *boards* watu ambao wametoka kwenye sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la maji. Bahati mbaya sana bado tunatoza kodi *solar pumps* au pampu zinazotumia nguvu ya jua na mitambo ya kuchimba visima au mabwawa. Sasa hii moja kwa moja inarudisha nyuma suala zima la upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya wanadamu lakini kwa wanyama na kwa kumwagilia na kufugia samaki. Napenda sana kuona jinsi gani ambavyo kodi inapunguzwa au inaondolewa katika pampu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya Tanzania peke yetu katika Afrika Mashariki ndiyo tunatoza kodi kwenye hizi pampu za sola; Kenya, Uganda, Rwanda

hawafanyi hivi. Hii sasa inafanya sisi uwekezaji wetu katika suala zima la upatikanaji wa maji linakuwa dogo vilevile hata katika umwagiliaji na ufugaji wa samaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la kuondoa ushuru katika majokofu au *cold storage* lakini hii imewekwa kwa ajili ya mbogamboga tu na tunafahamu kuwa *cold storage* inatumika hata kwa samaki, nyama na maziwa. Hii ingekuwa ni njia nzuri sana ya kuwawezesha hata akina mama vijijini wanaofuga ng'ombe wao kuwa na uwezo wa kuweka maziwa yao katika hali ambayo hayaharibiki na kuyafikisha sokoni. Kwa hiyo, mimi napenda kuona kuwa inapanuliwa badala ya kuwa kwenye *horticulture* peke yake basi iende mpaka kwenye mazao mengine ya ufugaji, hiyo ingesaidia vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la taulo za kike. Nimekubali maelezo yaliyotolewa na Serikali kuhusiana na suala hili vilevile napenda sana kutoa angalizo kuwa zile bidhaa ambazo zinatoka nje zinazolingia katika viwanda hivi ni lazima nazo zitolewe ushuru au zipunguziwe kodi ili sasa hivi viwanda vya ndani viweze kuchukua hii fursa vizuri na kuifanyia kazi. Pia nataka kutoa angalizo au ushauri kwa Serikali, kwa kipindi cha mpito katika hii miaka miwili ambayo tunangojea viwanda vichangamkie fursa hii, Serikali ihakikishe kuwa inawezesha upatikanaji wa hizi taulo za kike kwa bei nafuu kwa maana ya kuweka bei elekezi vilevile labda kutumia *MSD* kama msambazaji mkuu wa taulo hizi za kike ili ziweze kuwafikia watu wote wanaolengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la kuwatambua wafanyabiashara au wawekezaji wa kwenye sekta isiyokuwa rasmi. Hapa naona kama kuna kukinzana, kwa upande mmoja tumepunguza kodi ya mapato kwa wale wa sekta isiyokuwa rasmi kutoka Sh.150,000 kwenda Sh.100,000, tunaipongeza sana Serikali kwa hili lakini wakati huohuo tunazungumzia kuiwezesha sekta isiyokuwa rasmi peke yake, sekta rasmi hawajapunguziwa kodi kama hizo, matokeo yake ni kuwa watu wengi watapendelea kuendelea kukaa kwenye sekta isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunajikuta tunakuwa kama tunakinzana; huku tunataka kuirasimisha sekta isiyokuwa rasmi lakini huku tunaikandamiza sekta iliyokuwa rasmi. Kwa hiyo napenda sana kuona jinsi ambavyo tuna-*balance* hivi vitu ili sekta isiyokuwa rasmi iingie kwenye mfumo rasmi lakini wale ambao tayari wako katika sekta rasmi waendeleo kunufaika na kukua na kuleta ufanisi mkubwa zaidi katika uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhary Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Omary Kigua ajiandae.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi maoni yangu ni kwamba pamoja na Muswada huu wa Sheria ya Mapato ya Kodi lakini ni vizuri mtazamo wa Serikali uwe kuwapunguzia mzigo mkubwa wanaoubeba watu wachache katika nchi hii kuwatumikia watu zaidi ya milioni 55 katika nchi hii. Wafanyabiashara wanaolipa kodi katika nchi hii kwa mujibu wa taarifa ambazo nafikiri zina uhakika kidogo, hawazidi milioni mbili na laki saba, lakini Watanzania wako milioni 55.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba kuna sehemu kubwa ya watu ambao hatujaweza kuwaingiza katika mfumo wa kulipa kodi. Kwa hiyo, mzigo huu umebebwa na watu wachache sana ambao sehemu yao ni wafanyakazi, wafanyabiashara ambao wako *formal* na wafanyabiashara wakubwa ambao ndiyo zaidi wamebeba jukumu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa Serikali umekuwa mara kwa mara kuwaangalia hawa watu ambao tayari wapo. Kwa hiyo, katika nchi hii inakuwa kama ni adhabu kujiingiza kwenye mfumo halali wa kulipa kodi, yaani mtu akishakuwa-*registered* kwenye mfumo halali wa kulipa

kodi, mamlaka za TRA zinamuangalia yeye tu usiku na mchana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba ni vizuri tutazame kwa picha pana, namna gani tunakuwa na kundi kubwa zaidi la watu watakaolipa kodi ili mzigo huu usibaki kwa watu wachache. Hasara zake ni kwamba hawa watu wachache ambao kila saa tunawaangalia wanafilisika, wanatoka kwenye biashara, hawa ambao tunataka tuwahudumie sasa mwishowe watakosa mtu wa kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Kambi ya Upinzani inasema tunatumia ng'ombe ambaye hatujajiandaa jinsi ya kumlisha, tunakamua maziwa ya ng'ombe ambaye hatujajiandaa jinsi ya kumhudumia. Ni vizuri tuone jinsi tunavyoifanya kodi iwe ni *incentive*, iwahamasishe watu kufanya biashara kuliko kufanya kodi iwakatishe watu tamaa ya kufanya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani wanapotoa maoni kwamba tuangalie vyanzo vingine zaidi ya kodi peke yake vya kutusaidia kupata mapato, hili jambo tulichukulie katika uzito wake sana. Najua inawezekana Serikali ina mawazo hayo lakini basi iyachukulie katika uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni mabadiliko yanayofanyika kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332. Kama nilivyosema, Serikali imepunguza kiwango cha kodi cha watu ambao hawafanyi mahesabu kutoka shilingi 150,000 mpaka shilingi 100,000, kiwango cha kuanzia, ni jambo jema kabisa lakini ni vizuri tukahikikishe tunawapata hawa watu. Maana ukisema mtu anayeza shilingi milioni 4 maana yake unasema mtu anayeza chini ya shilingi 15,000 kwa siku, katika nchi hii hawa watu wako wengi mno lakini bahati mbaya mamlaka zinazohusika hazijawafikia hawa watu na ndiyo maana nikasema mzigo unabaki kwa watu wachache sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maoni yangu siku zote yamekuwa kwamba hebu tuwaongeze nguvu wafanyakazi wa *TRA* wawe wengi ili wafikie hawa watu. Kwa sababu inawezekana tatizo la *TRA* pia ni idadi ya wafanyakazi. Mimi huwa nahesabu kwamba wafanyakazi wanaoajiriwa *TRA* ni kama uwekezaji kwa Serikali kwa sababu wale watu wanakwenda kukusanya mapato, kwa hiyo, wawe wa kutosha ili wawafikie hawa watu. Kwa sababu ukiweza kufikia hawa watu ambao wanapaswa kulipa Sh.100,000 wala hutakuwa na sababu ya kuhangaika na watu wa Sh.20,000 kwa sababu hawa watu ni wengi sana katika nchi yetu ambao mauzo yao ni zaidi ya shilingi milioni 4 lakini yasiyofika milioni 11, ni wengi sana, ni watu ambao mauzo yao ni kati ya Sh.15,000 kwa siku mpaka Sh.30,0000 kwa siku ambao ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mama lishe tu akipata wateja kumi kwa siku anafikia katika kiwango hicho. Sasa ni kwa nini tusipanue wigo mpaka tukafikia hawa watu kuliko kuacha wafanyabiashara wakubwa wachache kila siku waumie, wanatoka kwenye biashara halafu tunakosa kabisa mapato katika nchi hii. Mimi nakubaliana sana na Serikali kupunguza hiyo kodi kwenda kwenye Sh.100,000, ni jambo jema sana lakini ni vizuri waone sasa wanafikiaje hawa wafanyabiashara ambao wanapaswa kulipa kodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia pia kwenye upande wa kuondoa watu wanaofanya mahesabu kutoka kwenye milioni 20 mpaka milioni 100; ni jambo jema pia. Hata hivyo, upande huu naona kwamba Serikali haijaweka kiwango ambacho ni *fixed* kwa wale watu ambao hawajafanya mahesabu, maana yake ambao wamefanya mahesabu wanatakiwa walipe Sh.450,000 na 3.5% kwa mapato yanayozidi shilingi milioni 20, lakini hamjaweka kiwango *fixed* kwamba hawa watu ambao hawapigi mahesabu kwa sasa kama hana *records* lakini ana-*range* kwenye hiyo *range* ya *20 million to 100 million* alipe shilingi ngapi ili asisumbuliwe kwa sababu lengo ni kumtaka Mtanzania ajue nikienda *TRA* nalipa shilingi ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkimuacha Mtanzania aki-*bargain* sana na maafisa wa *TRA* mtatoa hiyo nafasi ya *corruption*. Ni vizuri mara nyingi tuwe na kodi ambazo zinasadikia, zinaelewaka, mtu akienda *TRA* anajua anatakiwa alipe kiasi gani. Labda kama siyo lazima sana kwa sababu kuna watu ambao wanafanya mahesabu ya fedha nyingi, hao tuwaache, lakini kwa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo ili tuwasaidie, tuwa-*promote*, wawe na viwango ambavyo akikaa nyumbani kwake anajua mimi kwa mwaka nataka ni ilipe kodi hii kama nimefanya bishara yangu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri kama tunakubaliana kwamba kiwango cha juu cha kutofanya mahesabu kwa kutumia mhasibu ni shilingi milioni 100 basi tuweke viwango *fixed* ambavyo huyu mtu anakwenda kulipa bila kusumbuliwa na mtu wa *TRA*. Akifika *TRA* anajua kwamba mimi kama mauzo yangu ni *range* ya milioni 20 mpaka 100 natakwa nilipe Sh.900,000, Sh.1,000,000, analipa anaachana na *TRA* hakuna masuala ya kusumbuana na masuala ya kutaka watu wapeane kitu kidogo kidogo, kwa hiyo, nafikiri hili ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la *TBS*. Ni jambo jema kwamba tumehamisha wajibu wa *TFDA* kuupeleka *TBS* lakini tukumbuke kwamba *TBS* bado wana *load* kubwa ya kazi zao. Ukiangalia siku za nyuma *TBS* kumekuwa kama kuna urasimu fulani wa kuhudumia watu, pamoja na majukumu yao yalivyokuwa machache, tunapowaongezea jukumu la kusajili vyakula na kadhalika kazi ambayo ilikuwa inafanywa na *TFDA*; tumejiandaa vipi kuwaongezea kiwango cha watumishi ili wahudumie watu wanaotaka kufanya uwekezaji kwa haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hawa watu wanataka uwekezaji, wanataka kuzalisha lakini inachukua muda sana kupitishwa na Mamlaka ya *TBS*. Kwa hiyo, ni vizuri hili suala tuliangalie ili isiwe tena ikaja kuwa usumbufu kwa hawa wafanyabiashara wetu. Kwa hiyo, nadhani ni mambo ya msingi ambayo tukiangalia kwa uzito wake inawezekana tukawa tumetoa msaada mkubwa sana kwa mamlaka hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake, mimi niseme kwamba tuna wajibu mkubwa wa kuitumia kodi kama motisha ya kuhamasisha *private sector*. Tuna wajibu mkubwa wa kuifanya kodi kama sehemu kubwa ya kuwafanya wale watu ambao wanalipa wawe na moyo wa kulipa wenyewe zaidi kuliko kutumia nguvu nyingi na tuna wajibu mkubwa wa kufanya Mamlaka ya *TRA* iaminike, isionekane kama ni mamlaka ambayo inakwenda kuwaumiza watu. Mtu akimuona afisa wa *TRA* asione kama ameona simba, aone kama ameona binadamu mwenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la sasa hivi ni kwamba yaani ukikutana na afisa wa *TRA* unaweza ukapata presha kabla hata hujaambiwa unatakiwa ukafanye nini. Wamekuwa ni watu wanaoogopwa kwa sababu watu wengi wameshakufa kwa sababu ya kodi kubwa ambayo kimsingi hayaangalii uwezo wa watu. Kwa hiyo, ni vizuri tufanye *transformation* kubwa sana, tuwape tafsiri mpya maafisa wetu wa *TRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Saleh atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Kigua na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi humu ndani kimekuwa kikitajwa kitu kinaitwa *blueprint* na siku moja ulitoa agizo kwamba Wabunge tupewe ili tuwe sawa na Serikali katika uelewa wa kilichomo katika *blueprint* ili tuweze kuifuatilia na tuwajibike Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mpaka leo sijaiona hiyo *blueprint* na Wabunge wengine niliowauliza wanasema hawajapata *copy* ya *blueprint*, pengine wenzetu wanayo sisi hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi una nguzo zake. Ni lazima uzifuate nguzo hizo kwa sababu bila kufuata nguzo za kiuchumi huwezi kufanikiwa. Tupo hapa leo tunapitisha sheria ambayo ni ya lazima, baada ya bajeti lazima tuiptishe sheria hii ili kuipa mamlaka Serikali iweze kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa tunataka kujenga uchumi, lazima uwe uchumi ambao unatabirika. Mwekezaji anakuja hapa anajua kwamba ana uhakika uchumi unaweza kutabirika hakuna mambo yatakatoyotokezea. Lazima katika nchi kuwe na utulivu wa kisiasa, utulivu kwenye haki za binadamu na mambo mengine. Pia tuwe na ushindani halali. Tukiwa na ushindani halali basi mtu yeyote yule anaweza kuwa *interested* kuja kuwekeza kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa kodi, kodi inakusanywa *scientifically*. Kuna misingi ya kikodi, lazima iwe *harmonious*, lazima kodi isikusanywe kwa bugudha. Msemaji wa mwisho aliyepita amesema kwamba *TRA should pull up their act*, wajisafishe, waonekane kama ni wakusanya kodi, mtu asiogope kukabiliwa na mtu wa *TRA*. Pia tujenge utamaduni wa kulipa kodi. Utamaduni wa kulipa kodi umfanye raia aone kodi yake inatumika vipi. Ukimfanya raia anaamini kama kodi yake inatumika vizuri basi *twabaan* na yeye atakubali kutoa kodi bila tabu yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nipongeze kwamba sasa hivi Tanzania *tax base* ni ndogo sana. Ikiwa *tax base* ni ndogo sana wanaobeba mizigo mabeba yao lazima yataelemewa, ni vizuri Serikali itafute njia mbalimbali za kuongeza *tax base* ili walipaji kodi wawe wengi na mzigo uwe mwepesi na ndiyo maana vilevile nikisema hapo nakubaliana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba mfumo wetu wa mara hii haukuja na kitu kipya katika kodi, hakuna *innovation*, ni zile zile kodi za kawaida zimechezewa hivi zimebadilishwa hivi, hatukuwa na *innovation* katika Serikali. Tungependa Serikali kila mwaka ije na *innovative ideas* ili kuwe na hamasa ya kulipa kodi, lakini pia ishawishi watu wengine wajaribu kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mimi nayaona mazuri na ambayo nayaunga mkono mojawapo ni hili suala vifaa vya plastiki, lakini nakubaliana na upande wa Kambi kwamba hili liwekwe sawa, kwenye suala la vifaa vya ujenzi, sekta hii tunajua inaweza ikachangia kiasi kikubwa kwenye uchumi, kwa hivyo ile *concern* iliyotolewa na Kambi ya kutofautisha ya kujua vifaa vinavyotoka nje na ndani ingekuwa sawa, hili ni eneo zuri

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni hili la kuondosha kodi kwa majokovu au vifaa vya kuhifadhia. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbene kwamba wigo ungepanuliwa tukaenda kwingine zaidi kwenye uvuvi na kwenye vitu vingine. Wakati mwingine hata hizi *dry goods* zinapaswa ziwe katika *temperature* maalum, bila kuwa na *temperature* maalum zitaharibika, kwa hivyo hiyo pia itengenezwe vizuri. Pia hii ya vilainishi na ya tiketi inakusudia kuibeba *Air Tanzania*, si vibaya, lakini itumike vizuri kwa makampuni yote ya ndege ili ushindani uwe ni *fair*, kama nilivyosema pale juu unatakiwa tuwe na ushindani *fair*. Hata hivo, sidhani kama walivyosema kwenye Kambi sidhani kama itaongeza sana kwa sababu ni makaratasi ya nembo na kitu gani, lakini angalau itaweza kusaidia

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nimekipenda ni *Tax Ombudsman*, hii ni nzuri na inaweza ikatufaa sana, lakini kuwe na watu *impeccable* kwa tabia zao, waaminifu wa kutosha, kwa sababu hapo yatakuja yale aliyoyasema Mheshimiwa Japhary unakwenda kupatana, unakwenda kwa *tax abuse*, matokeo yake watu wanakugeuzia kibao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nimekifurahia ni kuondosha kodi *immediately*mtu akianzisha biashara apewe muda wa kujitayarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine alichokizungumzia ni hili suala lililosemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kuhusu punda na kodi za punda. Kwa kweli kama tusipoweka vizuri punda wata-*disappear* na baadaye tutawatafuta

kama nyara ya Taifa. Chochote kile kinachowahusisha Wachina *it is a big market*, kwa hivyo mahitaji yake yanakuwa ni makubwa sana. Labda niseme kidogo kuhusu punda kwa wale ambao hawajui. Punda ngozi yake ikisagwa inatoka *powder* inaitwa *gelatin*, *gelatin* inauzwa kilo dola mia 500 China au *Far East* kwa ujumla na wao wanaamini ina-*regulate menstruation* (hedhi), wanaamini inaondosha usingizi, wanaamini inaongeza nguvu za kiume, kwa hiyo kwao ni soko kubwa sana. Kwa hiyo kama hatukuongeza kodi au kutengeneza mazingira kwamba watu ambao wanaweza wakafanya mashamba ya kufuga punda yakawa ni rahisi kuyaendesha, tunaweza baada ya muda tukajikuta kwamba hatuna punda katika nchi hii

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nataka niseme kwamba, tunasema tunakwenda katika uchumi wa viwanda na uchumi wa kipato cha kati, lakini kuna haja ya kutengeneza mazingira mazuri zaidi ili tuelekee huko. Hali inavyokwenda hivi sasa ambapo bado inaonekana hakuna *space* kubwa ya wafanyabiashara kutoa maoni yao zaidi ya kwenda kwa Mheshimiwa Rais, tungependa *base* iwekwe huku kabla ya kumfikia Mheshimiwa Rais, taarifa zinaanza kufika kwa Serikali kwa njia nyingine, kwa sababu Rais hawezi kukutana na wafanyabiashara kila muda mfupi, inachukua muda mrefu sana tuongeze namna ya kutoa maoni wafanyabiashara na wawekezaji ili maoni yao yaweze kufanyiwa kazi, kabla ya kusubiri mpaka Mheshimiwa Rais apate muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Omari Kigua, nilishamtaja Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kusema machache juu ya hoja iliyopo mezani. Ni ukweli usiopingika kwamba kodi ndiyo kila kitu, bila kodi nchi haiwezi kwenda mbele, lakini moja ya sifa ya kodi lazima kuna mambo mawili

kwanza iweze kulipika kwa urahisi, lakini wale walipa kodi pia wawe *willing* wao wenyewe kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya yatafanyika vipi? Haya yanaweza kufanyika kwanza kwa kutoa elimu kwa walipakodi, lakini kuweka utaratibu ulio mzuri kwa walipakodi wenyewe. Wazungumzaji wengi waliozungumza hapa wamezungumzia namna ya ku-*wide tax base*, unapozungumzia namna ya ku-*wide tax base* maana yake utoe fursa kwa wananchi walio wengi waweze kulipa kodi na wasilipe wananchi wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina taarifa juu ya wananchi wa Tanzania kwamba *population* kwa mwaka 2019 tupo takriban 55,890,747; umri wa kuanzia mwaka sifuri hadi miaka mitano, ni 9,628,845; umri wa miaka sita hadi 19 ni 20,836,171; na umri kuanzia miaka 20 hadi miaka 64 tuko takriban 23,691,000. Hapa ndipo ambapo nataka nizungumzie kwamba, hapa ndipo tunataka tukusanye kodi.

Ukichukua wafanyakazi wa Tanzania hawazidi 500,000. Katika kundi hili wakulima ni takriban asilimia 65, sasa unaona kuna Watanzania takriban 13,000,000 ambao hawapo katika mfumo rasmi wa kulipa kodi. Sasa hapa ndipo ambapo Mheshimiwa Waziri namwomba sana kupitia Kamishna wa *TRA* hebu wakae chini waangalie ni Watanzania wangapi ambao wanalipa kodi na wapi ambao hawalipi kodi, kwa sababu kodi hizi zisilipwe na watu wachache kwa manufaa ya watu wengi, kila Mtanzania anao wajibu wa kulipa kodi ili tuweze kujenga barabara, tujenge zahanati, pamoja na mashule yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kulizungumzia tu hapa nipongeze kwenye hasa kwenye mabadiliko yenye *Cap 233* ambayo mabadiliko yamefanyika hapa. Niiipongeze sana Serikali wamelenga hapo hapo kwenye kuongeza *tax base* kwamba wameona waongeze na wamepunguza kodi kutoka 150,000, wamepeleka mpaka 100,000 na hapa wamelenga kukusanya mapato ya kutosha, lakini pia wamewapa *relief* hawa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nimeliona na ambalo pengine watu wengi hawajalionani hili la kwamba hawa walipakodi walipaswa kupeleka mahesabu yao kwa watu ambao ni wataalam wenye CPA. Hata hivyo, wamesema sasa kuanzia 20,000,000 hadi 100,000,000 ndiyo watakaopeleka pale, kwaiyo kundi hili kubwa maana yake kwanza litakuwa limepunguza gharama ya hawa wataalam wa mahesabu. Hili ni jambo zuri sana ni jambo la kupongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *Blue Print*. *Blue Print* hii haipo Wizara ya Fedha, lakini ipo kwenye Wizara nyingine, lakini *blue print* hii ndiyo ambayo inaleta *conducive environment* kwa ajili ya wafanyabiashara, kwa ajili ya *investors* wa nje, lakini na Watanzania kwa ujumla. Naomba jambo hili Serikali ilione kwamba ni jambo la kufanyia haraka sana na wameanza kwa kuondoa kodi hizi 54. Hili kwa kweli nipongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sehemu ndogo sana ya mabadiliko haya. Ili tuweze kupunguza kero hizi kwa kweli lazima *blue print* ifanye kazi sana, lakini suala la *blue print* lisiwe kwa Waheshimiwa Wabunge tu, liende mpaka kwa wataalam kule, liende kwa wananchi wetu waone kwamba dhamira ya Serikali hii sasa hivi ina lengo la kuhakikisha kwamba inatengeneza mazingira mazuri sana kwa wafanyabiashara na hii kwa kweli nadhani itatusaidia sana, tumeanza lakini nadhani sasa Wizara ya Fedha ambayo ndiyo wenye dhamana ya kukusanya kodi, nashauri sana sana wawe *serious* na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni uanzishwaji wa Ofisi hii ya Malalamiko, kwa kweli ni jambo la kupongeza sana. Nimeona wametaja sifa za huyo atakayeongoza ofisi hii, hii ni ofisi muhimu sana, ni ofisi ambayo itahitaji mtu ambaye ni mbobezi mkubwa sana wa mambo ya kodi, lakini pia mbobezi wa mambo ya fedha, lakini mtu huyu au ofisi hii pia tuiruhusu iweke utaratibu wa kwenda kwa wananchi kupata maoni yao, kwa sababu wakikaa tu ofisini hii inaweza isisaidie sana. Pia napongeza

kwamba haitakuwa ni ofisi ya mwisho ya malalamiko, wanaweza kwenda kwenye *Tax Tribunal*, hili ni jambo pia la kupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumza naomba niende kwenye maoni ya Kamati ya Bajeti. Kwenye ukurasa wa 19 wameomba Serikali, Wizara ya Fedha wafanye mabadiliko katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 2009 ambayo ni *The Local Government Finance Act*. Hapa nimekuwa *very interested* kuzungumzia kwa sababu inahusu Mkoa wa Tanga. Eneo la Mkoa wa Tanga kuna mashamba ya katani na maeneo yale kuna halmashauri kama tatu hivi tukizungumzia Korogwe Vijijini, Wilaya ya Mziha na sehemu ya Handeni halmashauri hizi zilikuwa zikikusanya kodi kupitia zao hili la katani, lakini halmashauri hizi zimekuwa zikikosa mapato hayo kwa muda mrefu kutokana na sheria hii ambayo inanyima halmashauri kukusanya kodi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwapongeze sana watu wa bajeti kwa kuliona hili kwa sababu kupitia sheria hii halmashauri au Mkoa wa Tanga wameweza kukusanya shilingi milioni 932 tu kiasi ambacho ni kidogo, lakini mabadiliko yakifanyika Mkoa wa Tanga kupitia hizi halmashauri tatu watakusanya Sh.9,324,511,377.90. Sasa unaona kwamba sheria hii ilikuwa inanyima mapato hizi halmashauri, kwa kweli namwomba sana Waziri wa Fedha aone umuhimu wa kuchukua maoni ya Kamati ya Bajeti kwa sababu ni eneo ambalo litasaidia kuwapa mapato halmashauri zetu na mapato mengi ya halmashauri sasa hivi yamepungua. Nina uhakika suala hili likifanyiwa kazi, basi halmashauri hizi ambazo zinategemea mapato makubwa kutokana na tozo hii ya asilimia tatu ambayo itatokana na zao la mkonge itaweza kuongeza mapato ya halmashauri zetu

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo pengine ningependa kuchangia, kwa siku ya leo ni eneo ambalo linahusu kodi tena. Nimeona kwamba kuna maeneo mengi ambayo wamefanya mabadiliko, lakini bado nishauri, namwombe Kamishna wa TRA analo jukumu kubwa sana

sana na timu yake kuweza kupitia sheria mbalimbali, tumepitisha sheria hizi, lakini bado wao wana nafasi kupitia mkutano ule na Mheshimiwa Rais wao kuweza kujifungia kuona kwamba ni maeneo gani mengine ambayo wananchi wamekuwa wakiyalalamikia na hususan eneo la Kariakoo. Eneo la Kariakoo watu wengi wamelizungumzia ni kitovu cha mapato pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo ambalo wengi wamelizungumzia, suala la *property tax*, hawa wenye majumba Kariakoo, *property tax* hizi wakizipeleka kwa wafanyabiashara hawa wadogo wadogo ambao ni wapangaji pale, jambo ambalo kimsingi siyo sahihi hata kidogo. Namwomba Mheshimiwa Waziri na watu wake wa TRA waangalie namna ya kulipitia hili ili wale wafanyabiashara ambao wana dhamira ya kulipa kodi ambayo siyo wakwepaji wa kodi waweze kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niweze kutoa mchango wangu kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019. Ni dhahiri wote tunakubali kwamba tunahitaji kodi ili iweze kwenda kujenga miundombinu mbalimbali kama hospitali, barabara na mengine, lakini lazima tuwe na muundo ambao unakusanya kodi zenye tija na kutoka *source* ambazo zina uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi kodi inaweza kuwa ni mojawapo lakini tuna vyanzo vingi sana ambavyo tungeweza kupata mapato mbadala na kutoku-*rely* kwenye baadhi ya kodi kwa kweli ambazo hazistahili kuwa kodi. Naomba kwenye marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa

Bidhaa, Sura 147, Serikali inapendekeza kifungu cha 7 chenye *HS code* 6703.00.00, 6704.11.00, 6704.19.00, 6704.20.00 na 6704.90.00 ambazo ni nywele bandia, bandia kope bandia, yaani na Waziri kabisa anasema kwamba lengo la kuweka hii kodi ni kuhakikisha kwamba tunapata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa na kama ilivyokuwa imependekezwa awali na nasikitika bado Serikali inang'ang'ania hizi kama chanzo, huwezi ukasema leo unaweka asilimia 10 kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha hizi nywele bandia na asilimia 25 kwa wale ambao wana-*import* ili uweze kuongeza mapato. Siyo chanzo halisia, hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe umependeza na hujaweka nywele bandia. Mheshimiwa Grace Kiwelu hapa, Mheshimiwa Dkt Sware, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Salome na wengine wote, sasa Watanzania akinamama tukiamua kwenda hivyo, tusiweke hizo nywele bandia, hiki chanzo siyo halisia, kabisa. Tunapita hapo tutapoteza muda, tutapitisha, tutafanya kila kitu, mwisho wa siku tutakuja hapa haya mapato hayapo, ndiyo yale wana-*project* bilioni kadhaa, wakija uhalisia makusanyo chini ya asilimia 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado nasisitiza kabisa hiki kiondolewe chote hiki kifungu cha 7 chenye *HS code* 6703.00.00, *HS code* 6704.11.00, 6704.19.00, 6704.20.00 na 6704.90.00, wakiondoe ni aibu kwanza. Hii wanaenda kusababisha wajasiriamali akinamama ambao wamewekeza kwenye *saloons* na hivi vitu vingine waweze kuyumba. Sasa kama ni Serikali ya wanyonge...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko kuna taarifa, Mheshimiwa Getere

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba nimpe mdogo wangu Esther kwamba kwamba habari ya nywele gharama za kutoa

nywele hazihusiki na wanawake zinahusika na wanaume. Sisi wanaume siyo wanawake...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, naona umesimama.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, hicho alichokisema kaka yangu ambaye baada ya Jimbo kuachiwa kaenda kule kijijini, ni udhallishaji wa wanawake, si kweli kwamba wanawake au kila mwanamke anategemea mwanume ili apendeze, huo ni udhallishaji, afute kauli yake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Mheshimiwa Getere amesimama akitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Esther Matiko, kuhusu nani wanunuzi wa vifaa bandia ama nywele bandia ama kope bandia na vitu vyote vilivyoandikwa kwenye hicho alichokuwa anachangia Mheshimiwa Esther Matiko, kwamba hata hivyo wanunuzi wa hivi vitu ni wanaume na amesimama Mheshimiwa Ester Bulaya akisema kwamba kwa kusema hivyo Mheshimiwa Getere anadhalilisha wanawake.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepata fursa ya kusikiliza nadhani michango yote ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri kabla hatujahitimisha jana. Hata hivyo, nilisikia humu ndani sisi wenyewe wanawake na kama kuna mtu hakisikia ataenda akafuatilie Taarifa Rasmi za Bunge, humu ndani alisimama mwanamke akisema kwamba...

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Nani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga nimesimama unazungumza.

Kwa hiyo, alichangia kana kwamba hoja hii namna inavyopelekwa mbele tusiisitize sana kwamba tunalipishwa kodi wanawake kwa sababu kulikuwa na mchango wa

namna hiyo. Huyu alivyosimama akasema hii kodi huwezi kusema tunalipishwa wanawake kwa sababu na wanaume wanahusika kwenye kununua. Sasa alipokuwa anazungumza mwanamke huyu sikuona popote ambapo tulisimama kuonyesha kwamba ule ulikuwa ni udhalilishaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimesimama hapa ili niweke vizuri, michango yetu anapochangia mwanamke kama na yeye anadhalilisha basi na yeye aambiwe hivyo na pia anapochangia mwanaume kama anadhalilisha na yeye aambiwe hivyo. Maana yake nini? Ni hivi yale maneno tunayoweza kuyasema mtaani huko tusiyaweke hapa ndani kwa sababu watu wengi walioko hapa ndani lakini pia hata huko nje, tunavyozungumzia hamsini hamsini siyo hamsini tu ya kuingia humu ndani ni hamsini na mambo mengine ikiwa ni pamoja na kujinunulia nywele na kulipa ada za watoto na mambo kama hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tusifike mahali tukaona wanaume ndiyo lazima watuhudumie, tuna uwezo wa kujihudumia wenyewe lakini ni pamoja na sisi wenyewe wanawake kulikubali hilo. Kwa sababu isitokee mwanamke anachangia kwa namna tofauti tukaona ni sawa lakini mwanaume akizungumza tukaona ni tofauti. Kwa hiyo, wanawake na wanaume kwenye jamii yetu tunatofautiana, wapo wanawake wanaotegemea wanaume lakini wapo wanaume wanaotegemea wanawake, tunategemeana.

Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru, muda wangu, nilikuwa nimeongea dakika moja tu. Hujaniuliza kama napokea taarifa au naiacha.

NAIBU SPIKA: Kwa sababu haikuwa taarifa, kwa hiyo, endelea na mchango wako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ila siku nyingine Wabunge kama hawa wasiwe wanaingia Bungeni. Kama umenisikiliza kuanzia mwanzo nimesema hiki

siyo chanzo halisia cha kodi, *you can not rely on this*. Halafu unatuaibisha sana watu Mara ndugu yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, kwa hiyo, bado nasisitiza kwamba hii kodi iondolewe kabisa. Mapendekezo yangu hii kodi yote iondelewe kwa vifungu vyote ambavyo nimetaja, kwanza siyo halisia lakini pili inaweza ikaweka ugumu kwa wale wa akina mama ambao wamejiwekeza kwenye ujasiriamali wa *salon* na vitu vingine kama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni Sehemu ya Nne, *amendment of Income Tax Act, Cap 332*. Katika marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kifungu cha 9, Serikali pia inapendekeza kiongezwe kipengele (d) kwenye kipengele cha (a)(iii) ambapo pamoja na mengine yote kuhusiana na taalo za kike mmesema mtaweka hiyo *exemption* kwa makampuni *for two years* kwa *corporate income tax* lakini pia kuna sheria ambayo iliondoa *import duty of which* makampuni hayajaelezwa, ni mawili tu ndiyo yamepata kupata msamaha wa kuingiza bila huo ushuru wa bidhaa. Kikubwa hapa taalo za kike pamoja na hizi *measure* ambazo mmezionyeshwa hapa hazitasaidia kupunguza hapa bado nasisitiza kwamba Kodi ya Ongezeko la Thamani iondolewe kwenye taalo za kike kama vile ambavyo tulifanya mwaka wa fedha uliopita. Hii itamsaidia siyo tu mwanamke wa Kitanzania, tulilenga pia kuwasaidia watoto wetu ambao ni wanafunzi wanashindwa kwenda shule wakiwa kwenye siku zao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *excuses* ambazo Serikali ilitoa hapa kwamba ikiweka *VAT* haina athari kwenye bei ya mlaji haina mashiko. Kama Serikali mnatakiwa kusimamia kuhakikisha kwamba ushuru umeondolewa huu wa *VAT* lakini wale wauzaji na wasambazaji wapunguze bei, *it can be done*, nyie Serikali vingapi mmevisimamia na Waraka zinatoka na wauzaji wanafuatilia, *why not this?* Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kabisa Serikali muangalie suala hili kwa jicho la kipekee kuhakikisha mnamsaidia siyo tu mwanamke wa Kitanzania bali na wale mabinti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kabisa jana nilisikitika Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba mojawapo ya *factor* ya kuondoa hii, kwanza baada ya kuondolewa kuna baadhi ya Wabunge hapa walizunguka wakawa wanapongezwa na nchi za nje, kwa hiyo, ikawa ni *factor* mojawapo ya kurudisha kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kitu ni cha ajabu sana yaani wakienda nje wakawa *proud of* kwamba Serikali yetu imeondoa kodi ni sifa kwa Serikali na wala siyo chanzo cha ku-*penalize* watu hawa. Hii ni ajabu sana kwa sababu Mtanzania akipewa tuzo huko nje ni sifa kwa Serikali yake. Kwa hiyo, naomba kabisa hii kodi iweze kuondolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha, *clause* ya 39(5).

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Muda wangu ndiyo kwanza kengele ilikuwa imegonga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, usiuzungumzie sana muda kwa sababu kengele ya kwanza imeshagonga hapa. Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, mwanamke wa Mara kwamba sisi watu wa Mara tunasikitika sana tunapokuwa tunazungumzia mambo ya pedi na nywele. Kule kwetu haya mambo ni aibu kuyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimpe taarifa kwamba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko malizia mchango wako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, sema muda umeenda lakini nasikitika kama na wewe ni mmoja wa watu kutoka Mara kwamba mwanamke wa Mara hastahili kupata pedi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki cha 39(5) kinasema kwamba biashara inavyoanzishwa hawa wafanyabiashara wanya wanapata ahirisho la kulipa kodi kwa miezi sita wanakuja kulipa baadaye. Mimi nasema hii haisaidii, napendekeza Serikali itoe msamaha kabisa kwa miezi sita ya mwanzo wakati biashara inaanzishwa ule mwezi wa saba ndiyo hawa wafanyabiashara waweze kutozwa kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukisema unafanya ahirisho la muda kwamba unampa muda wakati anaanzisha ile biashara *suppose* inafika mwezi wa sita au wa saba huyu mtu anashindwa kuendesha biashara ile ndiyo utaanza kuona mnakimbizana mnamkamatia mali zake maana biashara imekufa wakati anatakiwa alipe malimbikizo. Kwa hiyo, nina-*propose* wapewe *tax holiday* kama tunavyowapa makampuni ya nje yanayokuja hapa nchini, ya *six month* kuanzia mwezi wa saba ndiyo waanze kutozwa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa Serikali imeleta kifungu kingine ambacho kinaingiza kwenye sheria na kanuni kwamba sasa mwenye dhama ya kusimamia masuala ya vitambulisho vya wajasiriamali ni Waziri. Kwanza nashukuru limekuja lakini nasikitikia kwamba vitambulisho vilishasambazwa kitambo na ma-DC na Wakuu wa Mikoa leo ndiyo mnatuletea kipengele hiki kuingiza kwenye kanuni na sheria kwamba Wizara sasa iweze kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa hapo tunaenda kumtoza huyu majasiriamali kitambulisho Sh.20,000 wakati huo huo makampuni ambayo mapato yao *turnover* ni shilingi milioni 4 kwa mwaka hawatozwi chochote. Kwa hiyo, tuna

nia ya dhati ya kumsaidia Mtanzania maskini au tunafanya tu? Unamsamehe mtu wa shilingi milioni 4 asilipe chochote unaenda kumdai mama ntilie mtaji wake Sh.15,000 au Sh.30,000 unampa kitambulisho cha Sh.20,000. Kwa hiyo, hii nayo kwanza tuitafakari mara mbili mbili ikiwezekana iondolewe kabisa. (*Makofi*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Msigwa tutamalizia na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. MCH. PETERS. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi. Nina mambo mawili, matatu nitaongea kwa kifupi na kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumza nilitaka nitoe ushauri kwa Serikali kwa sababu tunapokusanya kodi lazima tuwe na jicho pana namna ya ukusanyaji kodi. Kwa mfano, mwaka jana au mwaka juzi tuliongeza kodi kwa watu wanaokuja kidini, kwa mfano, tukatoza dola 500 kwa ajili ya *residence permit, labor permit* dola 500 ambayo inafika karibu dola 1,000. Sasa ukiangalia jicho la Serikali ni kuangalia tu ile pesa ambayo wanaiingiza wanapoingia lakini hawamuangalii huyu mtu anapokuwa nchi ni kiasi gani cha pesa anakiacha ndani ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu anakuwa na watoto ambao watakwenda kusoma atapeleka pesa shuleni, tayari ni hela tunazipata sasa Serikalil haioni katika jicho hilo. Huyu mtu atakwenda kwenye *super market* ataacha pesa Serikali haioni kwa jicho hilo. Huyu mtu atakwenda kwenye *clubs* atakutana na watu mbalimbali wata-*socialize* wanatafanya manunuzi yapatikane katika nchi, Serikali haikuangalia hivyo inaangalia tu ile kodi ya mwanzo matokeo yake tumekimbiza watu wengi sana nchi za jirani zinawachukua kwa sababu wao wanalipa kidogo. Kwa mfano, Rwanda hapa wa-*missionary* wengi ambao ni

rafiki zangu wameondoka hapa wameenda Rwanda wakati sisi tunatoza dola 1,000 pale wanatozwa *equivalent* na dola 110 na *process* ni siku tatu wakati hapa nchini *it take ages*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali tunapotafakari masuala ya kodi na kuzuia hizi *permit* watu kuja nchini tuangalie ni matumizi kiasi gani yanaweza kutumika baada pale kwa sababu tukiji-*limit* kwenye hela ile wanaotoa mwanzoni ni ndogo sana matokeo yake tunapoteza maeneo mengi, shule zinafungwa, hoteli zingine ziliajiri watu zinafungwa kwa sababu watu wa nje waliokuwa wana-*accommodate* maeneo hayo wameondoka. Kwa hiyo, naishauri Serikali mnapofanya mambo muwe mnaangalia kwa mapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka kuzungumza katika Muswada huu, Serikali imekuwa ikisema inamjali mnyonge na kimsingi mtu mnyonge kwa Tanzania ni mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mkulima anafanya kazi usiku na mchana, ndiyo wanaolisha Taifa letu, wanafanya kazi kwa tabu sana. Kwa bahati mbaya Serikali yenu ya CCM siyo siri mmewavuruga wakulima wa korosho. Mmewaleta adha katika maisha yao lakini kama vile haitoshi sasa tena mnataka mvuruge wakulima wa pamba. Bei ya pamba soko limeshuka duniani na mkulima sasa hawezi kuuza pamba yake lakini nilitegemea mnapoleta sheria hizi walau mngempunguza hizi kodi.

T A A R I F A

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Si uvumilie?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa, kuna taarifa, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Msigwa, Serikali haijavuruga wakulima wa korosho bali Mheshimiwa Rais alilazimika kuingilia kati baada ya mfumo mzima wa mnada kutoa bei ya unyonyaji. Baada ya kuapishwa mimi mwenyewe nimeenda ghala kwa ghala kuangalia hali ya koroshona kuona korosho yetu bado ni bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichokifanya, sasa hivi tumeandaa *catalogue* ambayo inaonyesha *quality* ya korosho ni nzuri na sasa tunajiandaa kutumia mfumo wa *TMX* kuiambia dunia kwamba korosho ya Tanzania bado ni bora. Hata hivyo, kupitia wapotoshaji wachache kama Mheshimiwa Msingwa anavyofanya, dunia imelazimika kuamini kwamba korosho ya Tanzania si bora. Wewe ndiyo unawavuruga wakulima wetu wa korosho si Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kumpa taarifa hiyo, tutangulize uzalendo kwanza. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msingwa, unaipokea taarifa hiyo.

MHE. MCH. PETERS. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake siipokei kwa sababu yeye amesema walikuwa wanazuia bei za kinyonyaji lakini sasa nyie ndiyo mmepeleka bei za kiporaji kwa sababu wananchi hamjawalipa pesa zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri wa Viwanda nikushauri na ukamshauri Mheshimiwa Rais, hizi korosho bora mkachome kwa sababu mtaathiri hata korosho zinazokuja kwa sababu hazina soko, mmeziharibu, zinaoza. Sikutaka tufike huko lakini kama mna nia nzuri na nchi yetu hizi korosho zichomwe moto, muwalipe fidia ili tuanze upya kwa ajili ya *future reference* ili watu waone korosho ni bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali hii inasema inawapenda wanyonge hawa watu wa *ginneries* wana kodi

kibao na hawa ndiyo wateja wa wakulima wa pamba. Kwa mfano, kuna baadhi ya kodi anatozwa huyu mtu wa *ginneries*, anatozwa *fire*, *service levy*, leseni ya manispaa na viwanda, *weight* na *management*, *OSHA*, kodi ya mapato hizi zote zinaenda kwake.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Sasa Mheshimiwa Inno itakuwa Bunge gani hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msingwa kuna Kanuni inafunjwa, Mheshimiwa Innocent.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 63(4), Mheshimiwa Msigwa amesema kwamba korosho ya wakulima wetu imeoza na mimi nimetoka kwenye maghala yote tumefanya *cutting taste* tuna *catalogue* ambayo inaonyesha kila *lot* ya korosho ipo katika hali ya namna gani, korosho yetu bado ni bora. Sasa ningependa Mheshimiwa Msigwa athibitisha kama korosho imeoza kweli.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama korosho haijaoza basi kwa kutumia Kanuni za Bunge Mheshimiwa Msigwa achukuliwe hatua. Kwa sababu korosho ya wakulima wetu bado ipo katika hali nzuri na mimi nina ushahidi naweza nika-*print* hiyo *catalogue* nikakukabidhi sasa hivi na yeye kusema kwake kwamba korosho imeoza athibitisha kama kweli korosho imeoza. Nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati akiichangia Mheshimiwa Msigwa amesimama Mheshimiwa

Innocent Bashungwa kwa mujibu wa Kanuni 63 (4). Kanuni hii ya 63 inakataza kusema uongo. Kwa muktadha wa kanuni hii nzima ukiisoma inamtaka Mbunge anayesema Mbunge mwingine anasema uongo anapaswa kuthibitisha yeye kwanza kwa mujibu wa fasili ya (5) na nyingine zilizopo hapo ili sasa Mbunge yule aliyekuwa anachangia kabla ya yeye kusimama kuhusu utaratibu aweze kupewa fursa ya kuthibitisha yale aliyoyasema ama vinginevyo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini niseme hivi, kwa muktadha huo huo wa Kanuni ya 63 nadhani Mheshimiwa Msigwa na natumia neno 'nadhani' Mheshimiwa Msigwa hoja yake ilikuwa kwenye korosho kwamba bado zipo maghalani zinunuliwe. Sasa baada ya kupewa taarifa ndiyo ameenda huko kwenye korosho kuoza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa nyoosha machango wako vizuri ili tusizipungukie Kanuni zetu namna zinavyotutaka. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kutoa mwongozo vizuri na ningeomba tu ileweke sisi ni Wabunge na hapa tupo kuwatetea wananchi dhidi ya *government*. Kwa hiyo, hatuko hapa kitu chochote kinacholetwa na Serikali tukiamini. Ndio maana huwa inaundwa Kamati ya Bunge kwenda kuchunguza, *I don't trust what you are talking*, vinginevyo iundwe Kamati ya Bunge ikathibitishaye hayo unayoyasema, *why do you what me to trust what you are saying?*

Mheshimiwa Naibu Spika, niko hapa kwa niaba ya wananchi, mimi napata ripoti kwa wananchi, tupo hapa kuwasemea wananchi *verses the government* ili *government* iwatumikie wananchi inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichokuwa nasema hizi kodi zinamfanya mkulima apunjwe kwa sababu hawa watu wanachajiwa kodi zote hizi hapa mwisho wa siku hizi kodi kwenye pamba zinamfanya mtu anayeumia wa mwisho awe ni mkulima. Kwa hiyo, nilitegemea Muswada huu utakapokuja hapa kama kweli mnawajali wanyonge mngewakumbuka hata wanyonge wa pamba, mahindi

ambao mara nyingi wakilima mahindi yao mnazuia hayauzwi matokeo yake wanapata hasara, wanakuwa hawaondoki kusogea mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kwenye michango yetu tumesema mngempunguza kodi za mabati, za nondo, hivi vitu vya kujengea wananchi hawa wanyonge mnaowasema ingewasaidia.

Sasa mmevuruga wananchi wapo *stacked*, *it is obvious* wananchi wa Mtwara wapo *stacked*, hii haihitaji *rocket science* kuelewa kwamba shughuli ya korosho imewashinda na mngokuwa waungwana mngesema *we blue it*, tungewaona mna busara lakini bado mnabumbabumba tu, mnatudanganya hapa, *you blue it brother*. Mngetuambia tumeshindwa tuanze upya, *what is the way forward*. Sasa tusipokuwa waangalifu msimu wa korosho unaokuja tutaharibu tena kwa sababu ya ubishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilisema *if you are lost you don't have to accelerate you stop and you read the map*, unatafuta njia inaenda wapi. Tusipokuwa waangalifu, kama suala lenyewe ndiyo hiyo pamba ime-*stack* mbona hajampeleka Jeshi kwenye kununua pamba? Kama Jeshi ina-*work*, kama hiyo *methodology* mliyotumia *it is working* kwa nini hamja *deploy* makanda kwenda huko kwenye pamba si hainunuliwi sasa hivi hapa?

MBUNGE FULANI: Na kahawa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Na kahawa. *We told you* kwamba haya mambo yanahitaji *negotiation*, tunajadiliana, tunakuwa na *mutual understanding* na ndiyo maana tupo hapa kushauriana tunataka taifa letu liende mbele.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Msigwa, muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mashimba Ndaki, tumalizie na Mheshimiwa Mashimba Ndaki. Kanuni yetu ya 28, Fasili ya pili inanitaka niwahoji Waheshimiwa Wabunge ili tumalizie hizo dakika 10 za Mheshimiwa Ndaki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukubali kwamba na mimi nizungumze angalau kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kukubali mambo mengi ambayo kwenye Kamati ya Bajeti tulipendekeza kwenye Muswada na kwa kweli wamejitahidi kuyafanyia kazi. Wamekubali kutoongeza ushuru wa bidhaa kwa ile wanayoongeza kila mwaka asilimia tano, lakini pia wamekubali kwamba wafanyabiashara wanapoanza kufanya biashara na wawekezaji basi wapewe kipindi cha miezi sita mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze mambo machache tu, la kwanza ni Sheria yetu ya Bajeti na inaposomwa pamoja na Sheria ile ya *Public Finance Management*; ni kwamba Bunge lako linaanza kushughulika na bajeti mwezi wa Nne na kuendelea, lakini Wizara ya Fedha inaanza kushughulika na masuala ya bajeti na kikodi mwezi wa 12 na kuendelea na matokeo yake kunakuwa na *mismatch* ya namna fulani ya kushughulikia jambo lile lile. Sasa nadhani kuna haja ya kuangalia ili ku-*harmonize* hizi sehemu kama mbili au tatu zinazoshughulikia bajeti; Bunge, Wizara au Serikali lakini pia na wenzetu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha anakutana na wenzetu wa Afrika Mashariki kipindi ambacho Bunge lako Tukufu halijakutana na kuzungumza au na kuona kile

kitakachozungumzwa na Waziri wa Fedha kule Afika Mashariki. Sasa haya mambo nadhani yanahitaji kuwekwa sawa sawa ili kwamba tuweze kutembea pamoja na kwamba inapofika sasa tunashughulikia suala la bajeti ya nchi yetu hasa Bunge lako kuanzia mwezi ule wa Nne na kuendelea, basi kuwe na vitu ambavyo tumeshakubaliana tayari kupunguza mivutano ambayo inaweza kuwepo na wakati mwingine inaleta sintofahamu isiyo na sababu. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka nizungumzie suala la vitambulisho vya Wajasiriamali. Naishukuru Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwa *pro-active* na kufanya jambo hili sasa litekelezwe kwenye nchi yetu pamoja na kwamba upo upungufu ambao umekuwepo, lakini angalau sasa linatekelezwa, wajasiriamali wanasajiliwa ili baadaye waweze kulelewa na hatimaye waweze kufanya biashara kubwa. Kitu kimoja tu ninachotaka kushauri kwa Serikali ni kwamba vitambulisho hivi sasa viboreshwe. Kwa hivi vilivyo haviko tofauti sana kati ya kitambulisho cha mjasiriamali huyu na huyu, kwa sababu hakina hata jina yaani kimeandikwa tu “Kitambulisho cha Mjasiriamali”.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kiwe na jina lakini pia kiwe na picha ya huyo mjasiriamali, lakini pia kiwe na ujasiriamali huo anayofanya huyo mtu. Kama ni Mama lishe iandikwe mama lishe, kama ni muuza mitumba, kiandikwe muuza mitumba, vinginevyo hivi vitambulisho kwa hali vilivyo havijakaa sawa sawa, kwa sababu wanachofanya sasa wananchi wetu ni kupeana hivi vitambulisho. Wewe unacho kitambulisho? Sina, lakini unataka kwenda kuuza kwenye gulio? Ndiyo. Haya chukua hiki hapa cha kwangu. Wanapeana namna hiyo kwa sababu havijatofautishwa sana. Hilo ni suala lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, nataka nizungumzie suala la *under valuation* na *under invoicing* hasa ya bidhaa za nguo zinazotoka nchi za nje hasa maeneo mawili ya China na India. Kwa India tumepata taarifa kutoka kule kwenye Kamati kwamba angalau sasa kuna namna

ambayo wanafanya kwa sababu wameshasaini *memorandum of understanding* suala hili la *under valuation* na *under invoicing* halipo kwa upande wa bidhaa za nguo zinazotoka India, lakini bado kwa bidhaa zinazotoka China bado hawajafikia maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala hili linaumiza viwanda vyetu vya pamba hapa ndani kwa sababu bidhaa zinatoka China zinazuzwa kwe bei ya chini, zinaleta ushindani usio sawa. Kwa hiyo bidhaa zetu za nguo zinazozalishwa na viwanda vyetu zinakutana na ushindani usio sawa na vinashindwa kupata soko kwenye soko letu la ndani. Hivyo, naomba sana TRA, Wizara ya Fedha kwa ujumla walifanyie kazi suala hili ili angalau sasa tupandishe matumizi ya pamba ndani ya nchi tuepukane na habari ya kuuza pamba yetu nyingi nje ya nchi tunapokutana na bei imeshuka chini na kwa hiyo tunalazimika kushusha chini bei kwa wakulima wetu, kitu ambacho kwa utaratibu wa kuongeza kipato cha wakulima wetu, hakikubaliki. Kwa hiyo, naomba kwamba jambo hili lifanyiwe kazi haraka ili tuongeze matumizi ya pamba hapa ndani na pamba yetu tunajua itapanda bei tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia linavyozungumzwa na wenzetu suala la pamba, lakini sisi tunaotoka kwenye pamba sasa hivi tunalishughulikia, Mheshimiwa Waziri Mkuu anazo taarifa na ameshatupa taarifa ya kwamba analishughulikia kwa ukaribu sana na bei wala haijaanguka. Bei ni ile ile ya 1,200 haijateremka kwa wakulima wetu, sasa wenzetu wanalichukua vinginevyo, lakini tunajua wana nia gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yangu yamekwisha nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijazungumza yaliyoko hapa mezani niwataje Wabunge wachache watakoachangia mchana; Mheshimiwa Mendrad Kigola,

Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Salum Rehani, Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo machache hapa mbele, moja siyo tangazo ni maelezo nimeletwa hapa kwa maandishi kwamba wanaume wanaotegemea wanawake basi hao siyo wanaume. Haya ni maoni ya mtu, lakini sisi wanawake tunasema hivi, wako wanaume wanaotutegemea kwa hiyo hamna shida na wao ni wanaume siyo kwamba ni wanawake haiondoi uwanaume wao kwa kuwa watagemezi. Kwa hiyo ni sawa tu na pia wanaume wabadilike mtazamo wao namna wanavyowatazama wanawake. Ni lazima wanaume wabadilike ili na wao kama mwanamke anaweza kumwambia yeye akae nyumbani alee watoto, halafu yeye aende kazini basi mwache mwanamke aende kazini, wewe fanya kazi ya nyumbani. *(Vicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao hawakupata fursa ya kuingia Bungeni asubuhi japokuwa walikuwa wametangazwa na hawa ni wageni wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa. Wageni wake hawa ni Walimu 20 kutoka Shule ya Msingi Vinkawe, Mpwapwa. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Lubeleje. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kuanzia leo hadi tarehe 28 Juni, 2019, Bunge litakuwa na shughuli za kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2019.

Kwa madhumuni ya kutoa fursa kwa Miswada hiyo kupata muda wa kutosha wa kufanyiwa kazi. Kamati ya Uongozi katika Kikao chake kilichofanyika tarehe 18 Juni, 2019, kiliazimia kwamba kwa siku ya Alhamisi yaani kesho tarehe

27 Juni, 2019 na siku ya Ijumaa, tarehe 28 Juni, 2019, kusiwe na kipindi cha maswali ya kawaida ya Wabunge na pia maswali kwa Waziri Mkuu. Kwa uamuzi huo, maswali yaliyokuwa yamepangwa kujibiwa kwa siku hizo yatapewa kipaumbele wakati wa Mkutano ujao wa Bunge, ili Wabunge mpate fursa ya kujadili Miswada hii miwili kwa ukamilifu, kwa hiyo siku ya kesho na keshokutwa hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Tangazo lingine pia linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge pia mnatangaziwa na pia mnahamasishwa kununua kitabu kiitwacho "Kiswahili katika Vyombo vya Habari Ndani na Nje ya Tanzania". Kitabu hicho kimeandikwa na Mwandishi kutoka Shirika la Utangazaji la Tanzania, Ndugu Victor Elia na kuchapishwa na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Gharama ya kitabu hicho ni shilingi 10,000/= na kinapatikana eneo la mapokezi hapo nje. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mtakapokuwa mnatoka mnahamasishwa kununua nakala hizo.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni ya leo.

(Saa 7.09 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha, kuna baadhi ya Wabunge tulikuwa tumeshawataja kwamba tutaanza nao mchana huu. Tutaanza na Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Fedha. Nianze na kuipongeza Wizara ya Fedha kwa marekebisho mbalimbali ya kodi ambayo

yanalenga kuboresha ukusanyaji wa kodi pamoja na kuinua uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kuanzisha kitengo maalum ambacho kitakuwa kinashughulikia malalamiko ya walipa kodi nchini. Hili lilikuwa tatizo kubwa sana ilionekana kwamba wafanyabiashara wakipata matatizo wanakosa sehemu ya kupeleka sehemu malalamiko yao matokeo yake walikuwa wanabaki wananung'unika. Bahati nzuri Serikali mmeliona hilo na mme-*propose* kwamba kitakuwepo kitengo ambacho kitakuwa kinachukua matatizo na maoni mbalimbali ya walipa kodi na kuyafanyia kazi. Mimi hilo suala nimelipenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naipongeze Serikali pamoja na Benki Kuu ambayo ni Serikali yenyewe, Benki Kuu ilipunguza riba kwa benki kutoka asilimia 9 mpaka asilimia 7.5. Lengo kubwa ilikuwa kuona *impact* inapatikana kwa wananchi kule chini. Ina maana kwamba Benki Kuu ikipunguza riba benki za kibiashara tulikuwa tunategemea tupate matokeo yake kwamba na riba zile ndogo ndogo ambazo zinaenda kwa wananchi kule, wakopaji wadogowadogo waweze kupunguziwa riba lakini kwenye mabenki yale ya kibishara bado mpaka leo riba ziko juu.

Kwa hiyo, wananchi bado wengi ambao ni wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo wanashindwa kupata mikopo kwenye mabenki kwa sababu riba ni kubwa. Sasa niombe Serikali kwenye lengo hilo ili tuone matokeo mazuri basi tusimamie vizuri tuone riba kwenye mabenki ya biashara inapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja limeongelewa sana kuhusiana na taulo za kike. Sipendi sana nilirudie lakini nimeona na mimi niliongee. Suala lile ni la msingi sana kwa watoto wetu. Sasa hivi tunavyoenda kufuatana na mabadiliko ya hali ya hewa kuna mambo mengi sana yanajitokeza. Siwezi kusema kuna mambo mengi yanasababisha wakapata magonjwa sisemi hivyo lakini sasa hivi kuna mambo mengi yanatokana na usafi wa kimwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili la taulo za kike naunga mkono asilimia 100 na niipongeze Serikali kwamba na yenyewe imeliona hilo. Kuna *point* moja nimeipenda sana kwamba Serikali baada ya kuona kwa mapana yake watajenga kiwanda ambacho kitakuwa kinatengeneza hizi taulo za kike na kuhakikisha kwamba watoto wanaweza wakazipata kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *point* nyingine walisema kwamba taulo za kike zinaweza zikapatikana mtoto akatumia mwaka mzima, hiyo ni nzuri. Kwa mfano, mtu ananunua mwezi wa kwanza, mwezi unaofuata inabidi anunue tena lakini kama zitakuwepo anaweza akanunua akatumia muda mrefu na kwa usafi zikawa nzuri basi itakuwa imesaidia sana watoto wa kike. Kwa hiyo, hilo nimeona ni suala la msingi kwamba Serikali imeliona hilo, nashukuru sana hata Kamati ya Bajeti tulishauriana vizuri sana kwenye suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niishukuru sana Serikali kwa kutoa tozo kwenye masuala ya visima vya maji hata kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha aliongea vizuri sana hilo na nimeona nilirudie. Hitaji kubwa la kijamii vijijini ni maji na Serikali imeliona hilo. Sasa mimi nitoe *proposal* moja kwamba ili tushambulie kwenye sekta hii ya maji twende vizuri kuna *NGO's*, mashirika ya Kanisa na Serikali yenyewe ipunguze kodi kwenye mitambo ya uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye Kamati ya Bajeti tumeshauri, nimeona hapa tumeandika vizuri kwamba ile mitambo ya uchimbaji visima virefu tupunguze kodi. Kuna wafadhili wengi sana wanapenda kuleta mashine wachimbie wananchi visima lakini kama kodi imekuwa kubwa hata mashirika ya Kanisa wanashindwa kununua zile mashine, hata Halmashauri tu zinashindwa. Tunaweza tukasema Halmashauri inaweza ikanunua ile mitambo ikaendesha uchimbaji wa visima vijijini ili kutatua tatizo la maji, hii itakuwa imetusaidia sana. Nimeona hilo niliweke vizuri ili Halmashauri ambazo zina uwezo wa kununua mitambo hiyo ziwezi kununua kwa bei nafuu na kupeleka maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nimwombe Waziri hii sheria ambayo tumerekebisha kuhusiana na Wakala wa Forodha, kuna watu wengine hapa tunatafsiri vibaya. Tunajua hii sheria inaenda kufuta mawakala wa forodha, wale ma-*agent* lakini kusoma kwangu nimeona kwamba Serikali haifuti isipokuwa inampa nafasi mmiliki wa mzigo kama ana uwezo wa ku-*clear* kule bandarini aweze ku-*clear*.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimeona ni nzuri tu inatoa wigo. Kwa mfano, mtu ame-*import* mzigo kama ana uwezo wa ku-*clear* mwenyewe asiongeze gharama ya kumfuata *agent*. Kwa sababu *agent* anapo-*clear* mzigo bandarini siyo kama ana-*clear* bure kuna fedha pale anatoa. Sasa yeye kama anaona ana uwezo wa kwenda ku-*clear* mwenyewe anaenda pale kwa utaratibu uliowekwa ana-*clear* mzigo wake anaondoka, mimi nimeona ni jambo zuri.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna watu wengine wanaona kama sheria inaenda kufuta yale mashirika ya *forwarding and clearing*. Sasa namuomba Waziri akija hapa aifafanue vizuri kwamba sheria haifuti isipokuwa inampa nafasi yule anaye-*import* mzigo aweze ku-*clear* mzigo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo nimeliona, Serikali kwa mfano ikipandisha kodi ya kuingiza mizigo *importation tariff* inakuwa juu. *Point* kubwa inayoongelewa pale kwamba Serikali inafanya hivi ili ku-*motivate* viwanda vya ndani viweze kuongeza uzalisashaji na uingie katika masoko, ni sahihi kabisa yaani tuna-*reduce competition* kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, unaweza ukaona kuna *product* zinatoka nje zinaingia ndani wanakuja kuuza kwa bei nafuu sana, zile *product* zinaua viwanda ambavyo tunavyo hapa na vinaweza vikazalisha ile *product*, hapa naipongeza Serikali. Mawazo yangu, kuna bidhaa nyingine zinakuwa ni muhimu sana kwetu, kuna nyingine sisi tunatengeneza lakini hazina *quality*, nashauri viwanda vyetu

vitengeneze bidhaa bora siyo kwamba tunawapa nafasi ya kuzuia viwanda vya nje visilete bidhaa halafu viwanda vya ndani vinatengeneza bidhaa hafifu. Ni lazima watengeneze bidhaa bora ili kwenye soko hata kama tuna-*export* bidhaa yetu iingie kwenye *international market* na ikubalike vizuri, tukifanya hivyo itakuwa tumefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho limeongelewa sana lile suala la nywele na mimi naona niongee kidogo. Tumesema kodi ya ndani ni asilimia 10 maana yake kama kuna viwanda vya ndani vinaweza vikatengeneza nywele *it is okay* tumevipa asilimia 10 lakini zile nywele zinazotoka nje tumesema asilimia 25. Mimi nimeona ni nzuri sana kwa sababu kuna nywele zingine zinatoka nje ni *fake* na hiyo ni mojawapo ya kupunguza bidhaa *fake*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona nywele za nchi nyingine dada zetu wakivaa unafikiri ni kondoo wa sufi huwezi ukamtambua vizuri tena unaweza ukaona nafuu mtu abaki na nywele zake zile za asili. Una habari wanaume wengine sisi huwa tunapenda hata nywele hizi za kawaida ambazo mtu umezaliwa nazo, huwa tunazipenda sana, sasa kwa sababu ninyi mnaona kama *fashion* mnataka zile za nje na sisi wanaume labda tunapenda kichwa chako kile cha *natural* wewe unang'ang'ania labda tupige kodi kubwa kuzuia zisiingie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo lazima tukubali siyo kila kitu kinachotoka nje ni safi, kwa nini Wazungu wasivae nywele zile tunang'ang'ania sisi huku.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Ndio. Lazima hili tukubali sisi hatuwezi kuingiza vitu ambavyo havikubaliki. Hata mimi mke wangu mwenyewe anavaa zile lakini lazima ziwe *standard* hata ukiona mwanaume unavutiwa unaona amevaa nywele nzuri lakini siyo nywele nyingine zimekuja za

ajabu ajabu unafikiri mtu kichaa sisi tuangalie tu, hiyo haitawezekana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanasema wanaume tunagharamia, ndio, mimi nakubali zile lazima tugharamie wanaume lakini tugharamie kitu kizuri. Hatuwezi kuwa tunagharamia nywele za ajabuajabu yametimkatimka tu mitaani huko na hiyo lazima tupige kodi nzuri. Bahati nzuri Serikali imeweka asilimia 25, hiyo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtanisamehe sana kwenye hilo lakini tunataka *product* inayokuja iwe nzuri ambayo na sisi wanaume tutaipenda na wanawake zetu wakivaa tunasema huyu ametoka bomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigola, sisi tunavyovaa mawigi hatuvai kwa ajili yenu jamani ni kwa ajili ya nafsi zetu wenyewe na sisi wenyewe tunafurahi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mkumbuke tu hilo wanawake hatuwavalii nyie jamani. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Rehani, Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa ya kuchangia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Wizara ya Fedha, Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri na kubwa waliyofanya na angalau awamu hii bajeti hii ni nzuri sana, huko tunakotarajia kuelekea naona sasa tuko kwenye mstari sahihi kabisa na kazi inaenda vizuri kabisa. Pia niwapongeze kwa jitihada kubwa kwenye kuondoa zile tozo angalau mmeanza kuondoa tozo mbalimbali kwenye lile suala la *blueprint*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa *productive* yaani tuwe tunazalisha bidhaa Tanzania ambapo itakuwa bidhaa zenye gharama nafuu ambazo zitaweza kushindana kwenye soko la ndani na la nje ni lazima *blueprint* ianze kufanya kazi kwa asilimia 100. Bahati mbaya *blueprint* ni taasisi mbalimbali za udhibiti pamoja na Wizara mbalimbali ambazo zinatoza ushuru, tozo, ada na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kama nilivyoshauri siku zote tungeunda *Tanzania Regulatory Authority* ambapo taasisi zote hizi zitakuwa chini ya mwamvuli mmoja. Zikiwa chini ya mwamvuli mmoja kazi yao iwe ni ku-*regulate* yaani kuboresha na kudhibiti yale ambayo wanatakiwa kufanya na wakienda kwenye viwanda, biashara mara ya kwanza wawe wanatoa onyo, elimu na watoe muda wa kufanya marekebisho lakini mara ya pili karipio na mara ya tatu ndiyo wapige faini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ni kupiga faini tu imekuwa chanzo cha mapato. Lengo siyo hilo bali ni kuhakikisha kwamba tunafanya kazi vizuri na tunadhibiti ubora na viwango vya bidhaa zetu lakini pia itasaidia sisi tuweze kuzalisha vizuri. Niombe Serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha na Wizara ya Uwekezaji mkifanya kazi kwa pamoja nina uhakika jambo hili tutafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze kwamba mmepunguza ile *presumptive tax* kutoka Sh.150,000 kwenda Sh.100,000 ina maana *compliance* itakuwa kubwa, watu wengi wataweza kulipa na watalipa kwa hiari bila kulazimishwa. Changamoto inakuja moja, sehemu zote mmepeleka ni kwenye hii *formal sector*, hawa ni wale ambao hawaweki *record*, tunawatoza tu kutokana na mauzo yao. Kwa upande wa wale ambao wanatunza rekodi na wamejisajili inawezekana biashara yao imefanana kabisa ila mmoja aliamua kuwa *formal* yaani alimua kuwa rasmi na akasajili kampuni yake kwa sababu kusajili kampuni siyo kazi kubwa, sasa hawa hamjawasaidia ina maana wengi tutaondoka huko kwenye sekta ambayo ni rasmi tukarudi kwenye sekta ambayo sio rasmi. Ingetakiwa vivutio vingi viwe

kwenye sekta rasmi, huko ndiyo mngempunguza zaidi ili watu wengi waondoke huko kwenye sekta isiyokuwa rasmi na warudi kwenye sekta rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwamba suala hili la vitambulisho, lengo la kuwa na vitambulisho hivi naamini kwamba mtaendelea kurekebisha ili zile fomu wanazojaza kabla ya kupewa vitambulisho viwe vimekamillika wengi wao tuna uhakika wataondoka huko kwenye hivi vitambulisho vya Sh.20,000 na waanze kulipa kodi stahiki ambayo wanatakiwa kulipa, yaani wengi wao bado wanafanya biashara zaidi ya shilingi milioni 4 lakini wanalipa hiyo Sh.20,000. Sasa ili kutanua wigo wa walipa kodi ni vizuri kila mtu alipe kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubw anyingine Wizara ya Fedha itusaidie kupitia *TRA* pawe na usawa katika kufanya biashara. Unakuta mtu anafanya biashara analazimishwa kuwa na mashine ya *VAT* kwa sababu ameweka rekodi yake wenzake waliomzunguka wanafanya biashara kubwa zaidi ya yeye hawako kwenye *VAT*, yule mtu mnamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo mtu anakuwa na mashine ya *EFD* wengine wanaofanya biashara zaidi ya yule wala hawana mashine ya *EFD*, hutakaa ujue nani anatakiwa kulipa kodi kiasi gani. Kwa hiyo, suala la *EFD* tuendeleo kuisitiza ili kila mmoja alipe kodi anayostahili kulipa ndiyo tutakuwa na wigo mpana wa kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwamba Kamati pia mlishauriana na Serikali na safari hii Serikali imekubali, kwenye bajeti hii mmeweza kuondoa tozo nyingi kwa viwanda vya ndani lakini mmeweza kupandisha kwa bidhaa zinazotoka nje ili kulinda viwanda vya ndani. Hongereni sana kwa jambo hilo lakini sasa muendeleo kuangalia namna ya kulea viwanda hivi. Suala siyo kodi peke yake mkijumlisha na hili suala zima la *blueprint* na mazingira mengine, nina uhakika biashara itakuwa nzuri na kwa sehemu kubwa mtapata kodi katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu, mmeweza kuondoa ile shilingi milioni 100, mtu asiandae mahesabu kwa kupitia wahasibu ambao wamesajiliwa. Tulikuwa tunaomba pia kwa wale ambao wako kwenye sekta rasmi ambao pia wanafikia tu hiyo shilingi milioni 100 au chini ya shilingi milioni 100 wao sasa sheria inawalazimisha kuwa na mhasibu kwa sababu yeye amejisajili tu kuwa rasmi pia na huyo mngemuondolea kwamba na yeye pia kama hajafikia shilingi milioni 100 asiwe anaandaa mahesabu ile pawe na usawa na kuwa kivutio cha watu kwenda kuwa sekta rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama walivyosema wenzangu wote pamoja na Kamati Serikali ingeangalia namna ya kuondoa kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji na kutengeneza mabwawa na *solar water pumps*. Kwenye jambo hilo la mitambo ya maji kuna hoja kwamba wale ambao wako kwenye VAT wao wanapata msamaha moja kwa moja kwa sababu akiingiza kama *capital goods* anapata *exemption* kwenye *VAT on deferment*. Sisi ambao tuko kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi bidhaa zetu hatuwezi kupata huo msamaha wa kodi kwa sababu bidhaa zetu baadaye hazina VAT, kwa hiyo, hatupati huo msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi tunataka kutengeneza mabwawa kwa ajili ya maji ya kunywa, umwagiliaji, mabwawa ya kufugia samaki lakini pia itapunguza mafuriko. Tija ikiwa kubwa huko kwenye kilimo, watu wakizalisha kwa wingi zaidi *spending power* ikiwa kubwa *consumption* itakuwa kubwa na mtapata *indirect tax* badala ya *direct tax*. Kwa hiyo, Serikali tunaipongeza ninyi mbaki kutekeleza miradi ile mikubwa ya kimkakati kwa mfano Stigler's Gorge, SGR lakini hii ya maji mtuachie *private sector* pia tusaidiane na Serikali kwa kuondoa baadhi ya kodi ambazo tunasema na mtaona mtapata faida kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa naomba nikumbushie kuna kodi nyingi ambazo tumeshazifuta na zimepunguzwa au kuondolewa lakini zinaendelea kutozwa

tofauti na tulivyokubaliana. Kwa mfano, kwenye bidhaa zingine za *solor* tunatoza kodi wakati imeshafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kwenye *property tax*, mwaka jana tulikubaliana kwamba *property tax* itakuwa tunalipa kwenye zile miji yote na makao makuu ya halmashauri ya miji na maeneo ambapo Waziri atatangaza kwa kushauriana na Waziri wa TAMISEMI kwenye miji midogo lakini leo hii mpaka vijijini *property tax* tunaendelea kutozwa ambapo sio utaratibu ambao tulikubaliana. Kwa hiyo, naomba na hilo muweze kuliangalia ili tuweze kulitolea tamko ili watu wasiendeleo kupata tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nashauri kwamba *cycle* yetu ya bajeti tungebadilisha kwa sababu leo hii kwa sehemu kubwa hatutaweza kubadilisha jambo lolote. Ni vizuri sisi bajeti tungekuwa tunapita kama kawaida lakini hivi vikao vya kuangalia nini kipande nini kishuke ili watu wajipange, taasisi mbalimbali zisiweke tozo au ada na kuweka kwenye bajeti zao kabla ya mwezi Novemba. Kwa hiyo, ingeanza mwezi Septemba mpaka Novemba kabla ya bajeti za kuanzia ngazi za chini kuja juu hazijaanza kuandaliwa ingekuwa inarahisisha tusingekuwa tunapata shida na huko ndiyo tungekuwa na uhakika kwamba sera ya kodi na tozo ingekuwa ya uhakika zaidi na watu wengi wangependa kupata ushauri kutokana na jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *taskforce* ingeweza kufanya kazi badala ya kukaa ofisini na kusubiri wangukuwa wanatembea ku-*insight*, watu wanapotoa mifano basi waende waonyeshwe kwamba hapa biashara inaenda hivi, kwa sababu wegwi wao wamefanya tu kazi wamesoma baada ya kumaliza shule wamepanda vyeo na wamefikia hapo walipofikia lakini hawajawahi kufanya biashara. Sasa wakiweza kwenda kwenye mazingira ya biashara, wakaona wafanyabiashara wanavyofanya kazi hapa ndiyo wataelewa kwamba kumbe hili jambo tukifanya hivi, unaweza ukakosa *direct tax* lakini *indirectly* ukapata ajira na kodi nyingine nyingi badala ya wanavyofanya kazi leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilitegemea kwamba tungekuwa kwenye vifungashio vya mbegu, *lapidary equipment* na pia bidhaa hizi za kukaushia mazao na yale makasha ya jokofu. Pia wangetanua wigo kidogo kwa mfano kwenye majokofu yawe ya maziwa, samaki na nyama kwa sababu kazi ni ileile, ile itasaidia watu wengi kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie, ni jambo moja tu namalizia. Kuna jambo hili la kuagiza kwa mtu ambaye anafanya hiyo biashara. Naona wangeondoa na wangeweka pia hata wale Mawakala wanaouza wapate msamaha wa kodi, kwa sababu leo hii mkulima yupi ana uwezo wa kuagiza vitu hivyo moja kwa moja kutoka nje ya nchi. Kwa mfano halmashauri yetu, ukitaka kununua kwa mikopo kwa vikundi, hawataweza kwa sababu Sheria ya Manunuzi haiwaruhusu kutuma fedha nje kabla hiyo bidhaa haijanzia nchini, kwa hiyo mpaka iingie nchini ina maana tayari itakuwa imeshatozwa kodi. Kwa hiyo sasa ni vizuri, walengwa ni hao watu wadogo na huu ushirika wetu, kwa hiyo naomba pale wakati wa marekebisho watuondolee kwamba ni *agent* wa hiyo bidhaa kama ni majokofu, ni *agent* wa hapa hapa Tanzania au kama...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Salum Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo na Mheshimiwa Salome Makamba atafutia.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye Mswada huu wa Fedha. Kwanza niishukuru Serikali na Wizara ya Fedha kwa wazo hili la kuweza kuondoa tozo hii ya vilainishi vya ndege (*lubricants*) ambavyo vinatumika kwenye ndege zetu mbalimbali. Hii tozo mbali tu kwamba itasaidia kuzifanya ndege zetu kuwa na huduma rahisi zaidi kuliko zinavyoweza kujihudumia sasa hivi kutokana na hii tozo. Vilevile, tutahamasisha sasa nauli za ndege katika maeneo mbalimbali kwa sababu gharama za uendeshaji

zitapungua kidogo, tuna imani vilevile hata gharama za tiketi na mambo mengine zitaweza kuangaliwa kwa jicho la huruma zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo kwa kweli limenigusa moja kwa moja, ni tozo hizi za uingizaji wa haya majokofu. Hiki ni kitu muhimu zaidi kwa sababu sasa hivi kuingiza jokofu na kuwa nalo, yaani ukiwa na *cooled storage* katika eneo lako unatakiwa ulipe; kule kwetu sisi tunalipa karibu Sh.880,000. Inawezekana umeingiza mzigo kuhifadhi, inawezekana hujaingiza mzigo, lakini *cost* hizi ni kubwa sana na kwa kweli haziko *friendly*.

Kwa hiyo suala la kusamehewa haya majokofu yakishaingizwa basi zibaki zile tozo mbalimbali ambazo zinakuwa za kuingiza mzigo na kuweka lakini zile ambazo za kuingiza ziondolewe. Hiki kwa kweli ni kitu kimoja cha faraja na kitasaidia sasa kuweza kuchechemua wawekezaji mbalimbali na sekta binafsi kuanza kuwekeza katika eneo hili. Tanzania ni moja kati ya nchi ambayo kwa kweli ina tatizo kubwa la *post-harvest*. Asilimia 40 ya mazao yetu sisi yale ambayo tunasema mazao ambayo hayawezi kustahimili kukaa kwa muda mrefu yanapotea. Aidha, wakati wa kuvunwa, wakati wa kusafirisha lakini wakati wa kuhifadhi, kwa hiyo kupata punguzo hili au kuondolewa punguzo hili itawafanya watu mbalimbali wawekeze hivi vitu katika maeneo yetu ya mashamba na hivyo sasa kuwafanya wakulima kuweza kuhifadhi mazao yao na kupunguza ile *post harvest loss* kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linaweza kuchachamua uchumi ni suala zima hili la vifaa vya *plastic*. Tunachokihitaji kwamba tuweze kuwa na viwanda ambavyo vitaweza kutengeneza hapa vifaa vya *plastic* hasa vinavyohusu kilimo. Kwa mfano *drip irrigation kits*, lakini *pipe* hizi ambazo tunatumia kufanya *irrigation* katika mashamba yetu. Utamaduni wa sasa hivi au mfumo wa sasa hivi wa umwagiliaji maji unategemea *pipe irrigation*. *Plastic tools* ndivyo vitu vinavyotumika kwa ajili ya kuweza kufanyia hiyo *installment* ya *irrigation* katika mashamba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunachokihitaji kwamba, viwepo viwanda ambavyo vitaweza kutengeneza hizi bidhaa hapa nchini, mimi sina tatizo na bidhaa ambazo zinatoka nje na kutozwa kiwango kikubwa. Kwa mfano sasa hivi *balton kit* moja ya *drip irrigation* katika eka moja inagharimu karibu 2,400,000. Kitu ambacho wakulima wengi wanashindwa kuweze ku-*afford* na kuweza kununua na kuweza kutumia katika mashamba yao. Hali ya hewa tunaona tatizo tulilokuwa nalo hakuna uhakika wa mvua, lakini utakapopatikana unafuu huu wakulima wengi wataanza kulima kwa kutumia mipira hii ya maji, kwa hiyo hicho kitu kitaweza kusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tunaliona kwamba litaweza kusaidia ni vifaa vya ukaushaji. Tuna tatizo Tanzania ukaushaji tunatumia jua na wengine wanatumia kuni kwa kiasi kikubwa sana hasa ndugu zangu wa kule Kanda ya Pwani na kwenye maziwa wanaovua dagaa. Ndiyo maana dagaa zetu kwa kiasi fulani nyingine zinakosa ule ubora wa *food process* inavyotakiwa ifanyike hasa kuzianika mpaka zikawa katika; wenyewe wanasema ziwe zimenyooka kama alifu, haziwezi kupatikana katika hali hiyo kutokana na *methods* ambazo tunatumia kwenye uanikaji.

Kwa hiyo tutakapopata hili punguzo watu wengi au wawekezaji wengi wataleta vile vifaa, watakuwa wanaanika kwa kukodisha hivi vifaa na kuweza kuipata hii bidhaa ambayo tutaweza kuisafirisha nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tutaweza kusaidia ni vifaa kama vya *green house*, vitakavyoletwa hapa na kuondolewa hizi tozo itahamasisha kilimo hiki na watu wengi watalima kwa uhakika zaidi. Leo *green house kit* moja inauzwa kwa zaidi ya 8,000,000 ile wanaita 20 x 10. Tutakapopata punguzo hili itashuka na hivyo kipato cha mkulima kitapanda kwa sababu *green house* moja ukiitunza inakuletea 15,000,000. Kwa hiyo tukipata punguzo hili una uhakika wa kutengeneza 20,000,000 na una uhakika wa kuhakikisha kwamba mkulima umemkomboa na umemwongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naliona kwamba litaweza kusaidia ni suala zima la huu ukaushaji kuweza kutengeneza viwanda vya ku-*grind*. Tunahitaji sana *tomato powder* ndani ya nchi, *demand* ni kubwa lakini hakuna viwanda ambavyo vinajitokeza kutengeneza *tomato powder*. Wenzetu Ulaya nchi kama Israel na nyinginezo *tomato* haiuzwi, hatuli *tomato fresh* kama tunavyokula sisi hapa. Tunakula *powder* ambayo unatia tu kama bizari kama mchuzi biashara imekwisha. Sasa hiyo biashara itaweza kuwa chachu sasa ya viwanda vidogo vidogo katika maeneo yetu tukipata hii tozo kuondolewa na kuhamasisha uchumi na kilimo kwa upande wa nchi yetu. Tutaweza kukausha *tomato*, tutaweza kukausha vitunguu, tutaweza kukausha vitunguu maji na bidhaa nyinginezo mbalimbali ambazo zipo katika maeneo yetu. Hata tangawizi tutaweza kuuza, tangawizi ya *powder* ambayo kwa kiasi kikubwa sasa hivi sisi tunaingiziwa ndani ya nchi kutoka nchi nyingine.

Kwa hiyo chachu ya viwanda vidogo vidogo katika maeneo yetu ya uzalishaji itakuwa kubwa zaidi kama hizi tozo zitaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, niishukuru Serikali kwa kulikubali wazo hili. Niombe kwamba sasa sekta binafsi uwanja na mlango umefunguliwa wazi, tuwekeze katika hilo eneo na tutaifanya Tanzania kweli kuwa ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Taska Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Khadija Nassir ajiandae.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia *Finance Bill*. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mpango na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya siku zote hizi kuhakikisha kwamba hii *bill* inakuja vizuri na Watanzania waweze kupata nafuu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia ushuru wa bidhaa. Napenda sana kuipongeza Serikali kwa kuondoa ushuru wa bidhaa za mvinyo wa mazao yanayosindikwa nchini Tanzania. Hii itatusaidia sana kuwakaribisha wawekezaji kuja kufungua viwanda nchini kwetu Tanzania na ukiangalia kwamba tunayo matunda mengi sana nchini kwetu Tanzania. Matunda kama maembe, mapapai, mapera, mananasi, machungwa ambayo yanalimwa kwa wingi Tanzania lakini tulikuwa tunakosa wawekezaji kuja kufungua viwanda nchini kwetu kwa sababu ya kodi ambayo ilikuwa imewekwa. Kwa kuviondolea kodi viwanda hivi vitakavyofunguliwa nchini kwetu, itatusaidia sana kupata wawekezaji wengi na ukiangalia kwamba nchi yetu ni ya amani, kila mtu yuko huru, mtu yeyote anaweza akaingia hapa akafungua kiwanda chake, akaajiri watu haina masharti ambayo yanamkatisha tama mtu kufungua kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo, amani yenyewe ninayoisema ni kwamba niitolee mfano kidogo tu siwezi kuitaja nchi ninayotaka kuisema. Kuna nchi nyingine huwezi kutembea baada ya saa nne, ukitembea mita 100 unaulizwa kipande cha kodi. Kwa hiyo amani hii tuliyonayo ni nzuri kwa wawekezaji na kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa hiyo nipongeze sana hilo la kuondoa ushuru wa bidhaa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulipongeza na kulizungumza ni kuondoa ushuru wa kodi ya mapato katika *Income Tax Act Section 9*, imeondoa ule usumbufu wa kufanya mahesabu kwa wafanyabiashara wa milioni 20. Ukiangalia kwa dunia ya sasa mtaji wa milioni 20 kwa wafanyabiashara wakubwa wakubwa ilikuwa ni mtaji mdogo lakini ulikuwa na usumbufu mkubwa sana wa kumtafuta mhasibu aje kukufanyia hesabu halafu akishatoa zile hesabu ndiyo uende ukakabidhiwe mapato yako. Zaidi ya hapo ilikuwa inaongeza gharama kwa sababu yule mtu wa kuja kukufanyia hesabu inabidi umlipe tena fedha ili aje afanye hesabu yako. Sasa kwa kuweka kiwango hiki cha kutoka milioni 20 mpaka milioni 100, kwa

kweli naipongeza sana Serikali, hapa imepiga hatua na imewafanyia vizuri wafanyabiashara wetu nchini Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu haya marekebisho yote pamoja na ile ya wafanyabiashara wa chini ya milioni 4,000,000 kupunguziwa kodi. Kwa pamoja niombe haya marekebisho yaandikwe vizuri na yawekwe kwenye mbao za matangazo ikiwezekana kwenye halmashauri ili wananchi waweze kusoma kwa sababu yakiachwa hivi hivi bado kuna watumishi ambao siyo waaminifu watawazungukia tena wale wafanyabiashara na kuwadai kodi. Kwa sababu ukiangalia pia kuna kodi nyingi ambazo Serikali ilizifuta hata mwaka jana, lakini bado wale watumishi ambao siyo waaminifu huwa wanarudi kwa mgongo wa nyuma kuwadai wafanyabiashara kodi. Niombe TRA iandae zile kodi zote ambazo zimefutwa na Serikali zibandikwe kwenye matangazo ili Watanzania wote wazione. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuleta vile vitambulisho vya 20,000. Ila naomba kutoa angalizo kwenye hivi vitambulisho vya 20,000, niombe Serikali iweze kuweka picha ya mtumia kitambulisho ili mtu aeleweke ni nani anayefanya biashara katika lile eneo. Kwa sababu kwa kuiacha wazi mimi leo naweza nikaamua nikanunua kile kitambulisho nikakaa Kisasa nikauza biashara yangu na kesho nikahama nikaenda Majengo nikauza biashara yangu kwa sababu kile kitambulisho hakina picha. Labda kama kingeweza kuwekewa kwamba na eneo la makazi ni wapi, lakini *idea* ni nzuri kwa sababu ukiangali wananchi walikuwa wanateseka sana kwa kupitia hawa watoza ushuru ambao walikuwa wanadai mia mbili, mia mbili kila siku, walikuwa wanawanyanyasa wakiwakuta wanawamwagi vitu vyao, wanawaambia huruhusiwi kuuza mpaka umelipa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuleta hiki kitambulisho ina maana mfanyabiashara atakuwa huru kuuza biashara yake mahali popote, ili mradi tu hiki kitambulisho kiboreshwe

na pia utoaji wake yule mwananchi wa kawaida unaweza ukaiona 20,000 ni ndogo, lakini kwa mfanyabiashara wa kawaida kama mama anayeua njugu au anayeua vitu vyake vidogo vidogo kama mchicha kupata hiyo 20,000 kununua kile kitambulisho inakuwa ni shida. Kwa hiyo utaratibu uwekwe kama vile mtu anaweza akalipa kidogo kidogo labda kwa awamu nne elfu tano tano mpaka anatimiza ile 20,000 itakuwa imemsaidia zaidi huyu mama wa chini anayeua karanga na huyu kijana wa chini ambaye anatafuta maisha labda na yeye pia kwa kuuza njugu, kwa kuuza mchicha, kwa kuuza matunda kwa kitu chochote ili aweze kuweka ile fedha yake. Akiuza aweke kidogo kidogo ikifika 5,000 alipe mpaka atimize hicho kitambulisho cha 20,000, ukiiacha kuitoa 20,000 kwa mara moja wengine kama huko tunakotoka kuweka 20,000 inakuwa shida kidogo. Niiombe tu Serikali ijaribu kuangalia hapo jinsi ya kuwasaidia hao wafanyabiashara wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala lingine, ni kodi ambazo zimepunguzwa kama za visima vya maji. Niipongeze Serikali ni nzuri kwa sababu zilikuwa zinasaidia kwenye maeneo ambayo maji hayatoki, watu walikuwa wanachimba vile visima wanawasaidia wananchi. Ukiangalia maeneo mengi nchini kwetu Tanzania hayana maji, kwa hiyo walikuwa wanawasaidia wananchi wa eneo lile kupata maji. Sasa kwa kuwawekea kodi tulikuwa kama vile wanataka kuvunjwa moyo wa kutaka kusaidia wananchi wa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sehemu nyingi wananchi bado wanatumia maji ya visima na bado maji ya bomba hayajaenea kwenye vijiji vyetu, ndiyo kwanza tunahangaika kutafuta maji ya bomba. Tumeanzisha miradi ambayo tunataka tuchimbe maji ya bomba na Watanzania wote waweze kutumia maji ya bomba. Kwa kifupi ni kwamba maji ya bomba hayajafika vijijini, kwa hiyo kwa kuondoa hii kodi, hii tozo ya kwenye visima vya maji ni sahihi kabisa. Naipongeza Serikali itasaidia sana, itawafanya wafanyabiashara wengine wenye uwezo waweze kuchimba maji na kuwasaidia wananchi wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningeweza kulizungumzia, nawashangaa sana wanaume wanasimama humu ndani wanachangia mambo ya nywele, mimi nafikiri wangechangia mambo yanayowahusu wao. Hivi vitu ni *personal issue* za wanawake, mwanamke anahitaji yeye mwenyewe anajiangalia leo afanye nini; asuke nywele ya rasta, aweke hilo wigi, anyoe kipara au afanyeje. Sasa mwanaume anasimama humu anasema mimi nampenda mke wangu akisuka kipilipili, *so what!* Kila mtu ana *interest* yake, kuna mwanaume mwingine anampenda mwanamke aliyenyoa kipara, mwanaume mwingine anampenda mwanamke aliyevaa wigi, mwingine anampenda mwanamke...

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska kuna taarifa huku, Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, kwa kiasi kikubwa hayo mawigi tunanunua sisi kwa ajili yao.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska una dakika moja malizia mchango wako.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mheshimiwa Selasini siwezi kuipokea kwa sababu akinamama sasa hivi wameamka wanashika uchumi. Akinamama wanafanya biashara za kila aina, wanauza maduka, wanapika mama ntilie, wana hoteli, wanaendesha mpaka magari na bajaji. Kwa hiyo, suala la kuwaambia kwamba wanaume wanawanunulia nywele si sahihi, si sahihi kabisa, taarifa yake hiyo siipokei. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akinababa wanapenda sana kutelekeza watoto, hizo nywele utaweza kununua!

Tukihesabu watoto wa mitaani wanaotembea ni wale watoto ambao wamekimbiwa na baba zao, sembuse hiyo nywele kununua.

MBUNGE FULANI: Sema!

MHE. TASKA R. MBOGO: Wanaume huwa hawawezi kumnunulia mwanamke nguo wala kitu, mwanamke huwa anajiremba mwenyewe. Kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba akinamama wasife moyo, wanaovaa wigi wavae wigi, wanaotaka kusuka wasuke, wanaotaka kusuka rasta wasuke na hizo nywele hata kama zimepanda kodi sisi tutazinunua tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Taska hao wanaume wanaochangia ni kwa sababu wanatuunga mkono sisi akinamama, si wanajua sisi ni jeshi kubwa, lazima watuunge mkono; kwa hiyo wanatuunga mkono akinamama, tuko vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Salome Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Mussa Mbarouk ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi naomba nisiendeleze mjadala wa mawigi, wanawake wenzangu wamesema sana na nawaunga mkono japo mimi sisuki mawigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichangie kidogo kwenye *Finance Bill* na nimkumbushe tu Naibu Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha kwamba mara nyingi mapendekezo mnayoyaleta ya kuongeza kodi au kuboresha mazingira ya kodi tangu nimeingia Bunge hili yamekuwa ni mapendekezo ambayo yana mtazamo wa muda mfupi. Pia, pamoja na kazi kubwa ninayoamini mnaifanya nyuma ya pazia, mnajipa muda mfupi kujitathmini uwezo wenu wa

kutekeleza yale ambayo mmeyapendekeza. Hili limeonekana katika uondoaji wa VAT katika taulo za kike na katika mapendekezo mliyoyaleta mwaka jana na mwaka juzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nishauri tu kwamba Wizara ya Fedha inapoleta mapendekezo ya kodi kwanza ilete mapendekezo ambayo tuna uhakika ni endelevu lakini pili ijipe muda wa kutosha wa kujaribu mapendekezo yao na siyo mwaka mmoja kama wanavyofanya kwa sababu mwisho wa siku haileti tija na naamini rasilimali nyingi zinatumika, rasilimali fedha, muda na *research* zinafanyika kuweza kutuletea hapa mapendekezo haya, naamini hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niongezee kwamba tunayo changamoto kubwa na Waziri wa Fedha amekiri kwenye suala la vitambulisho vya wajasiriamali. Hili tulilisema tangu mwanzo wakati linaanzishwa na kwa bahati mbaya nafikiri sasa ni wakati muafaka Bunge litafute namna ya kufanya *lobbying* ya kuleta hoja nzito zenye maslahi makubwa kwa wananchi ndani ya jengo hili kwa sababu hoja inapoonekana imetoka upande wetu hata iwe nzuri kiasi gani watu wanaona ni bora tuipinge halafu tutakubaliana nao baadaye. Haya tutayaona hata kesho kwenye Muswada wa mabadiliko madogo ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha amekiri kwamba mapungufu makubwa yako kwenye vitambulisho vya wajasiriamali na vitambulisho hivi havina jina, picha, saina ya mtoaji, haeleweki hizo pesa zinazokusanywa zinaenda wapi yaani hamna mfumo maalum na wala hatujui ni namna gani tutazifanyia *audit* pesa hizi.

Kwa hiyo, pamoja na Serikali kukiri kwamba kulikuwa na makosa fulani fulani wakati wa kutekeleza agizo hili la Mheshimiwa Rais, naomba zoezi la vitambulisho vya wajasiriamali lisitishwe kwa muda mpaka pale mtakapopata namna bora ya kukusanya mapato hayo maana tulishauri kwamba lisifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikufahamishe tu kwamba kitambulisho cha mjasiriamali kina bei kubwa kuliko kitambulisho cha Utaifa. Kitambulisho cha Utaifa kinatolewa bure, kitambulisho cha mjasiriamali unalipiwa Sh.20,000. Ukipewa kitambulisho cha Taifa unakaa nacho milele, ni cha kwako hakuna ku-renew lakini cha mjasirimali kinakaa mwaka mmoja. Kwa hiyo, niseme vitambulisho hivi vya ujasirimali iko haja kubwa...

T A A R I F A

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, kuna taarifa, Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hivi vitambulisho vina mapungufu mengi havina picha, jina kwa sababu mchakato wake haukuanzia Bungeni, ulianzia Ikulu na Wakuu wa Mikoa na Wilaya waliitwa kule. Kwa hiyo, vingeanzia Bungeni tungeshauri viwe na picha na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni taarifa tu ambayo nataka nimpe kwamba siku nyingine wakumbuke kwamba Bunge liko na linaweza likashauri namna bora ya kuweza kufanya mambo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, endelea na mchango wako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru Mheshimiwa Haonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza kuhusu vitambulisho vya ujasiriamali na kitu ambacho napenda kushauri kwenye Bunge lako Tukufu ni kwamba visitishwe na ikibidi vikirudi vitolewe bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu Sheria ya Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki...

T A A R I F A

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome, kuna Taarifa nyingine, Mheshimiwa Maulid Mtulia

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumheshimu sana mchangiaji lakini nilikuwa nataka kumpa taarifa ya vitambulisho vya wajasiriamali vilikuja vikiwa ni mbadala wa kodi kubwa ambayo wajasiriamali walikuwa wakilipishwa, shilingi 500 kila siku. Kwa kupata kitambulisho kile wanalipa chini ya shilingi 50 kwa siku. Kusitisha kitambulisho kile maana yake ni kuwarejesha wajasiriamali kwenda kulipa shilingi 500 kwa siku kwa mwaka shilingi 180,000. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, namheshimu sana Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni lakini nimwambie kwamba Waziri wa Fedha amekiri vitambulisho vina mapungufu, hata wewe ni nani unataka kupotosha Bunge hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya wajasiriamali ushauri wangu ni kwamba vina mapungufu makubwa na Serikali imekiri na naishauri Serikali isitishae zoezi la vitambulisho hivi mpaka taharuki ya utekelezaji wa vitambulisho itakapotatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleee na Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mbunge anayeendelea kuchangia, anaonesha hisia za kutetea wajasiriamali lakini nataka nimpe taarifa hata madaktari wanapokuwa hospitalini, wanapokutana na *challenge* kwa mgonjwa huwa hawaitishi huduma ya mgonjwa bali wanamuweka pembeni halafu wanaanza kutafuta *solution*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati tunatatua changamoto hizi, vitambulisho hivi vitaendelea kuwasaidia kwa sababu kabla ya vitambulisho hivi waliumia. Kwa hivyo, nilitaka tu nimpe taarifa mchangiaji, vitambulisho hivi akiri visisitishwe kwa sababu mwanzo kulikuwa na tatizo kubwa kuliko hili la hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, malizia mchango wako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, huyo hakuwepo Bungeni tangu tumeanza Bunge la bajeti, kwa hiyo, alikuwa na hamu ya kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria ya ushuru wa nondo, Serikali katika Muswada iliyoleta wanasema kwamba wameongeza bei ya ushuru kwa nondo zinazotoka nje ya nchi. Mimi nakubaliana na Serikali na *measures* wanazochukua. Kitu ambacho napenda kuishauri Serikali, watengeneze mazingira mazuri ya uzalishaji wa malighafi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tunashauri kuhusu *SGR* na mradi wa Rufiji walisema kwamba kile chuma hakifai basi kitafaa angalau kwenye ndondo tujenge Mheshimiwa Waziri. Tunakuomba utusaidie ku-*push* mradi wa Mchuchuma na Liganga kwa sababu tutapata chuma cha kutosha ambacho kitatusaidia kushindana na vyuma vinavyotoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mabomba ya plastiki. Haya nayo pia yamepandishwa kodi. Wewe ni shahidi, hapa Bungeni likiulizwa swali linalohusu maji safi na salama, Wabunge wote wanasimama na wanataka kujua hatma ya maji. Leo hatujawafikishia wananchi maji safi na salama na yanayotumika ni haya mabomba, hivi Serikali haioni umuhimu wa kuondoa kodi kabisa kwenye mabomba haya ili wananchi wapate maji safi na salama? Mimi sioni sababu. Juzi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha wakati anahitimisha alisema kwamba kuna bidhaa ambayo ni ya msingi kwa wananchi kwa hiyo tusiwaadhibu kwa sababu ni lazima watanunua, bidhaa hii ipatikane ili watu wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa haraka kwenye *incentive* katika taulo za kike. Mimi nakubaliana na Serikali wamefanya utafiti wao wanasema kwamba walaji wa mwisho bei ya taulo haijapungua na wanasema kwamba wametengeneza mazingira ya kuleta viwanda. Tunayo miaka miwili ambayo wananchi na watoto wetu utu wao utadhalilika kwa sababu ya kushindwa kujitiri ili waweze kuhudhuria masomo. Serikali iwe sikivu iwasaidie tupate taulo hizi angalau bure kwa hiyo miaka miwili mpaka pale watakapoamua kwamba viwanda hivi vianze kufanya kazi na kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Khadija Nassir ajiandae.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na maoni ya Kamati ya Bajeti. Maoni ya Kamati ya Bajeti katika ukurasa wa 19, Mkoa wetu wa Tanga, Halmashauri sita kati ya 11 zina kilimo cha mkonge. Kwa maelezo yaliyopo pale ambayo wenzetu wa Kamati ya Bajeti wamesaidia kuishauri Serikali, naiomba Serikali yangu Tukufu iweze kuyakubali mapendekezo haya ili kusudi Mkoa wa Tanga na wenyewe uweze kujiinua kwenye uchumi pamoja na kupata ushuru wa mazao badala ya *service levy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sisi Mkoa wa Tanga haya mashamba tunachukua *service levy* tu kwa ushuru wa huduma lakini mkonge hauna tofauti na pamba, koroshu, kahawa na tumbaku. Kwa nini sisi Mkoa wa Tanga na mikoa mingine ambayo imepanda mkonge kama Pwani, Kilimanjaro, Morogoro na sisi tusingizwe katika zao hili kupata ushuru wa mazao. Tukipata ushuru wa mazao maana yake tutaongeza kipato na kwenye hii bajeti yetu kuu mapato ya Serikali yataongezeka kuliko hivi sasa.

Naiomba sana Serikali, najua kwa vyovyote vile kwa sasa hivi kwa bajeti hii inaweza isiwezekane lakini niombe kwa maana ya mwakani basi mfikirie hili suala la mkonge kwa mikoa ambayo ina mashamba ya mkonge na sisi tuingie katika mazao yale ambayo yanaweza yakatoza ushuru wa mazao badala ya *service levy* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimesimama kwa ajili ya hili tu. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Nassir, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kutujalia afya njema na kupata nafasi ya kuzungumzia Muswada huu ambao tunaujadili sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala zima la taulo za kike. Kwa hesabu za haraka haraka kutokana na kutokumudu gharama za ununuzi wa taulo za kike, mtoto wa kike hukosa masomo kwa mwezi kati ya siku tatu mpaka sita na ukipiga mahesabu kwa mwaka anaweza kukosa kati ya siku 36 au siku 72 kwa mwaka. Sasa hatumtendei haki kwa sababu tu ya kukosa taulo za kike kwa vile anapokuwa katika mazingira hayo anakuwa hayuko huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kusema kwamba eti baada ya kupewa punguzo la VAT kwa asilimia 25 walionufaika ni wafanyabiashara, hili sikubaliani nalo. Kama vile tunavyopiga marufuku bidhaa nyingine, kwa mfano, tulivyopiga marufuku mifuko ya *plastic*, tumeweza, Serikali yetu imejitahidi imepunguza mpaka matatizo ya dawa za kulevya, tumeweza, inakuwaje wafanyabiashara watushinde baada ya kuwasamehe asilimia 25 wawe wanafaidika zaidi kuliko Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu ushauri kwamba kwa kuwa taulo hizi zinatumiwa na watoto wetu, dada zetu, shangazi zetu, mama zetu na wake zetu ikibidi kodi hii iendelee kuondolewa. Mwaka jana wakati nikichangia nilitoa mfano, Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya alisaini sheria kwamba wanafunzi wote nchini Kenya wapatiwe taulo za kike bure na Serikali inafidia. Sasa ukiitazama Kenya haina *resource* nyingi kama sisi Tanzania, sisi tuna Mlima Kilimajaro, mbuga za wanyama nyingi kuliko Kenya, madini ya aina zote, gesi, tuna dhahabu, almasi, kwa nini tushindwe na Kenya? Nashauri Serikali yetu itoe taulo za kike bure kwa watoto wa kike ili wapate uhuru wa kujinafasi katika masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua na wewe ni mwanamke hili linakuhusu, huoni ambavyo umepata elimu wewe mpaka leo umekuwa Naibu Spika na inshaallah Mwenyezi Mungu akijaalia pengine kipindi kijacho utakuwa Spika, basi na wewe utusaidie kupiga debe tuhakikishe

kwamba watoto wa kike wanapatiwa taulo za kike bure.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima hili la kupata *tax holiday* kwa wafanyabiashara. Kilio hiki kwa kweli Wabunge tumekisemea sana lakini tunashukuru kwamba Serikali imeweza sasa kutoa ile *tax holiday* ya miezi sita kwamba mfanyabiashara wa Tanzania naye awe kama mfanyabiashara wa Kenya, Burundi au Uganda apate kujiweka sawa kwenye biashara yake, ajihakikishie biashara yake inakwendaje kuangalia faida na hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshauri, mara nyingi tunavyopitisha mambo hapa ukifika kule chini unaambiwa Waraka bado haujafika. Kwa mfano, suala la msamaha wa kodi ya vyombo vya usafiri tulipitisha hapa tukaipeleka kwenye mafuta lakini pia suala la kufanya *transfer* kwenye vyombo hivi vya usafiri kukawa kuna tatizo unaambiwa Waraka haujapelekwa chini. Naiomba Wizara na Serikali kwa ujumla, tunapopitisha mambo hapa basi Waraka haraka upelekwe kule kwa wananchi kwa sababu jambo likiwa la kumnufaisha mwananchi Waraka unachelewa lakini jambo likiwa la kumbana mwananchi likitamkwa tu hapa Bungeni, kesho asubuhi linaanza kufanyiwa kazi. Sasa tunaomba hizi tozo na kodi mbalimbali ambazo zinasamehewa basi Waraka ushuke kule chini ili wananchi wetu wasiweze kusumbuliwa.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la vitambulisho hivi vya wajasiriamali. Sasa hivi tunaona jinsi Wabunge wanavyopiga kelele hapa lakini sasa ni kweli kwamba vimepitia kwa Wakuu wa Mikoa na ma-DC, imekuwa mpaka bodaboda naye pamoja na kwamba analipia *license*, *TRA*, *sticker* kwenye Halmashauri na malipo mengine kadha wa kadha lakini bado anaongezewa mzigo sasa wa kulipa kitambulisho kile cha ujasiriamali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu, kwanza havina ubora kwa sababu hakina picha,

hakielezi aina ya biashara lakini bodaboda na yeye ni dereva kama alivyo dereva *tax* kwa sababu ana *license*, kama alivyo dereva wa basi na kama alivyo dereva wa gari ya *private*. Sasa kama tunamshushia Sh.20,000 ya kitambulisho cha ujasiriamali bodaboda maana yake sasa madereva wa Wabunge nao watalipa Sh.20,000 ya kitambulisho, madereva wa mabasi watalipa kitambulisho na madereva wa *tax* watalipa. Mimi naona bodaboda tuwaache waendeleo kulipa *SUMATRA, TRA, sticker* katika Halmashauri na walipie vile vituo vyao vya bodaboda ule ujira ambao wamepata kulipa katika kila kituo cha bodaboda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bodaboda huyu tuumbuke pikipiki sio ya kwake, yeye ameajiriwa. Kwanza apeleke hesabu kwa tajiri halafu apate fedha za kujihudumia yeye na familia yake, kwa kweli tunawatwisha mzigo mkubwa bodaboda. Mimi naomba tuliondoe suala hili kwa bodaboda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye suala zima hili za kuongeza kodi katika vifaa vya ujenzi. Nimeona kwenye kitabu kwamba ipo katika *East African Common Tariff* lakini tujjulize sisi Watanzania kwanza ni soko kubwa sisi la bidhaa za *plastic* za Kenya, pili tunapoongeza kodi kwenye bati, nondo, fito za plastiki, mabomba ya plastiki, tujue tunaongeza gharama za ujenzi. Mtu wa kawaida nyumba anaweza akajenga kwa miaka saba au nane, leo tena badala ya kumshushia gharama za ujenzi, tunamuongezea. Mimi naona kwenye hili wale wawakilishi wetu, Waziri wa Fedha mnapokutana katika vile vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki mjaribu kututetea sisi Watanzania ili na sisi tupate manufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaloshauri katika hili, hizi bidhaa pamoja na kuongezewa kodi, mimi naomba ziondolewe, lakini zitakapoondolewa kodi pia pawe na nembo maalum ya ubora kwa sababu wananchi wa kawaida labda wa vijijini hawezi kujua kwamba nondo hii inatoka Kenya au hii imezalishwa kwenye kiwanda cha ndani. Hawezi kujua plastiki hii inatoka Kenya au plastiki hii inatoka

kwenye viwanda vya ndani. Mimi nafikiri ni vyema tuhakikishe vinakuwa na nembo ya ubora ambayo itasaidia sasa wafanyabiashara wale wasije wakatufanya kama kwenye taulo za kike...

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk, kuna taarifa.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu nilitaka nimpe taarifa msemaji aliyekuwa akichangia, Wabunge wengi wa upande wake ikiwemo na yeye ni miongoni mwa Wabunge walioikataa bajeti ya shilingi trilioni 33 isipite.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Twendeni taratibu tu, daktari akichelewa kazini na akakutibu, twendeni taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sisi tulijipanga na bajeti yetu ya shilingi trilioni 33 na wao wakaikataa, sasa kile anachokichangia tuondoe ushuru kwenye maeneo mbalimbali angetueleza mbadala wake utakuwa ni nini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk, malizia mchango wako.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipokei taarifa yake. Kwanza huyu ni mtoro, anazungumza kusudi asije akatajwa kama alivyotajwa mara ya kwanza kwamba ni mtoro. *(Makofi)*

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Kuhusu utaratibu

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea, lingine, kwenye mitambo ya kuchimba visima, naamini unajua kwamba kama unavyosema kwamba likizungumzwa suala la maji....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk kuna kanuni inavunjwa.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni taratibu za kawaida unapopewa taarifa *either* uikubali ama uikatae, anakubali taarifa yangu ama anakataa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendeleo kusema kwamba....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk. naomba ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge huwa nawakumbusha mara kadhaa, Kanuni ya 68(8), unapotoa taarifa, ni kwamba anayezungumza amekuwa amezungumza jambo ambalo wewe unataka kuongezea hapo.

Kwa hiyo, hoja ya mimi kuuliza kama taarifa mtu anaipokea ama haipokei, ni mpaka iwe taarifa, kwa muktadha wa kanuni zetu na tusome, kanuni ya 68(8). Mheshimiwa Mbarouk malizia muda wako.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililopenda kuzungumzia ni kwenye mitambo ya kuchimba visima, nashukuru kwamba, hili nalo tumelizungumza, lakini niombe kwamba, kodi nayo ipunguzwe kwenye mitambo ya kuchimba visima kwa sababu, watu wengi au Wabunge wengi linapozungumzwa suala la maji hapa wanakuwa wanachangia sana, kila mmoja analalamika kwamba, maji kwake hakuna, lakini ikiondolewa kodi kwenye mitambo hii ya kuchimba visima, wachimbaji watapunguza gharama za uchimbaji na vilevile wataisaidia Serikali katika kumtua mwanamke ndoo

kichwani. Kwa hiyo, naomba suala hili nalo liangaliwe, ili watu hawa waweze kusamehewa kodi katika mitambo ya visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, nimalizie sekta ya uvuvi, kwenye suala la uvuvi, tumeona kwamba, baadhi ya wavuvi ni sehemu ya mapato ya nchi yetu, lakini kwa mfano, baada ya kuchomwa nyavu, lakini wapo wavuvi wengine mashine zao zilichukuliwa kama *bond* kwao. Sasa niombe, wale wavuvi waliokuwa wamechukuliwa mashine zao kwa mfano kule Tanga, warudishiwe kusudi waendeleo na shughuli za uvuvi ili waweze kulipa kodi na kuchangia pato la taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho....

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana muda umekwisha Mheshimiwa, shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Khadija Nassir, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa nipende kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu, lakini pia nipende kuongea machache tu kabla sijatoa mapendekezo yangu katika hoja hii ambayo tuko nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka uliopita katika kipindi kama hiki cha kujadili mapendekezo ya maboresho ya sheria ya mbalimbali, mimi nikiwemo na wenzangu tulisimama kuongelea issue ya *double taxation* kwenye umeme ambao unakwenda Zanzibar na hili ndilo ambalo linanipa faraja leo kuweza kusimama tena, kwa sababu baada ya kupiga kelele nyingi Serikali yetu imeweza kusikia na sasa hivi suala hilo limekwisha. Kwa hiyo, nipende

kuipongeza Serikali kwa hilo, lakini pia nipende kutoa mapendekezo machache tu na sitatumia muda mrefu kwenye ongezeko la thamani ya kodi kwa bidhaa ambazo zinakwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba, kipato cha Mzanzibari wa chini kabisa ni kidogo uki-*compare* na kipato cha Mtanzania bara wa kawaida na kwa hili linapelekea sana sana kufanya maisha ya wazanzibari kuwa magumu. Tumekuwa na tatizo la *double taxation* kwa bidhaa ambazo zinakwenda Zanzibar. Hili limepelekea kuwa na mzunguko finyu sana wa biashara kule Zanzibar na ukizingatia kwamba Zanzibar ni kisiwa, uchumi wake tunategemea sana kwenye mzunguko wa biashara lakini pia kwenye masuala la utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafahamu, mapendekezo yote ambayo sasa tutayapitisha, yatakwenda kuathiri makusanyo ya kodi ambayo tunayapata kwa sasa hivi, lakini tusiangalie tu ukusanyaji wa kodi, tuangalie namna gani ambavyo tutaweza kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi wa kawaida wa Tanzania visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu, hata sasa nikipendekeza kwamba, wale wafanyabiashara ambao hawana uwezo wa kununua bidhaa kutoka kwenye viwanda, hata nikipendekeza waweze kupewa *exemption*, tutatoa mwanya kwa wale wafanyabiashara ambao siyo waaminifu kuweza kukwepa kodi. Kwa hiyo, sitaki kwenda huko, lakini nina mapendekezo machache tu kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni huko nyuma, zaidi ya miaka 25 tulikuwa na utaratibu wa *tax refund* na hili lilikuwa linakwenda vizuri sana, japokuwa lilikuwa na changamoto ndogondogo kama vile fedha kurudi kwa wakati na mambo mengine. Sasa napendekeza kwamba, utaratibu ule urudi, lakini tuufanyie maboresho yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuona namna ya kuweza kufungua akaunti, *separate* ya kuweza kuingiza hizi

fedha ili zitakapotakiwa sasa kurudi kusiwe na mkanganyiko au kusitokee changamoto yoyote. Kwa kufanya hili tutaweza kuwawezesha wale wafanyabiashara kule Zanzibar sasa kuweza kutanua wigo, lakini pia kuweza kuwasaidia wananchi wa kawaida kupunguza ule ugumu wa maisha ambao upo kule sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kupendekeza, kama hilo pia tutaona, au Serikali itaona kuwa halifai kwa sasa hivi, tuone basi namna ambavyo tunaweza kufuta ongezeko hili ili sasa visiwani kule, biashara ziweze kushamiri, lakini pia maisha yaweze kuwa marahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi langu kwenye hili lilikuwa ni hilo, naamini kwamba Serikali italifanyia kazi na sisi tuweze kuona manufaa, lakini pia tuweze kuona matunda ya biashara kwenye nchi yetu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Chiristopher Chiza ajiandae.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hii hoja muhimu kwa ajili ya kodi zetu. Kwanza ningeanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Fedha. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana, lakini pia nipeleke na pongezi kwa Kamati yangu ya Bajeti nafikiri nao wamefanya kazi kubwa ambayo inawezesha hata huu Muswada ukawa mzuri kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kabisa kulikuwa na hoja nyingi za wadau na hoja nyingi za Kamati ya Bajeti, lakini Waziri ameweza ku-*accommodate* hoja zote hizo kwa kiasi kikubwa, labda ni mambo machache tu ambayo yanahitaji maboresho kidogo. Kwa hiyo, ningependa tu niende kwenye mapendekezo ya hayo masuala machache ambayo labda Mheshimiwa Waziri angeangalia ni namna gani anaweza

kuyaboresha kwenye huu Muswada. Jambo mojawapo ni suala la wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania katika Afrika ni mojawapo wa wafugaji wakubwa, tunazalisha ngozi nyingi, lakini hii ngozi inatozo mbili kubwa. Kuna 10% ambayo inatozwa kwenye *export* ya ngozi ambayo imetayarishwa kiwango cha *wet blue*, lakini kuna tozo ya asilimia 80 ambayo inatozwa kwa ngozi ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi tozo, zilikuwa ni kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu. Sasa kwa hali ilivyo sasa hivi, nafikiri wengi watakubaliana na mimi kwamba *tannery* zilizokuwepo ambazo tulikuwa tunataka tuzilinde zipate malighafi sasa hivi hazifanyi vizuri. Kwa hiyo, anayeumia hapa ni mkulima, anazalisha ngozi lakini ngozi haina soko. Mimi katika jimbo langu tunazalisha ngozi sana na sisi ni wafugaji, kwa kiasi kikubwa ile ngozi haina soko! Utapeleka wapi kwa vile mnunuzi mfanyabiashara yeye ile kodi siyo ya kwake, kodi inaangukia kwa mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba kutakuwa na mahitaji ya wenzetu wa nchi za Afrika Magharibi, ambao hii ngozi wanaitumia kama chakula. Sasa hawa walikuwa wananunua ngozi kutoka kwenye nchi ambazo zinazalisha sana ngozi za Ethiopia pamoja na Sudan na hawa walisitishab kupeleka ngozi huku, kwa sababu katika hali ya kawaida ngozi tunategemea tuivae kama viatu au bidhaa mbalimbali na ziweze kulete utajiri mkubwa kwa nchi yetu. Kwa hiyo, napendekeza ya kwamba, ile hoja ya *export levy* ya 10% wangejaribu kuangalia ni namna gani ili tuwe *competitive* na wenzetu, iondolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi vilevile hii ya asilimia 80, *excise duty* inamuumiza mfugaji, iondolewe. Wakulima wetu kwa kweli hawapati manufaa yoyote ya ngozi, kiasi kinachopelekea kwamba hata ngozi yenyewe sasa hivi haina ubora kwa sababu inakuwa haina thamani tena. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie hilo suala kwamba, anayeumia hapa ni mfugaji na siyo mfanyabiashara. Kwa hiyo, hii

ingeondolewa kabisa na ingewezekana wangepunguza hata nusu ingeweza kuwasaidia wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna mahitaji mengi sana ya maji, sasa hivi kutokana na karibu vijiji vingi vimepelekewa umeme vijijini, kwa hiyo, kutakuwa na urahisi wa kuchimba visima ambavyo vitatumia umeme. Naungana na wenzangu ambao wanapendekeza tuondoe kodi kwenye vifaa vya kuchimbia visima, zikiwemo *pumps*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni suala muhimu, ni suala ambalo linaendana na sera yetu, ni suala ambalo litaisaidia sana Wizara kuweza kupeleka maji vijijini. Kwa sababu kukiwa na umeme, ukachimba visima, majirani zetu, nchi zetu majirani hawana mito, wanategemea visima hata kwenye umwagiliaji. Kwa hiyo, tukichimba mabwawa na tukichimba visima, tunaweza kupeleka maji kwenye vijiji vingi kama ilivyokuwa kwenye umeme wa *REA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la kodi kwenye mikopo ya kutoka nje, Serikali imeweka pendekezo kwenye huu Muswada kwamba iondolewe kodi kwenye riba ya mikopo inayopatikana kutoka nje. Hilo ni suala zuri, litaipunguzia Serikali mzigo wa kuanza kutoza kodi kwenye fedha zao wenyewe ambazo wamezikopa kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza iende zaidi, tuna mahitaji mengi hapa ya *FDI*, fedha kutoka nje kutokana na mikopo. Ili mabenki yaweze kukopoa huko nje, nayo yanalipa riba na hii riba inakwenda kwa wakopaji, kwa hiyo, ningependekeza, hii nafuu ambayo imewekwa kwenye mikopo ambayo Serikali inapokea moja kwa moja, iende vilevile na kwenye mabenki yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wake hapa, ni kwa sababu, fedha tuliyonayo hapa nchini, nyingi ni ya muda mfupi, lakini ili uweze ku-*finance* miradi unahitaji fedha ya muda mrefu na fedha za muda mrefu unaweza kuzipata

kwenye masoko ya nje. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie ni namna gani iendani na hilo wazo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ambalo ni muhimu sana ni hiki kitengo kipya, cha *Tax Ombudsman*, hii ni hatua nzuri sana, ila ninachoomba, ili ionekane hiki kitengo kiko huru, kisiwe chini ya *TRA* na wala kisiwe chini ya Wizara, kiwe nje ya hizi ofisi, kitaonekana kiko huru zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nataka tu nisisitize kwamba hatua nyingi hizi ambazo Serikali inachukua, ziangalie ni namna gani vievile tuna *improve administration*, mengi hapa yameongelewa, tumelalamika sana, lakini unakuja kugundua kuwa, nafuu zilikuwepo, lakini *administrations* za kodi hazikuwa nzuri. Nilikuwa najaribu kuangalia hapa, *East African Community Gazette*, kumbe kulikuwa na suala ambalo kulikuwa na nafuu sana, kodi ziliondolewa, kwenye haya mataulo, mwaka 2017, lakini hili nafikiri wengi hatukulijua, mpaka leo tunafikiria kwamba hii kodi bado ipo. Kwa hiyo, ningependekeza kwamba tu-*improve* kwenye *administration* ili hizi kodi ziende moja kwa moja kuleta nafuu kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Joram Hongoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher na Mheshimiwa Saada Mkuya Chiza ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupewa nafasi kuchangia kidogo Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019, (*The Finance Bill of 2019*). Nianze kwanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na pia niipongeze Kamati kwa ushauri wao kwa Wizara na wameweza kuja na Sheria mpya nzuri ya Fedha ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kidogo kuchangia kuhusu upande wa kuondoa ongezeko la thamani

kwenye makasha ya majokofu ambayo yanatumika kwa ajili ya kuhifadhia matunda, maziwa, au mazao yanayotokana na *hot culture* na mazao ya nyama na mboga. Niipongeze sana Serikali, kwa sababu waliokuwa wanaathirika kutokana na hizi kodi za kulipia haya makasha ni wakulima na hawa wafanyabiashara wenye majokofu haya walikuwa wanaingiza gharama za majokofu, gharama za VAT kwenye bei ya mazao ambayo wanayauza wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kufanya hivi, maana yake ni kwamba sasa mazao yao, kwa mfano kule kwetu tunazalisha maparachichi, mazao kwa mfano ya maparachichi, mazao ya mboga sasa, naamini kwamba bei itapanda kidogo kwa sababu baadhi ya gharama ambazo wafanyabiashara walikuwa wanaziingia, zimeweza kuondolewa. Kwa hiyo, hilo sasa ni wajibu wa Wizara kusimamia, kuhakikisha kwamba je, ni kweli baada ya kupunguza hiyo VAT, wakulima wamenufaika au bei zinabaki palepale. Kwa hiyo, hiyo ni muhimu sana kufuatilia ili tujue kama kupunguza huku kuna tija kwa wakulima au hakuna tija kwa wakulima wetu wa mazao haya ya mbogamboga, lakini pia wa mazao ya matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuondoa ushuru au kuongeza ushuru kwenye vifaa vya plastiki ambavyo vinatumika kutengenezea miundombinu vinavyotoka nje, hatua hii ni muhimu na niipongeze sana kwa sababu, ni kweli kwa kuwa nchini tumeanza kuzalisha vifaa hivi vya pastiki, mabomba ya plastiki na yanayotumika kutengenezea miundombinu kwa mfano ya maji, vipo viwanda vya kutosha. Mwanza wanazalisha, Dar es Salaam wanazalisha na tunaamini siyo muda mrefu na viwanda vingine vitaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli visingeweza ku-*compete* na wenzetu wanaozalisha nje. Kwa hiyo, kuongeza hii tozo ya asilimia 10 maana yake tuna-*discourage* uingizaji wa hizi bidhaa toka nchi za nje na hatimaye tunaongeza wawekezaji wa ndani wawezwe kuzalisha vya kutosha, lakini

pia tunaongeza fursa za ajira kwa vijana wetu kama ilivyoelezwa. Kwa hiyo, nipongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi sasa *TBS* ni muhimu sana kusimamia uzalishaji wa hizi bidhaa za mabomba, kwa sababu kama hawatasimamia vizuri na mwisho wa siku viwanda vikaanza kuzalisha mabomba ambayo hayaweze kustahimili, hayawezi kuwa na sifa stahiki, mwisho wa siku wananchi au wanaotaka kutengeneza miundombinu hii watarudi kulekule kununua kwenye nchi za wenzetu na hatimaye baadaye sisi wenyewe tutarudi sasa kuruhusu kurudisha hilo ongezeko, kupunguza bei.

Kwa hiyo, ili tuweze kulinda ni lazima na sisi sasa tusimamie, *TBS* wasimamie viwango vya uzalishaji, ubora wa haya mabomba yatakayokuwa yanazalishwa kwenye viwanda vyetu ili baadaye na sisi tuweze kuuza hata na nchi za nje kuliko kuendelea kuuza tu hapa ndani. Kwa hiyo, lazima tuwe na soko la nje, lakini pia tuwe na soko la ndani ili viwanda vyetu viwe endelevu na ajira ziweze kuongezeka kupitia hivi viwanda vya mabomba ya plastiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipongeze kwa kurekebisha ile Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 ambayo sasa imeongeza kifungu kidogo ambacho kinaahirisha ulipaji wa kodi kwa mfanyabiashara au mtu anayeanzisha biashara au mwekezaji mara tu anapoanza biashara yake au anapoanza uwekezaji aanze kulipa kodi. Sasa amepewa miezi sita angalau kugharamia gharama nyingine kwa mfano, pango, leseni na vitu vingine ajipange kwa ajili ya kulipa kodi. Hatua hii nzuri sana na itawezesha wafanyabiashara sasa kujipanga vizuri na hatimaye kuweza kushiriki katika kulipa kodi

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi wafanyabiashara wetu wamekuwa wanakwepa kulipa kodi pale wanapoanzisha biashara kwa sababu kwanza fedha nyingi wametumia kwenye mtaji wa uanzishaji wa biashara hiyo kwa maana ya chumba labda au eneo la kufanyia biashara na gharama nyingine lakini sasa kwa sababu hii kodi

imeahirishwa kwa muda wa miezi wa sita wataweza kujipanga vizuri na hatimaye kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nipongeze hatua ya Wizara kwa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mitambo hasa ya kuchimbia visima. Ni kweli hii ilikuwa inakwamisha sana uchimbaji wa visima kwenye maeneo mengi na tunasema kwamba Tanzania tunataka tumtue mwanamke ndoo kichwani lakini kwa kuwa kodi ilikuwa kubwa na vifaa hivi vilikuwa na VAT gharama za uchimbaji wa visima ilikuwa juu sana, utakuta ni shilingi milioni 20, shilingi 24 sasa Watanzania wengi hawawezi kumudu gharama hizo za uchimbaji wa visima, kwa hiyo, wengi walikuwa wanashindwa kuchimba visima. Kwa sababu mitambo hii sasa kodi itapunguzwa maana yake wataweza kununua mitambo hiyo na tunaamini kwamba maji katika maeneo yetu ya vijijini, mama zetu kule vijijini ambako mabomba ya kawaida au maji ya mtiririko na maji ya msukumo wa umeme hayawezi kufika basi sasa wataweza kuchimbiwa visima na hatimaye kupata maji na kuhakikisha kwamba mwanamke anatuliwa ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu kodi iliyowekwa kwenye bidhaa kama zile mawigi na nywele. Mimi ningesema kwamba sasa Serikali kwa nini mmeacha kuweka kwenye kucha maana wanawake wengi utakuta wanaweka kucha ndefu wanakuwa kama jini hivi, ingeongezwa kodi kwenye hayo mawigi, kucha na kope za bandia, mbaki hivi hivi, mnavaa mnapendeza mkiwa hivi hivi *natural*. Kwa hiyo, niwaombe sana pengine hizi kucha na kope za bandia nazo zingeongezwa kodi siyo mawigi tu peke yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, inavyoonekana huu mjadala wa sisi wanawake namna tunavyotaka kuonekana unachukua sura mpya kila saa lakini wacha nisingumze sana hapo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Saada Mkuya, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe ajiandae.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi. Kwanza naunga mkono hoja pamoja na mapendekezo ya kodi ambayo yameletwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Waheshimiwa Wabunge wanako-*propose* kuna kodi ziondolewe *at this stage* labda ingekuwa busara *sometimes* Serikali ikaelezea *process* ile tunayofikia mpaka tukaja na haya mapendekezo ya kodi. Siyo jambo jepesi na Watendaji wetu wote wa Serikali wanashiriki katika kufanya *process* hii mpaka tunafikia hapa tulipo. Ni *process* ndefu ambayo ina-*involve sleepless night* na vitu vingine kama hivyo. Kwa hivyo, nadhani hili jambo si jambo jepesi kama ambavyo tunaliona lakini Watendaji wana-*consume a lot of time and energy* kufikia hapa tulipo. Kwa hivyo, nadhani sisi kama Waheshimiwa Wabunge lazima tu- *appreciate process* hii mpaka hapa ambapo tunafikia na mpaka ambapo Serikali imeleta hiki ambacho imekileta. *(Makoff)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi wakati nilipokuwa nikichangia Bajeti Kuu ya Serikali nilipongeza sana Serikali kwa sababu *this time around* hatukwenda katika kutafuta kodi mpya per se lakini tuna *interest* ya kuangalia *how best* tunaweza tukazisimamia kodi tulizonazo ili kuleta yale manufaa ambayo tunayatarajia. Kwa sababu si lazima tuwe na kodi mpya lakini muhimu ni kuweza kukisimamia kile ambacho unacho na kufikia pale ambapo unatarajia. Kwa hiyo, *again* naipongeza sana sana Serikali kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mapendekezo ambayo aliyadokeza Mheshimiwa Khadija Nassir hususan kwenye suala la *VAT* ambapo Serikali imeondoa *VAT* kwenye umeme ambao unauzwa kwa *supplier* kule Zanzibar. Hii ni hatua nzuri na ni hatua ambayo itapelekea kwa kiasi fulani kuweza kupunguza mzigo wa gharama za maisha kwa

wenzetu wa Zanzibar. Labda ingekuwa busara vilevile sasa tukaangalia eneo hili la bidhaa ambalo limekuwa gumu kidogo kuli-*administer* lakini naamini kwamba hatujashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mwaka 2016 bidhaa ambazo zilikuwa zinapelekwa Zanzibar zilikuwa zinapitia katika *process ya refund* lakini ikaonekana kidogo *process* hii imekuwa na changamoto kuikusanya ile *refund* na kuipeleka Zanzibar wakati pengine Zanzibar wanataka kutumia wakati ambapo pengine *refund* ile ilikuwa bado haijapelekwa. Kwa hivyo, kuanzia mwaka 2016 tulipobadilisha ile Sheria ya kupitia *Finance Bill* kukawa kuna kipengele cha *zero rate goods* ambazo zinanunuliwa *from locally manufacturer* yaani anayenunua ni yule *VAT registered in Zanzibar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo imeleta changamoto kwa maana kwamba gharama ya maisha imepanda kwa sababu kwanza wanaonunua kutoka kwa *manufacturer* ni wachache lakini bidhaa muhimu zinazotumiwa na wananchi Zanzibar ni bidhaa za kawaida zinazonunuliwa katika maduka yetu ya kawaida. Hilo limeleta changamoto kwa sababu kwa upande wa Bodi ya Mapato kule Zanzibar na wao wanataka wakusanye *VAT* pale ambapo inatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili tumeona kwamba ikiwa wale wafanyabiashara watanunua kwenye maduka mengine halafu ziwe *exempted* itakuwa tunapalilia hili jambo la ku-*dump* bidhaa zinakuwa Zanzibar hazifiki lakini zinatumiwa njia nyingine za panya kuziingiza tena bidhaa hizi sokoni zi-*compete* na bidhaa nyingine ambazo zinalipiwa kodi. Hilo hatulitaki na hakuna mtu anayelipenda. Maana yake nini? Siyo kama Serikali tumeshindwa kufanya hivi, sasa hivi kama ilivyoonyeshwa katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inasema kwamba tunaangalia jinsi gani tutaweza kwenda mbele zaidi ku-*strengthen* hata hizi *electronics system* kuweza ku-*capture* hata wale ambao wanakwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeiomba sana Serikali iangalie hizi *electronics system* zinaweza vipi ku-*address* changamoto hii ambayo inatukabili. Kwa mfano, hata kama tunatumia *TANCIS*, tunaweza kubaini bidhaa hizi zimenunuliwa na tukazi-*track* wapi zimekwenda, lakini vilevile *iTAX* inaweza ikasoma bidhaa hizi zimenunuliwa na wapi zinakwenda. Tunahitajika sana sasa kama watendaji wa *TRA*, hili wala siyo la Mheshimiwa Waziri, lakini watendaji wa *TRA* tufikiri *outside the ordinary box* ili kuweza ku-*address* changamoto hii ambayo imekuwa kubwa in *such a way* kwamba kwa wenzetu kule maisha yamekuwa na gharama kubwa na hili siyo lengo la Serikali. Nadhani katika jambo moja ambalo Serikali inaleta *tax measure* ni pamoja na kuhakikisha kwamba kunakuwa na urahisi wa kukusanya lakini haiwi *bad* kwa wale wananchi ambao ndiyo wanalipa kodi na ukizingatia *VAT* ni yule *final consumer* ambaye ndiye anayelipia nadhani hapa tumeona kwamba *effect* yake mara moja imeweza kuathiri maisha ya watu kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo hili, tumekuwa tukilizungumza muda mrefu na imekuwa kama tumegota maana yake kama tumekuwa hatupati *solution* na tunaishia tu kuangalia kwamba hii athari yake inaweza ikawa hivi lakini hatujaenda mbele zaidi kuangalia vipi jambo hili tunaweza tukali-*address*. Kwa hiyo, natoa ushauri vilevile kwa *Commissioner General* mpya katika moja ya *task* zake ambazo atakuwa anazikabili ni pamoja na ku-*address* changamoto hii. Kwa kuanzia inawezekana kabisa labda akaenda akaonana na mwenzake kule Zanzibar wakaweza kulizungumza maana yake sasa hivi imekuwa hapa ndipo tulipofikia lakini bado tuna *room* ya kuweza kuangalia vipi mifumo yetu hii ya kielektroniki inaweza ikaimarishwa na jambo hili likawa *addressed*. Masuala haya hayatotumika *tax measure* nadhani ni *administration* zaidi kuliko kuingiza *measures* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi sikuwa na jambo kubwa sana la kulizungumza na nisichukue muda wako, naunga mkono hoja na naipongeza sana Serikali kwa hatua hizi, najua mpaka hapa tulipofikia ni *energy* kiasi gani

tumeweza ku-*consume*. La msingi, naomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri akubali kwamba jambo hili sasa liangaliwe kwa mtazamo mpya zaidi ili kuweza ku-*address* changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa kuna mapato ambayo yanapotea kwa upande wa Tanzania Bara lakini kuna mapato vilevile yanapotea kwa upande wa Zanzibar. Pengine tukiliangalia kwa mapana yake linaweza likasaidia kuweza kupata mapato zaidi lakini linaweza vilevile kusaidia kuwa-*administer* hizi bidhaa ambazo zinakwenda Zanzibar. Pia tukiangalia mifumo yetu inaweza vilevile ikatusaidia ku-*capture* wale ambao wanakwepa kodi kupitia *system* hizi zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *otherwise* naunga mkono hoja na naipongeza sana Serikali kwa hatua hii. Nashukuru. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, Mheshimiwa Maulid Mtulia ajiandae.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Kwanza niseme kwamba naipongeza Serikali na naunga mkono hoja lakini nina maboresho machache ambayo ningeshauri Serikali iweze kuyafikiria ili yaweze kuingia katika *Finance Bill* ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la jumla nilitaka niiombe Serikali kwa dhati, mpaka leo wanunuzi wa pamba hawajaingia kununua zao la pamba katika maeneo yetu. Ningeomba zichukuliwe hatua za haraka sana. Vilevile ningeshauri Serikali utaratibu wa kisheria na ninaamini sheria zinavyotungwa ni kwa ajili ya kumtumikia mwanadamu na wala siyo mwanadamu kuwa mtumwa wa sheria. Kama sheria haiko *practical* katika mazingira halisi, nashauri itazamwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, bei ya pamba inakuwa *determined* na bei ya soko la dunia. Tumetangaza bei ya shilingi 1,200 lakini kwa utaratibu ni kwamba pamba hizi zinatakiwa zinunuliwe kupitia *AMCOS* pale kwenye *AMCOS* pamba inapowekwa katika *go-down* ni mnunuzi ndiyo mwenye gharama ya kubeba ile pamba kurudi nayo kiwandani kwake. Kwa hiyo, kuna *additional cost* ya *transportation*, kuna asilimia 3 ya *cess*, kwa hiyo, bei ya mnunuzi inazidi shilingi 1,200. Kwa hiyo, wanunuzi wengi hawaendi na Serikali imeonyesha nia ya kutoa *guarantee* kwa wanunuzi katika *financial Institution, financial institution* ikiangalia *contract* ambazo wanunuzi wanazo, inaona kuna *risk* ya mnunuzi huyu atakwenda kukutana na hasara sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwashauri ule utaratibu wa Ma-DC kuwalazimisha wanunuzi wa pamba kununua pamba kupitia *AMCOS*, naomba Wizara ya Kilimo na Serikali itoe *relief* wakulima wapeleke moja kwa moja kwa wanunuzi kwa sababu itampunguzia gharama ya *transportation* huyu mnunuzi. Hii imetokea maeneo ya Bariadi, wakulima walianza kuuza pamba kwenye *ginery, DC* akatoa amri ya kumzuia mnunuzi asinunue matokeo yake pamba imebaki mikononi mwa wakulima. Kwa hiyo, naomba Serikali tutafute *intervention* ya haraka, futeni shilingi 100 ya bodi ili bei ya pamba iweze kuwa *affordable* kwa mnunuzi kununua, hili lilikuwa la jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja iliyoko mbele yetu, Serikali imefanya *effort* kubwa sana kutaka kufanya *reforms* na *harmonization* mbalimbali lakini naomba nitoe ushauri. Hapa kumekuwa na hoja ya pedi muda mrefu sana, kuna *measure* inatajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo imetolewa kwa ajili ya *diapers* kwamba kwenye ushuru wa forodha tuna *exemption* inasema kwamba kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwenye malighafi ya kutengeneza taalo za watoto (*baby diapers*). Nawaomba Serikali wekeni hapa na pedi ili i-*accommodate two products*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja ya Serikali kwamba *measure* hii imekuwepo siku za nyuma lakini hatukuona *efficiency* ya *measure* hii ikionyesha uwezekano wa bidhaa hii kuwa *affordable*. Inawezekana kuna matatizo ya kiutawala lakini tunawaomba muweke *clarity* hapa itamke kabisa taulo za akina mama na taulo za watoto. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilitaka nishauri, Serikali tumeamua kuwekeza kwenye *airline*, leo tunawekeza katika *airline industry* na tumetoa *measure* ya kutoa *exemption* kwenye *lubricants*, nawaomba Serikali muende hatua ya mbele. Nawashukuru mmetoa *clarifications* ya *local operators*, mmeweka wazi kwamba *local air transporters*, nawaomba ondoeni kodi ya *withholding* ya *ten percent* pale ambapo mfanyabiashara anapoamua kununua ndege kwa sababu *private sector* hawanunui ndege kwa *cash* wananunua ndege kwa *credit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, anaponunua ndege ile kwa *credit* ile *down payment* anayolipa kwa mujibu wa sheria zetu anatakiwa alipe *ten percent withholding tax*. Nawashauri futeni hii, mmefanya *effort* ya kuweka *exemption* kwenye *lubricants* na nafahamu mmefanya *effort* ya kuweka *exemption* ya VAT kwenye *insurance* na *spareparts* za *airline*, nawaomba sana muweke *exemption* ya ku-*remove withholding tax on re-payment of principal payment on purchase of aircraft*. Hii itatusaidia sisi ku-*attract a lot of investors* kuja kwenye sekta ya ndege katika nchi yetu na wafanyabiashara wa ndege watakuja hapa kuwekeza kuwe na *linkage* kati ya *Air Tanzania Investment* na hizi ndege ndogondogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwenye suala la ngozi, ameliongea Mheshimiwa Njeza, sekta ya ngozi ina mzalishaji wa ngozi ambaye ni mfugaji na mfanyabiashara wa kuchinja mifugo lakini ina *trader* na *processor* na hawa *processors* wamegawanyika sehemu mbili. Kuna *processor* aliyeko katika *level* ya kwanza anaye *produce wet blue* lakini kuna anaye *produce crust* na anaye *produce finished goods*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa kuwa sisi hatuko kwenye kijiji tuna-*compete* na *other players around the world*, taarifa ya Kikosi Kazi cha Wizara ya Mifugo imesema wazi changamoto kwenye sekta ndogo ya ngozi ni mbili. Moja, ni *export levy* ambayo tunaiweka kwenye *ten percent* ya *wet blue* matokeo yake viwanda vilivyoko ambavyo ni viwanda saba katika nchi yetu haviwezi kununua ngozi hizi kutoka kwa wakulima kwa sababu ngozi haziziki nje. Nawaomba Serikali waiteni wenye viwanda sainisheni nao *performance agreement* muwasimamie waweze kununua ngozi tuweze ku-*process* ngozi hii na ku-*add value* ili tuweze kwenda *level* ya *crust* na *level* ya *finished goods*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa ku-*excise duty* mliyopunguza kwenye mazao yanayotokana na mvinyo unaotengenezwa na ndizi na vitu vingine. Ushauri *extend* hii *docket* muongeze na mvinyo unaotokana na zabibu. Zabibu inachajiwa Sh.200 *per kilo*, tume *propose* Sh.60 kwenye mvinyo unaotokana na mazao yanayotengenezwa na ndizi, nini ushauri wangu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni Mkoa wa Dodoma, ndiyo tunazalisha zabibu. Zabibu ina changamoto ya vifungashio kwamba kwa kuwa vifungashio vyote tuna *import processor* wa mvinyo unaotokana na zabibu anakuwa *not competitive outside* mipaka ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wakiongeza hiyo, tukampa na yeye *incentive* ya Sh.61/=, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, dada yangu Mheshimiwa Ashatu ambaye yuko hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwenye mpango tunatenga *ten billion* kwa ajili ya ngozi. Ushauri wangu wa-*allocate* hizo *ten billion* kwenye zabibu ili tuweze kupanua sekta ndogo ya zabibu, wakulima walioko Dodoma waweze kufaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niwaombe sekta ya kilimo ndio imeajiri Watanzania wengi, nawaomba sana pendekezo ambalo tumelitoa kwenye Kamati na wadau wamekuja nalo la kuomba *exemption* ya VAT kwenye

vifungashio kwenye *grain drying equipment* kwenye sheria wamesema kwamba *for a person engaged on agriculture* yaani yule mkulima wa Nzega ndio anunue hiyo *equipment*, nawaomba waongeze *for a person engaged on agriculture and the dealers and agent* kwa sababu *wanao- import* hivi vifaa sio mkulima wa Nzega... (Makofi)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, nadhani hoja yako imeeleweka.

Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba ajiandae.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunakamilisha kazi ambayo tumeifanya kwa takribani miezi au siku 50 za kazi lakini tuko hapa zaidi ya takriban miezi mitatu ambapo mapato yote ambayo tumeainisha kwenye *volume one revenue estimates*, sasa tunayatumia sheria *of course* bado kuna mapato ambayo sijayaona *addendum* ikiwa imekuja hapa ya vitambulisho vya Wamachinga ambayo bado hayajaweza kuoneshwa hasa kwenye taarifa hii ya mapato ya Serikali, mapato hayo yameelekezwa wapi, naamini kwamba *by* kesho wakati tunapitisha kwa sababu Sheria ya Fedha ndio hasa inaenda ku-*effect revenue book* ambayo tulipewa hapa, kwa hiyo naamini kwamba *addendum* itaweza kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu moja ya mapato ambayo kikawaida hatuioni kwenye *Finance Act* lakini tunakuwa tumeipitisha na hatuioni kwa sababu haionekani kama ni kodi na hii ni eneo hasa la mikopo. Katika eneo hili ningependa tuangalie uwezekano wa *Finance Bill* zinazokuja tuwe tunaweka katika *Finance Act* kwa sababu ya kuweza kutoa ruhusa ya kisheria kwa Serikali yaani Bunge kutoa ruhusa ya kisheria kwa Serikali kuweza kwenda kukopa ili tuwe tunaweka ukomo wa mikopo ambayo Serikali

inakwenda kuchukua hasa mikopo ya nje ambayo inakuja kujenga na kuongeza deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwaka huu tunatarajia kukopa kwa mujibu wa mfumo wa bajeti, sura ya bajeti ya mwaka 2019/2020 jumla ya shilingi trilioni 2.3 kama mikopo ya kibiashara. Ukitazama kwenye ukurasa wa 104 wa Hotuba ya Bajeti tunakuta kwamba mikopo yenye masharti ya kibiashara tunakwenda kukopa jumla ya shilingi trilioni 2.3, lakini sasa ukiangalia kwa mfano Serikali sasa hivi inahangaika kutafuta mikopo kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake walipokuwa kule DC Washington kwenye mkutano wa majira ya kipupwe ya mikutano ya *Bretton Wood Institutions* walikutana na watu wa Benki ya *Standard Chartered* kwa ajili ya kuomba mkopo wa dola za Kimarekani bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati, kipande cha kuanzia Morogoro mpaka Dodoma na baadaye kwenda mpaka Isaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaenda kukopa fedha hizi kwa ajili ya reli hii, lakini reli hii ni reli ambayo inakwenda kunufaisha nchi nyingine, hainufaishi nchi yetu kwa sababu ya mwelekeo wa reli yenyewe. Nilikuwa natazama hapa namna gani ambavyo bandari zetu zinakua kwa kuongeza mizigo, nimekuta kwamba bandari ambayo ni *fastest growing* inayokua kuliko bandari zote katika nchi yetu ni Bandari ya Kigoma, ambayo mwaka jana imekuwa kwa asilimia 43.7. Bandari nyingine inayofuata ni Bandari ya Tanga, lakini Bandari ya Mwanza ambako ndio reli inakwenda mwaka jana imekuwa kwa *negative 31.8 percent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilishangaa Rais wa Congo alipokuja hapa nchini, Serikali ilimpeleka kuangalia *SGR* na alivyoenda kule wanazungumzia kuifanya Rwanda kuwa *Logistic hub*, *SGR* iende mpaka Rwanda, Congo waende kuchukua mizigo Rwanda, maana yake ni kwamba tunaiua Tanzania, tunaiua Bandari ya Kigoma na Bandari ya Kigoma itakuwa haina maana yoyote, nami hili naona ni uhujumu kwa nchi yetu na jambo hili linapaswa kuzuiwa. Njia

pekee ya kulizuia jambo hili ni kuhakikisha kwamba mikopo ambayo tunakwenda kukopa huko nje kujenga reli kwa ajili ya kupeleka kwenye nchi nyingine, Bunge likatae ili lielekeze mikopo ambayo inakusanywa iende sehemu ambayo italeta maendeleo kwa ajili ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilipenda kulizungumza, kuna mazungumzo hapa kuhusiana na suala zima la pamba ni dhahiri kwamba Waheshimiwa Wabunge wana wasiwasi kwamba tunaenda kupata matatizo ambayo tuliyapata kwenye zao la korosho na Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwa undani sana namna gani ambapo tunaweza tukatatua tatizo hili na mimi sina haja ya kurudia eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja tu ambalo naomba niwakumbushe na naiomba Serikali ilichukue kama wazo, kuna haja kubwa kwamba haiwezekani kila mwaka tunakuja hapa Bungeni tunalalamika kuhusu kuporomoka kwa bei ya mazao na namna gani ya kuwalipa wakulima. Mwaka jana tulikuwa na mgogoro mkubwa wa korosho haujakwisha, mpaka leo mmesikia mijadala kuhusu korosho. Mwaka huu sasa tuna mgogoro wa pamba ambapo bei iliyotangazwa na Serikali na bei ya soko la dunia haviendani. Sasa napendekeza kwamba, Serikali ilete Muswada wa Sheria wa kuunda Mfuko wa *Price Stabilization* ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa tunachanga change kidogokidogo, bei za soko la dunia zikiporomoka tuweze kuwafidia wakulima kiwango kile ambacho kimeporomoka na hatutakuwa tena na mgogoro wa bei za mazao yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Serikali ichukue wazo hili, tumekuwa tukilizungumza mara kwa mara iende ikalifanyie kazi na mfumo ambao unaweza kusaidia hili ni kuanzisha mfumo wa hifadhi ya jamii kwa wakulima ambapo ndani yake kunakuwa na fao la bei ambalo linaweza likatatua matatizo kama haya ambayo tunayapata kwenye pamba sasa hivi na tuliyapata mwaka jana kwenye korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya mwisho inahusiana na mapendekezo ambayo Serikali iliyaleta kuhusu *sanitary pads*. Serikali imeeleza hatua mbalimbali ambazo imechukua, Kamati ya Bajeti na napenda niipongeze sana Kamati ya Bajeti imezungumza na Serikali na Serikali imeweza kuongeza makampuni ambayo yatakata ile nafuu ya kodi ya mapato ya miaka miwili kwamba ni makampuni ambayo yapo hivi sasa na makampuni yatakayoanzishwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wakati tunazungumza hapa Serikali ilitueleza na ni hoja ambayo Mheshimiwa Bashe pia ameizungumza kwamba kuna *duty remission* ambayo imekuwepo toka mwaka 2009, miaka 10 ambapo uingizaji wa *raw materials*, malighafi za kuzalisha *sanitary pads* hapa nchini kodi yake ya ushuru wa forodha ni asilimia sifuri na kwenye Kamati ya Bajeti Serikali imetuletea ushahidi wa namna gani ambavyo hilo limekuwa likitekelezwa na hapa nina orodha ya makampuni ya Tanzania ambayo yanafaidika na nafuu hiyo na ni makampuni mawili tu sitaki kuyataja kwa majina kutokana na daftari la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha nini? Hii inaonesha kwamba Serikali inashindwa kutimiza wajibu wake wa kuwaelewesha Watanzania nafuu gani ambazo zipo zinaweza zikatekelezwa ili kuweza kuhakikisha kwamba bei ya *sanitary pad* inapungua na ndio maana mpaka baada ya Serikali kubanwa sana ndio tumeweza kufahamu kwamba kuna *duty remission* hii ambayo ingeweza kusaidia, Serikali ingeieleza toka mwaka jana, Serikali ingechukua hatua za kueleza wadau wote katika sekta, leo hii pengine tungekuwa tunajadili masuala mengine kuhusiana na suala la *sanitary pads*.

Naitaka Serikali ihakikishe kwamba hii nafuu inafahamika kwa wazalishaji kwa sababu ni nafuu ambayo ni kubwa, ni nafuu ambayo ingefahamika toka mwaka jana inawezekana leo tusingekuwa na kelele ambazo tunazo mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba niombe Serikali iendeleo kufikiria wazo ambalo Kamati ya Bajeti imelitoa la kuona ni namna gani ambavyo VAT katika bidhaa hizi muhimu na sio kwa wanawake peke yake na hata kwa watoto zile *diapers* waziwekee *zero rating* kwa bidhaa zinazozalishwa ndani na bidhaa zinazozalishwa nje, ukichukua *measures* zote hizi ya *import duty* ya *zero rating* na hatua za kiutawala za bei elekezi, nina hakika kabisa kwamba tutaweza kuuza au wananchi wetu wataweza kununua *sanitary pads* kwa chini ya Sh.1,500/=, inawezekana inahitajika Serikali itimize wajibu wake, wajibu wa kuongoza na sio wajibu wa kutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maulid Mtulia atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Edward Mwalongo ajandae.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi nianze kama kawaida kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na hatimaye kupata fursa hii ya kujadili Muswada huu wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019/2020. Nikushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa, kimsingi nitakuwa sijafanya sawa kama sitawashukuru Wizara kwa kukubali kuja na marekebisho ya sheria takribani tisa kama walivyoorodhesha hapa na hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali na kwamba Serikali yetu sikivu na imekuja na mabadiliko haya kwa lengo la kuleta ustawi kwenye nchi yetu na kuhakikisha tunakusanya kodi za kutosha kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kodi kimsingi kila mwananchi anapaswa kulipa kodi na naamini wananchi tunalima kodi ama *direct* kodi au *indirect* kodi, lakini lazima kila mtanzania ajue ana wajibu wa kulipa kodi ili kuchangia maendeleo ya nchi yake. Niwatake watu wetu wa Kinondoni kwa kweli tujitahidi tulipe kodi kwa sababu Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ametupa miradi mingi sana katika

Jimbo letu la Kinondoni. Tuna mradi wa mkakati wa soko la Magomeni, soko la Tandale, *Coco beach* na barabara ya *DMDP*, mambo ni mwemwelemwemwele Kinondoni. Kwa hiyo tunapoonaa mambo haya yanafanyika maana yake lazima pesa zinazotumika ni fedha za kodi na sisi tuwe wa mfano kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kodi tunakubaliana kwamba wenye kingi walipe zaidi, wasio nacho wapunguziwe au waachwe, katika mahitaji ya lazima tupunguze kodi, lakini mahitaji matumizi ya *leisure* matumizi ya burudani na starehe tulipe kodi. Kwa msingi huo nakumbusha wananchi wetu wanalamika sana kwamba inapofika mgonjwa amefariki katika hospitali hasa za Serikali wale wananchi wakionesha kwamba hawana uwezo tuwepo na kitu kusamehe, msamaha wa maiti kwamba huyu maiti tunakubaliana alikuwa analipa kodi na hata hao ndugu zake wanalipa kodi na hata sisi Watanzania wengine tunalipa kodi isifike mahali maiti ikazuliwa, ikazikwa na *city* kwa sababu tu maiti imekosa pesa ya kulipia gharama ehe, kwa sababu hata waganga wa kienyeji ukifariki tu wanakupa maiti yako nenda ukazike, sasa haiwezekani hospitali za Serikali yetu, mwananchi wetu aliyekuwa akilipa kodi miaka yote, ndugu zake wanalipa kodi miaka yote... (*Makofi*)

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtulia kuna taarifa, Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji, sio hivyo tu pale mimi kwangu Tabata ninakoishi kuna Mzee mmoja ameapa amesema yeye akiagua asipelekwe Muhimbili kwa sababu maiti ya mjukuu wake imekaa Muhimbili miezi mitatu, kwa hiyo ameacha wosia kabisa pale msikitini akasema akiagua asipelekwe Muhimbili, kwa hiyo mimi na ku- *support* hicho unachokisema. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka hiyo sio taarifa hiyo, ungesubiri upewe fursa yako ya kuchangia kwa sababu sio taarifa kuhusu mambo ya Kinondoni. Mheshimiwa Maulid Mtulia.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba hilo alilolisema liingie kwenye mchango wangu ili watu wa Kinondoni waone.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni *very serious*, tusilichukulie kwa wepesi na ndio maana nikasema tunapokuja kwenye dhana ya kodi, tutoe kodi kwa watu wenye uwezo watoe zaidi, wasiokuwa na uwezo wasamehe, lakini kwenye mambo ya lazima tunaweza kuweka upungufu wa kodi, lakini kwenye mambo ya *leisure* tukaongeza kodi, huo ndio msingi hasa wa kodi. Sasa hili jambo tusilichukulie kwa wepesi, tutafurahi sana kwamba Serikali wakiruhusu wananchi wetu huko kwa kweli watapata stara ya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachooona ni kwamba tuna kila sababu ya kuongeza vyanzo vyetu vya kodi. Nataka Waheshimiwa Wabunge wenzangu kama tutakubaliana, tufike mahali katika yale mambo ambayo tunaamini mambo haya si ya lazima, Serikali wakija na mapendekezo ya kuongeza kodi tuwape moyo, isiwe kila jambo Serikali wanatuletea la kuongeza kodi katika jambo la *leisure*, jambo la starehe, jambo la burudani tunapinga, lakini Serikali hiyo hiyo inapopeleka mapato kidogo katika mambo ya msingi mambo muhimu vilevile tunalalamika, tujue kwamba ukusanyaji wa kodi ndio unapelekea huduma za kijamii ambazo tunazitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia makampuni ya simu, juzi hapa tu tumeona *Airtel* wametoa gawio kwa Serikali, lakini kimsingi makampuni ya simu na Watanzania tunapenda sana simu, tunalipa bando, tunalipa muda wa maongezi sana yanapata faida. Wakati umefika sasa Serikali iweke utaratibu, tuweke sera kwamba makampuni yote ya simu kwa sababu faida zake ziko wazi, Serikali iwe na *share*

katika makampuni ya simu kama ilivyokuwa kwenye *Airtel*, kama ilivyokuwa kwenye *Voda* na vilevile makampuni yote yasiyokuwa na *share* ya Serikali, Serikali iweke *share* pale ili Serikali yetu iongeze mapato. Mfano, maana yake tuna hiyo *Tigo*, kuna *Halotel*, kuna *Smart*, kuna *Zantel*, makampuni yote na kitaalam watu wengi wanapata hofu sana kwamba makampuni ya simu tunazidi kuyasajili, simu ni mtandao wa habari, ni jambo ambalo muhimu na jambo ambalo linahitaji kuwa *serious* kupata *information* zote zinazokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposajili makampuni mengi ya simu mpaka mtandao unasumbua wakati mwingine hata kupata mtandao kutoka kampuni moja kwenda kampuni nyingine inakuwa ni shida uwapigie simu jamani hapo vipi mtandao hapo hamna waongeze wafungue hiki, kwa hiyo ni vizuri tuwe na utaratibu wa kuwa na makampuni ya simu machache ambayo yanafanya kazi kwa ufanisi na makampuni yote Serikali iwe na *share*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuongeze kodi katika mambo yetu ya michezo ya bahati nasibu. Hatuwezi kuendelea kama Taifa letu ni Taifa la watu wanaotaka kuishi kwa kubahatisha. Sasa hivi vijana wako kwenye mikeka kila ukipita vijana wanachana mkeka, imefika mahala mpaka watendaji wa Serikali, nina wasiwasi mara nyingi Mheshimiwa Spika anatukataza hapa, jamani Waheshimiwa Wabunge msicheze bahati nasibu, lakini Taifa limefika mahali wanategemea kupata utajiri kwa njia ya kubahatisha. Sisi ambao tumewahi kusoma *mathematics* tunajua bahati na sibu ni *probability* na mchezaji haji na *capital* yake eti ataitumia *capital* yake kuwapa watu zawadi, mchezeshaji anachokifanya anakusanya pesa za wanyonge, pesa za Watanzania hawa 1,000,000, anatoa washindi watatu, kwa hiyo ni pesa za wanyonge zinakusanywa zinachukuliwa na mabwanyenye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya zaidi kuna makampuni ya bahati nasibu mpaka ya kutoka nje, yanatoka Uingereza, yaani leo Waingereza wanatuletea kampuni ya bahati nasibu kuchukua pesa zetu za wanyonge

wakishazikusanya, wanaziingiza kwenye dola zikishakuwepo kwenye dola zinapelekwa Uingereza, hatuwezi kuwa na Taifa kama hili kwamba watu wanakusanya uchumi wao watu wanyonge zinakusanywa haiwezekani na kama kuna ulazima wa kuwa na bahati nasibu basi iwe bahati nasibu ya Taifa, ili pesa hizi za hawa watu wenye tamaa isiyokuwa na uelewa zikikusanywa zirudishwe kwenye maendeleo ya wananchi wetu wa Tanzania hapa, maana pesa ya Mtanzania, kwa tamaa yake ya kupata utajiri, kaenda kucheza akipata heri, akikosa ule mzunguko wa pesa uende ukarejeshe kutengeneza hospitali zetu, ukarejeshe kutengeneza barabara zetu na sio kuchukuliwa hela kupelekwa nje, halafu Watanzania wakaachwa hivihivi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya zaidi kuna makampuni ya bahati nasibu mpaka ya kutoka nje, yanatoka Uingereza. Yaani leo Waingereza wanatuletea kampuni ya bahati nasibu kuchukua pesa zetu za wanyonge, wakishazikusanya wanaziingiza kwenye dola, zikishakuwa kwenye dola zinapelekwa Uingereza. Hatuwezi kuwa na Taifa kama hili kwamba watu wanakusanya uchumi wa watu wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna ulazima wa kuwa na bahati nasibu basi iwe Bahati Nasibu ya Taifa ili pesa hizi za hawa watu wenye tamaa wasiokuwa na uelewa zikikusanywa zirudishwe kwenye maendeleo ya wananchi wetu wa Tanzania hapa. Maana hii ni pesa ya Mtanzania kwa tamaa yake ya kupata utajiri, kaenda kucheza akipata kheri, akikosa ule mzunguko wa pesa uende ukarejeshe kutengeneza hospitali na barabara zetu na siyo kuchukuliwa hela kupelekwa nje halafu Watanzania wakaachwa hivihivi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli jambo hili tunatakiwa tuliangalie sana. Bahati nasibu ama iwe ya nchi au Serikali iwe ina-*share* ili kuzuia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajjandae.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii lakini nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia *Finance Bill* ambayo ndiyo inatupeleka mwisho wa kuhitimisha bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Wizara, Waziri na Naibu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kuandaa bajeti na Muswada huu. Kipekee kabisa niendeleo kuipongeza Wizara na Serikali nzima kwa kukubali mapendekezo na kuja na *addendum* za mapendekezo ambayo yamerekebishwa ambayo kwa kweli ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Kamati ya Bajeti, Kamati ya Bajeti naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba Serikali ipokee pongezi zifuatazo. Naomba ipokee pongezi za wafanyabiashara wote wanaoshughulika na vinywaji. Viwanda vyote Tanzania vimeipongeza bajeti hi kwa sababu kwenye vinywaji hamkugusa na walipokuja kwenye Kamati wametoa pongezi. Naomba nizilete kwenu kwa niaba ya wafanyabiashara wote wa vinywaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaletee pongezi nyingine za viwanda vyote vya sigara. Viwanda vyote vya sigara vimekuja kupongeza ndani ya Kamati ya Bajeti wakisema mtufikishie pongezi Serikalini kwa sababu mme-*maintain* kodi ambazo zilikuwepo mwaka jana. Pia pongezi nyingine ni kwa viwanda vingine vya ndani ambavyo ushuru wake mmeweza kuulinda. Kwa hiyo, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ipokee salamu hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niipongeze Serikali kwa ujumla kwa sababu imeamua kuendeleza, kulinda na kusajili biashara ambalo tu ni jambo kubwa na kwa kweli lazima muendelee kujipongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye Muswada wenyewe, labda nianze moja la ndugu yangu mdogo wangu Mheshimiwa Zitto Kabwe. Ni moja tu katika kukuweka sawa, umesema vizuri kwamba Serikali inakopa, nakubaliana na wewe na tumelezwa kwenye bajeti lakini unaposema Serikali hainufaiki kabisa na mikopo hii, hapo ndipo utakuwa hukukwenda vizuri. Umesema vizuri Bandari yetu ya Kigoma inakua, nakubaliana na wewe, lakini ukuangalia tunapojenga *Standard Gauge* mizigo sasa hivi kwa reli hii tuliyonayo inayopokelewa bandarini na inayokuja kwenye mfumo wa reli ni asilimia 5. Tuna imani kwamba kwa *Standard Gauge* mzigo sasa utakuwa mwingi na nina imani Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haisemi inapeleka *Standard Gauge* Mwanza tu na hata Kigoma kwetu *Standard Gauge* itakuja. Kwa hiyo, kuwa na subira Chama cha Mapinduzi kitakupa Sera na Ilani mambo yataenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko hizi hatua ambazo Serikali imezichukua za *sanitary pads*. Ushauri wangu sioni tukifanikiwa haraka kushusha bei kwa sababu huu ushuru wa *corporate* kutoka asilimia 30 kwenda 25 kwa viwanda vilivyopo kidogo tutaanza, lakini kwa viwanda vipya ambavyo tunaanzisha kwa sababu mpaka viweze ku-*mature* gharama za kuanzisha viwanda mpaka waweze kuwa na faida itatuchukua muda mrefu. Tatizo hili ni kubwa, akina mama wanazihitaji hizi pedi leo na siyo kesho, kwa hiyo, hizi hatua nazo lazima tuziangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mmesema mnaanzisha viwanda vingine Simiyu na Kibaha, hiyo ni *measure* ambayo itachukua muda mrefu. Pia mmesema mtaweka *performance agreement*, naomba Wizara muendeleo kuliangalia agizo hili, hili ni moja ya eneo ambalo litaweza kuangusha hii *promise* mliyoiweka kwa wananchi wetu. Tumekuwa na *zero rate* ya *raw material* kwa pedi zote

ambazo zilikuwa zimezalishwa tangu miaka hiyo lakini bei hazijaweza kushuka. Kwa hiyo, ni vizuri eneo hili muendeleo kulifanyia kazi kwelikweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uondoshwaji wa mizigo bandarini. Ni jambo zuri kisheria kuanzia zamani ilikuwa inaruhusu watu binafsi kutoa mizigo lakini safari hii mmekuja na *move* kwamba lazima tutumie watu binafsi, *clearing and forwarding* wasiweze kutumika. Kwa hiyo, naomba mliangalie tena vizuri kwa sababu mtajaza watu pale bandarini patakuwa pamejaa na pale *railway* hata nmna ya kuvuka watu kuja kuingia *TRA* pale kwenye bandari, tuangalie watu watakuwa ni wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tuendeleo kulifanyia kazi. Kama tutaona kwamba inaleta usumbufu na watu binafsi hawajui namna ya kuingia kwenye *computer*, kila bidhaa inayokuja ina *code* namna ya kuingiza kwenye *computer*, wanafunzi wetu tu wa vyuo vikuu ambao wamemliza *form six* kama wanaomba mikopo *online* wanashindwa kwa sababu walijaza vibaya, tutakuwa na *rejects* nyingi sana pale *TRA* kwa sababu watu wamejaza vibaya na hatimaye sasa *delay* kutoa mizigo itanza kuwa kubwa. Kwa hiyo, ni vizuri kama Serikali muendeleo kuangalia ili tuone namna ya kuweza kutatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tunazo changamoto za kisheria, kuna *agreements* mbalimbali ambazo zipo. Kwa hiyo, ni vizuri nazo hizo muendeleo kuziangalia kwa sababu watu wengine wanaendelea kuamini *clearing and forwarding*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulijadili ni *TFDA* na *TBS*. Nakubaliana na *move* iliyopo ya kuhamisha *function* hii kupeleka huku na nyingine kupeleka huku. Changamoto tuliyokuwa nayo kwenye taasisi hizi ilikuwa siyo nani anafanya nini, lakini tatizo tulikuwa na uharaka wa watu kupata *certificate*, kwa kupeleka *function* hii huku na huku, je, uharaka huo tumeupata? Gharama kuwa ndogo, je, ndiyo *move*? Kama *move* ndiyo hiyo mimi nakubaliana

naye lakini kikubwa muda wa kupata *approval* ulikuwa mrefu sana. Mtu anapeleka *sample* yake, inachukua mwaka mmoja, miwili, mitatu kwa hiyo, ningeomba kwamba hilo nalo tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *circle* hii ya Serikali kujadili hizi kodi za Afrika Mashariki. Tunapoletewa kwenye Kamati yetu ya Bajeti kodi nyingine za Afrika Mashariki zinakuwa zimeshafanyiwa mchakato na Waziri, tunakuwa sisi sasa hatuna namna ya kwenda kuibadilisha. Kwa hiyo, ningetamani tuone kwamba aidha Sheria yetu ya Bajeti iweze kuwa *reviewed* ili tuweze kuona wakati gani Kamati ya Bajeti ya Bunge ina-*intervene* kabla hizo sheria hazijawa *approved*. Kwa sababu zikiletwa hapa Bunge tuna *rubber stamp* kwa vitu ambavyo hatuwezi kubadilisha. Kwa hiyo, naona tupate *avenue* ya kubadilisha Sheria yetu ya Bajeti ili kuwe na *avenue* ya Kamati ya Bajeti ku-*intervene* kabla hizi sheria au hizi tozo hazijawa *imposed* kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine kwa kweli naishukuru Wizara tumeenda vizuri na mengine yote imerekebisha vizuri kama ilivyo kwenye *addendum* zake. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja waende wakachape kazi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Edward Mwalongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye *Finance Bill* ambayo tunaendelea kujadili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme mambo machache sana, nianze na suala la vitambulisho. Vitambulisho vya wajasiriamali ni muhimu sana na vimesaidia sana wajasiriamali wengi kuwa na utaratibu mzuri wa kufanya biashara zao. Hata hivyo, Serikali imetuahidi kwamba itatoa Waraka, naomba sana watakapokuwa wanatoa huo

Waraka waangalie jambo moja la muhimu sana. Katika kodi zote ambazo tunalipa kupitia mishahara kuna kodi ya *Pay As You Earn*, wanaolipa ni wale tu ambao mishahara yao iko juu ya kima cha chini na hata wenye mishahara juu ya kima cha chini huwa inaondolewa kiwango cha kima cha chini cha mishahara halafu kiwango kinachobakia ndicho kinachotozwa kodi. Kwa hiyo, ningepomba sana hata kwa hawa wajasiriamali...

T A A R I F A

MHE. SULEIMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwalongo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bungara.

MHE. SULEIMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana msemaji anayesema sasa hivi kwa kuunga mkono kwamba vitambulisho vya wajasiriamali virekebishwe. Nachomuunga mkono yeye Serikali kabla hatujatoka katika kikao hiki Wabunge wote tupewe orodha za wajasiriamali kwa kuwa waliahidi. Kabla hatujatoka Bungeni hapa tupate hiyo orodha.

Kwa hiyo, ninampongeza sana lakini ni vema wote tupate hizo orodha kama tulivyoahidiwa. Kwa hiyo, nakupongeza sana kijana wewe unaweza kuwa Waziri siyo Ubunge tu. Ahsante sana. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna muda huwa mnapenda masihara hivi lakini taarifa kwa mujibu wa kanuni zetu si kwa ajili ya kupongezana moja, lakini la pili taarifa siyo kwa ajili ya kuunga mkono anachozungumza mtu. Ndiyo maana huwa tunapigiana makofi kama unaunga mkono, siyo hoja ya kusimama ili umwambie unamuunga mkono la siyo tutakuwa hatumalizi michango huu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwalongo, endelea.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuliweka sawa hilo, naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu uko mkanganyiko mkubwa sana wa utoaji wa hivi vitambulisho kwenye maeneo yetu na umezua taharuki kubwa sana. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ilianganalie suala hili mapema na kama Serikali ilivyotuahidi kwamba italeti Waraka hapa utakaokuwa unaelekeza kwa sababu ziko kada ambazo zinapewa hivi vitambulisho au zinapaswa kupewa vitambulisho lakini ukianganalia kipato chao kiko chini ya kima cha chini cha mshahara ambao Serikali imeweka kama ndiyo kima cha chini cha Mtanzania kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningeomba nirejee kwenye kodi ambazo kwenye *Finance Bill* iliyopita tuliweza kuzijadili hapa, kodi ya majengo. Tulisema nyumba zinazotowza kodi ya majengo ni nyumba zote zilizoko kwenye miji lakini imetokea kwamba ziko Halmashauri za miji kwa mfano Halmashauri ya Mji wa Njombe, ni Halmashauri ya Mji lakini ina vijiji kata kumi. Sasa unapokwenda kutoza kodi ya nyumba kwenye vijiji vilivyoko ndani ya Halmashauri ya Mji kidogo inaleta shida. Mimi naomba sana Serikali ilianganalie suala hili kwamba tuko tayari kulipa kodi hii ya nyumba kwenye Mji wetu wa Njombe na Mitaa ya Njombe na mitaa iliyoko vijijini yenye sifa ya mitaa lakini kwenye vijiji vilivyoko ndani ya mji, yaani vilivyoko ndani ya utawala wa Halmashauri ya Mji inaleta shida sana kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tabia ya wananchi wa vijijini watashindwa hata kujenga nyumba kwa uwoga tu kwamba nikijenga nyumba nzuri wataniletea kodi. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali ilianganalie suala hili na nafikiri ni busara ya kawaida kabisa kama ni kijijini, sawa eneo la utawala linasema ni ndani ya Halmashauri ya Mji, lakini pale mahali ni kijijini kabisa. Kwenye Halmashauri yangu ya Mji Njombe Vijiji kama vile vya Mamongolo, Ng'elamo vipo zaidi ya kilometa 90 toka Njombe Mjini ambavyo kwa kweli ni vijiji kabisa. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ilianganalie hili na iweze kutoa

maelekezo kwa *TRA* kwamba maeneo ya vijijini hata kama yako ndani ya utawala wa Halmashauri ya Mji waweze kuona namna gani wanaweza wakasaidia kuwafanya hawa wananchi waweze kuishi bila kulipa hiyo kodi ya majengo kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la wigo wa kodi. Hapa tunalalamika sana juu ya mapato ya Serikali na mapato mbalimbali kwa ajili ya kuiwezesha Serikali yetu kufanya kazi vizuri. Wakati wa mchango wangu nilitoa ushauri kwamba Serikali iangalie namna gani itaweza sasa kuzipa majukumu taasisi zote za Serikali kwa maana ya Wizara zote za Serikali kuhakikisha kwamba zinakuwa na kitengo maalum kinachosimamia ajira kwenye sekta binafsi kwa sababu Wizara nyingi zimekuwa zenyewe sasa badala ya kukuza sekta binafsi ili ajira ikue ili tuweze kupata *Pay As You Earn*, zimekuwa hazijishughulishi kabisa na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake zinavuruga kule kwenye sekta binafsi na kwa kuwa hazina jukumu la msingi la kuhakikisha kwamba mapato kupitia *Pay As You Earn* kutoka sekta binafsi yanakuwa ndiyo maana zinakuwa hazisimamii na zinaweza zikavuruga kabisa. Nilitoa mfano juu ya baadhi ya sekta za Serikali ambazo zinafanya shughuli kama hiyo.

Kwa hiyo, ningepomba sana Serikali ijitahidi sana itengeneze utaratibu rasmi ambao utasaidia sasa kuhakikisha kwamba kila Wizara, Idara ya Serikali kama kuna shughuli ya aina hiyo inafanywa na sekta binafsi basi iwekewe utaratibu rasmi ili iweze kuhakikisha kwamba na yenyewe inachangia na kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, Njombe tunapenda sana kulipa kodi na tuko tayari kulipa kodi lakini jengo letu la *TRA* kwa kweli linasikitisha sana. Ilikuwa ni kama vile nyumba ya kuishi au ilikuwa ni ofisi ndogo tu ya Mamlaka ya Pareto miaka hiyo na sasa ndiyo *TRA* Mkoa. Kwanza jengo ni dogo, limechakaa, linavuja lakini pia watumishi ni wachache sana. Wananchi wanakwenda pale kulipa kodi

wanasubiri siku mbili yaani mwananchi yupo tayari kulipa kodi lakini anasubiria siku mbili msongamano ulioko ndani ya *TRA* ili alipe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri nafikiri unanisikia, muangalie jengo la *TRA* Njombe mhakikishe kwamba Njombe wanapata jengo zuri na wanaweza kutoa huduma vizuri kwa wananchi. Maana haipendezi unaenda kulipa kodi halafu unapoteza na muda tena pale badala ya kwenda kufanya kazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, tutamalizia na Mheshimiwa Ali King.

MHE. ZUBERI A. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kwenye hii *Finance Bill* ya mwaka huu. Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa mimi uwezo jioni hii nisimame nitoe mchango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoweza kusimamia maendeleo na kuhakikisha rasilimali za nchi yetu zinawanufaisha watu wote. Jambo kubwa ambalo haliwezi kupingika, jambo alilokuja nalo kuhusu vitambulisho vya wajasiriamali ni muhimu sana, ni ubunifu mkubwa sana na inasaidia sana kupunguza kero mbalimbali ambazo walikuwa wanazipata wajasiriamali wetu wadogowadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye jambo hili, naomba nitoe ushauri kwamba ugawaji wa vitambulisho hivi ni vizuri vikazingatia takwimu ya wajasiriamali wa mahali walipo kwa sababu zipo sehemu za pembezoni kabisa, wilaya au mkoa ya pembezoni vitambulisho vimegawiwa kiasi

kwamba hata uwiano wa wajasiriamali wa mahali pale unakuwa haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi ukienda Dar-es-Salaam (Kinondoni) vitambulisho vinatafutwa na havionekani lakini ukienda vijijini huko, Ifaraka ndani ndani au Mlimba huko, utakuta kuna wajasiriamali wanapewa mpaka wauza matango, ni kwa sababu tu Mkuu wa Wilaya anavyo vile vitambulisho hakuna wa kuwagawia. Kwa hiyo, zingechukuliwa takwimu sahihi kwamba hivi vitambulisho tunapeleka wilaya gani na kule tunategemea kupata wajasiriamali kiasi gani, lakini wazo la vitambulisho vya wajasiriamali ni zuri sana, ni kuboresha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Wabunge wenzangu, hakuna mwanadamu akapanga jambo likakosa changamoto. Changamoto ndio chachu ya maendeleo, kwa sababu pasingekuwa na kitu kinaitwa uboreshaji pasingekuwa na changamoto, uboresha mahali ambapo umepata changamoto. Kwa hiyo, jambo hili ninalipogeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nawapongeza sana Wizara kwa namna wanavyokwenda kuvilinda viwanda vyetu vya ndani. Hapohapo kwenye kulinda viwanda vya ndani, naomba nitoe mchango wangu lazima Wizara waangalie kwamba gharama ya uzalishaji wa viwanda vyetu vya ndani ni kubwa sana kiasi kwamba tunapokwenda kusema tunaenda kuweka ushuru kwenye bidhaa za nje ili kulinda viwanda vyetu vya ndani tunaweza tuka-*create scarcity* ya bidhaa hio hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kiutaalam mimi ni msindikaji wa nafaka, nimeshashuhudia jambo hili mara nyingi sana. Nitoe mfano mmoja, gharama ya kusindika ngano Tanzania mtu anashindwa kujenga kiwanda cha ngano nje ya Dar-es-Salaam kwa sababu tu hajawekewa *exemption* ya gharama ya usafirishaji wa malighafi kutoka Bandarini Dar-es-Salaam labda kuipeleka Mwanza au Mbeya. Mtu akijenga kiwanda Mbeya hawezi ku-*compete*

na mzalishaji wa Dar-es-Salaam, lakini mtu aliyejenga kiwanda Uganda, malighafi ikapitia Bandari hii ya Dar-es-Salaam ana uwezo wa ku-*compete* na mzalishaji wa Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili hata mimi linanipa kutofahamu kidogo kwa sababu inawezekana vipi malighafi ipitie Dar-es-Salaam inakwenda Uganda, inachakatwa kule inaletwa Tanzania ana-*compete* na mzalishaji mwenye kiwanda Dar-es-Salaam lakini malighafi hiyohiyo huwezi kujenga kiwanda Mbeya kwa sababu utashindwa ku-*compete* na mzalishaji wa Dar es Salaam? Hapo naomba Serikali Serikali ijaribu kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo hili ndiyo linalofanya viwanda vingi vijengwe Dar es Salaam hasa vile viwanda ambavyo tunategemea malighafi labda nusu yake inatoka nje ya Tanzania yaani tuna-*import*. Maana yake viwanda hivi huwezi kuvijenga nje ya Dar es Salaam ambapo ipo bandari kwa sababu gani? Ukivijenga Mbeya au Mwanza huwezi ku-*compete* na mzalishaji wa Dar es Salaam kwa sababu Serikali haijafikiria gharama za usafirishaji wa malighafi kutoka Dar es Salaam kupeleka Mbeya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hilo naomba Serikali walichukue na waliangalie kama kweli tuna nia, kwa mfano hapa wamesema kwamba Wakuu wa Mikoa wameagizwa wafungue viwanda kwenye mikoa yao. Utawezaje kufungua kiwanda ambacho labda nusu ya malighafi inabidi uagize kutoka nje. Ukikijenga nje ya Dar es Salaam, gharama hii ya usafirishaji ile bidhaa utashindwa kuiuza. Kwa hiyo, naomba Serikali ije na utaratibu iangalie namna ya kuviwezesha viwanda hivi kuvipanua pengine viwanda hivi vijengwe hata nje ya Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka niongelee suala la hizi bidhaa (*transit goods*). Mara nyingi, kama nilivyosema mimi ni msindikaji wa nafaka, nimeshafanya kazi zaidi ya miaka 25 kwenye kampuni ya watu binafsi kwenye sekta binafsi. Mnufaika mkubwa wa

transit goods ni wafanyakazi wa *TRA* wale wasio waaminifu, hawa ndiyo wanaonufaika sana na hizi *transit goods* na huwezi kuwaondoa asilimia 100 wafanyakazi wasio waaminifu *TRA*. Sasa naomba Serikali ije na utaratibu tunafanyaje? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja, kuna mwaka mmoja, mwaka kama 2005 hivi palikuwa na *scarcity* kubwa sana ya nafaka. Serikali kwa makusudi ikaamua kwamba nafaka zote ziondolewe ushuru na kweli zikaondolewa ushuru, lakini *products* zake hazikuweza kushuka. Kwa hiyo, ni nani walikuwa wanufaika wakubwa? Wanufaika wakubwa walikuwa wafanyabiashara na watu wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupunguza ushuru kwa lengo la kuwanufaisha wananchi, lakini bado kwenye ufuatiliaji na usimamizi kwamba, je, kile ambacho tumeondoa ushuru, manufaa haya kwa wananchi yamefika? Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na kitengo mahsusi cha kufuatilia hizi nafuu za kodi zinafikaje kwa walengwa. Vinginevyo tutaendelea kuwanufaisha wale ambao ni wafanyakazi/watendaji wa *TRA* na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nitoe mchango wangu kama alivyochangia mchangiaji aliyepita kwamba kuna usumbufu mkubwa sana kwenye ofisi za *TRA*. Yaani mtu ni mlipakodi anakwenda kupeleka fedha kwenye taasisi ya Serikali halafu anasumbuliwa utafikiri yeye ndiyo anakwenda kuomba kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili linapunguza vilevile morali ya watu kulipa kodi kwa sababu mfanyabiashara anatakiwa apange siku kwamba leo ni siku ya kwenda *TRA*, ina maana kama ni duka afunge, kama ni kiwanda kisimame, yeye anakwenda kulipa kodi *TRA*. Jambo hili ni jambo ambalo wanatakiwa waliangalie sana, jambo la kuliondoa. Jambo hili vilevile linapunguza hata wawekezaji,

wengi linawakatisha tamaa pale wanapopata usumbufu wanapohitaji huduma hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo tu mawili, nilitaka niyatolee ufafanunuzi katika mchango wangu wa leo. Vinginevyo naunga sana mkono hoja ya Serikali. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, tutamalizia na Mheshimiwa Ali King. Hayupo, Mheshimiwa Ali King.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kuja kuchangia sheria hii ya masuala ya kodi (*Finance Act*) kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita katika *points* kama nne; *point* moja ambayo imezungumzwa na watu wengi, lakini mtemewa mate na wengi huloa, nami nitarejea tena, *sanitary pads*. Kwanza tunaipongeza sana Serikali kwa kutanua wigo katika kutoa msamaha kwenye makampuni ambayo yapo tokea mapema pamoja na yale makampuni mapya kwa miaka miwilimiwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kushauri Serikali ingeendelea na ule msamaha ambao ulikuwepo mwaka jana kwa sababu inasemekana kwamba haukusomeka vizuri. Watu wangeuelewa kidogokidogo basi tungefika katika hatua nzuri, lakini kwa kukatiza pale ina maana ile faida haijapatikana kwa sababu wamefaidika watu wachache. Hatua ya kutangaza kwamba watu waelewe kwamba kumetoka msamaha ingefuatwa, basi nahisi tungefikia mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachotaka kuchangia, ni *competitiveness* ya viwanda vya ndani, kumudu ushindani. Kwanza naipongeza Serikali kwa hatua za kikodi ambazo zimechukuliwa katika hii *Finance Bill*

ambazo zinakwenda kunufaisha viwanda vyetu vya ndani na vitakuwa vinaleta ushindani. Hata hivyo, nataka nitoe angalizo moja au nishauri kwenye sehemu moja, kuna viwanda vya ndani hasa vya nondo kwamba viwanda hivi sheria zake nyingine ili zibadilishike kuna mahusiano ya kikanda kama vile ni *SADC*. Kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue hatua hizi za haraka kwa sababu viwanda hivi vya nondo na tuna miradi mingi ndani inaweza ikatusaidia hata katika kukuza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumza ni uhakika wa takwimu zinazohusika katika kutoa maamuzi haya ya kikodi. Maamuzi ya kikodi wakati mwingine tunatoa lakini takwimu tunazotumia siyo sahihi. Tumekaa na wadau wazalishaji wamesema kwamba mahitaji ni tani 570,000 lakini wao wamezalisha tani 210,000, upungufu ulikuwa ni tani 360,000 lakini bado tukaona kwamba tuweke kodi zaidi katika mafuta ambayo yanaingia ndani. Sasa hapa mimi nina wasiwasi kama kuna mchezo mbaya tunachezewa na wenzetu na mchezo huu hakuna anayeucheza ni majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwa sababu tani 210,000 hizi 360,000 kwa taarifa ya Waziri tumesema kwamba tumepunguza *import* ya mafuta ya kula kwa asilimia 94. Sasa kama tumepunguza kwa asilimia 94 hizi 360,000 zimepitia wapi? Wakati wazalishaji wenyewe wanasema kwamba wanahitaji kutumia tani 3,000 kwa kuzalisha lakini wanatumia 2,000 ina maana kwamba bado hatujaweza kumudu. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali ijaribu kutumia takwimu sahihi vinginevyo tutakuja kupata magendo. Magendo yanakuja wala hayalindwi kwa bunduki, magendo tunaweza tukayalinda kwa sera, kwa hiyo tuwe na sera nzuri ambazo tutumie takwimu sahihi ili kupunguza haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza sana Serikali, hili ndiyo jambo langu la mwisho. Serikali naipongeza kwa kuweka *zero rate* katika umeme unaotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar, tunaishukuru sana hapa Serikali, lakini pia

Serikali ijaribu kuangalia katika *zero rate* iliyowekwa katika bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na zinazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Naipongeza hatua ile ya kufikiria kwamba tuweke *zero rate* ni sawa lakini tutizame ilikuwa tunakinga tatizo gani? Pale mwanzo tulikuwa na sheria ambayo inaruhusu marejesho ya mwaka 1997, sheria ile ya marejesho ilikuwa tatizo ni kurejeshheana. Sasa tatizo kama ilikuwa ni kurejeshheana ilikuwa tuweke sheria ya kurejeshheana lakini tukaweka kwenye *zero rate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulipoweka kwenye *zero rate* tukaanzisha changamoto nyingine mbili kwamba sheria inavyotaka, sheria inataka kwamba ni lazima bidhaa zitoke kwa *manufacturer* na siyo rahisi kwamba watu wote wanaweza kwenda kununua kwa *manufacturer*. Ukisema unanunua kwa *manufacturer* ina maana wewe ni lazima uwe mfanyabiashara mkubwa sana. Isitoshe sheria ikasema huyu mtu lazima awe *VAT registered* na *ZRB*, siyo wote wanaokuwa *VAT registered* na *ZRB*. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto ya pili ambayo sisi tulifikiri kwamba ingekuwa dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mshairi mmoja anasema kwenye msitari mmoja tu anasema dawa imekuwa sumu nimeila midomoni. Ulifikiria ni dawa lakini kumbe sasa dawa imegeuka imekuwa sumu, hii imekuwa sumu; tuelekee wapi? Basi turudi kwenye marejesho kwa sababu kwenye marejesho lile tatizo linarekebishika kirahisi na kwenye marejesho basi tufungue *ESCROW Account* katika tatizo hili husika ili kusiwe na kigugumizi katika kurejeshheana. Hilo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili; basi tuwe na sheria kama ilivyokuwa *proposed*, lakini tuongeze isiwe kutoka kwa *manufacturer* peke yake, lakini pia isiwe kwamba mtu lazima awe *VAT registered*, lakini tukiiweka vizuri na tukaweka kwamba ni lazima kwamba *customs entry point* zetu ziwepo kwamba ile *entry* itakuwa inaonekana kote. lkiwekwa kwenye *entry* kwa mtu ambaye ananunua ina maana kwamba hapo hataweza mtu kukimbia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali ijaribu kutathmini, itazame changamoto ile ya mwanzo na iliyopo sasa hivi ipi kubwa. Hivi sasa hivi malori mengi sana utasikia kwamba yamepakia bia zinataka kusafirishwa kupelekwa Zanzibar lakini ukitazama hao wanywaji wa bia huko Zanzibar na hizo tani ambazo zinakuja zikazunguka humuhumu hazifiki kule, lakini tukiweka hii *entry*, tukiingiza kwenye *entry* itaonekana kote kwa sababu tunatumia mfumo mmoja.

Kwa hiyo, naishauri Serikali ijaribu kuweka hii *custom entry* ambayo itakuwa inaonesha bidhaa inapokwenda na zile zilizotoka zote zitakuwa zinaoneshwa, ikiwa pagumu hapo hatuwezi kutoka, turudie ya zamani, hayakuwa mabaya sana kiasi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa michango kwa siku ya leo na kabla hatujaahirisha nimepewa taarifa moja lakini nafuatilia *Hansard* inasemaje, kwa hiyo nitatoa maelekezo kesho kuhusu maneno ambayo kuna uwezekano kwamba yametumika katika mmoja wa Wabunge wakati akichangia hapa na simtaji kusudi kwa sababu ni mpaka nisome *Hansard* huenda hakuna hayo maneno au kama yapo nitayatolea maelekezo siku ya kesho.

Jambo lingine, kuna mchangiaji kabla hatujasitisha shughuli za Bunge mchana alizungumza kuhusu kupata nakala za *blueprint*, sasa taarifa niliyonayo ni kwamba kwa hapa Dodoma zipo nakala chache na Katibu atazipokea hizo nakala chache zilizopo, nakala 50. Zingine zitawekwa maktaba wale na ataweka utaratibu mzuri Katibu, Wabunge ziwapate vipi, lakini nyingine zitakuja kwa ajili ya Wabunge wote. Kama kutakuwa na uwezekano basi zikifika kabla hatujaahirisha Bunge basi Ijumaa wote mtagawiwa, lakini kama haikuwa hivyo taarifa kwa sasa zitakuwepo nakala kwenye maktaba yetu ya Bunge, kwa hiyo mnaweza kupita pale kuzitazama na hizo nakala chache Katibu ataziwekea utaratibu ili ziwafikie Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa mchango hapa lakini sina uwezo wa kuusoma tena nikiwa nimesimama, kwa hiyo kama nilivyosema nitatoa mwongozo wa jambo hilo siku ya kesho. Katibu ananiambia kuna tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa kitabu cha *Tanzania Starting Business Procedures* ambacho kimechambua taratibu zote za kupata vibali kwenye Taasisi za Serikali wakati wa kufungua biashara kipo nje ya Ukumbi wa Msekwa kinauzwa Sh.20,000/=. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kununua kitabu hicho ili muweze kusoma na kujua taratibu mbalimbali za kupata vibali vya kuanzisha biashara na pengine mnaweza kuwashauri na wapiga kura namna ya kufungua biashara na taratibu zinazotakiwa.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili.

(Saa 1.33 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 27 Juni, 2019, Saa Tatu Asubuhi)